# Nipashe

Jumanne Aprili 16, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579893

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



Nipashe
TESA
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI
Je, wajua? Tembe za uzazi wa mpango kwa wanaume zapita jaribio la awali
Mnyamakale mwingine apatikana Rukwa, jina lake latolewa kitaaluma, si Kiswahili
Wazazi, walezi wilayani Mbeya wanyooshewa kidole cha lawama

UKURASA 13



## Mtoto auawa kwa panga kitandani akiwa na mama

UKURASA 3



# CAG Assad bado gumzo

**JINAMIZI** lake bado latanda bungeni, vyama vinane vyatoa tamko zito, mjadala wazidi kushika kasi mitandaoni... *ukurasa wa 2*



## TRA yakusanya trl. 11.9/- miezi tisa

UKURASA 3




Baadhi ya viongozi wa vyama vinane vya siasa wakisaini tamko la pamoja jijini Dar es Salaam jana, walitangaza kufungua kesi katika Mahakama ya Afrika ya Mashariki (EACJ), kupinga Sheria ya Vyama vya Siasa namba 1 ya Mwaka 2019. Pia walizungumzia sakata la Spika wa Bunge, Job Ndugai na CAG, Prof. Mussa Assad. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wabunge upinzani wahoji kauli ya Mkuu wa Majeshi

UKURASA 3


SPECIAL FEATURE ON INDUSTRIALIZATION DEVELOPMENT IN TANZANIA

"NCHI YA VIWANDA"





The Guardian Ltd, through its Leading Newspapers, The Guardian and Nipashe in collaboration with CTI will publish special supplement focusing on Industrialization Development in Tanzania, phase one on 18th April 2019.



We are inviting The Government and Private Institutions to participate in this special feature.



Contact:

Moses Masunga,
Email:moses.masunga@guardian.co.tz,
Phone No.0755 642851,



Charles Masele,
Email:masele7@gmail.com,
Phone No.0789 637363.

The Guardian Nipashe CTI


MICHEZO SIMBA, YANGA ZATANGAZA VITA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# CAG Assad bado gumzo bungeni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

UAMUZI wa Bunge kutofanya kazi na Prof. Mussa Assad (pichani), Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), limeendelea kuwa gumzo bungeni, safari hii chombo hicho cha kutunga sheria kikitangaza kufuatilia habari iliyoandikwa na moja ya magazeti ya kila siku kuhusu suala hilo.

Mara tu baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni jana asubuhi, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika (Chadema), alisimama na kuomba kutoa hoja Bunge lijadili kile alichoeleza gazeti hilo limeingilia haki za Bunge kufuatia kuchapisha habari yenye kichwa "Bunge lamtupa CAG".

Mnyika ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Tanzania Bara, alisema kilichoandikwa na gazeti hilo kinakinzana na azimio la Bunge la kutofanya kazi na Prof. Assad.



Huku akieleza kuwa hana uhakika kama wabunge wote wamelisoma gazeti hilo na kubaini ukweli wa kinacholalamikiwa na Mnyika, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyekuwa anaongoza kikao cha Bunge, alimpa dakika tatu mbunge huyo kueleza msingi wa hoja yake.

Mnyika alisema toleo la juzi la gazeti hilo liliandika habari yenye kichwa "Bunge lamtupa CAG" na kueleza kuwa chombo hicho cha kutunga sheria kimemtaka Prof. Assad akajieleze kwa Rais John Magufuli.

"Ninachofahamu Bunge halijawahi kuazimia jambo kama hili, kilichoazimiwa na Bunge ni kutofanyakazi na CAG na siyo kumtaka akajieleze kwa Rais Magufuli. Habari hii imeingilia haki za Bunge," Mnyika alisema.

Baada ya Mnyika kujenga hoja yake, Naibu Spika (Dk. Tulia) alisema hana uhakika kama habari hiyo imeandikwa kwa kuingilia haki za Bunge na si wabunge wote wameisoma.

Kiongozi huyo wa Bunge alisema hoja ya Mnyika itafanyiwa utaratibu wa kawaida kwa kulipitia gazeti hilo kisha wabunge watajulishwa kama kuna kifungu cha Sheria ya Kinga na Madaraka ya Bunge kilichovunjwa.

INAENDELEA UK 8

## ...Mnyukano washika kasi mtandaoni

**Na Mary Geofrey**

MNYUKANO unaoendelea baina ya Spika wa Bunge, Job Ndugai na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, umehamia mitandaoni ambako watu wanaendelea kuzua mijadala kila kona.

Ikiwa imepita siku moja tu tangu Ndugai amshauri Prof. Assad kujipeleka kwa Rais John Magufuli akajieleze kwamba alikosea kuliita Bunge dhaifu, watu mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii wameonekana kukosoa hatua hiyo.

Ripoti ya CAG ya ukaguzi wa mwaka 2017/2018 iliwasilishwa bungeni Jumatano iliyopita na baadaye kuzungumza na kuiwasilisha kwa vyombo vya habari inayoonyesha 'madudu' yaliyobainika katika sekta za umma.

Wadau mbalimbali kwenye makundi ya Whatsapp, Instagram na Facebook wameeleza kuwa Spika amejichanganya kwa sababu kuna madudu ambayo CAG ameyabaini na ameshaeleza msimamo wake kuhusu 'udhaifu' aliouelezea kwa Bunge hilo.

INAENDELEA UK 8



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli na Makamu Mwenyekiti wa CCM, Visiwani, Rais Dk. Ali Mohamed Shein, wakitoka kwenye kikao cha Kamati Kuu (NEC), Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na muda ni kuanzia saa nne asubuhi. Mnada huo utaendeshwa na Madalali tajwa hapo chini kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZNIA LTD**

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| Hamida Mohamed Aley | Kiwanja/ Banda | Tandika-Mtaa Nyambwera | 27/04/2019 | Emashi Auctioneer |
| Ridhiwan K. Kyella/ Jonadhan Shirima) | Nyumba | Mbagala – Kibondemaji B | 04/05/2019 | Tausi A/Mart |
| Nisile Boazi Mwakajumba | Nyumba | Majohe - Kichangani | 04/05/2019 | Champion A/Mart |
| Haji Khamis Juma (Sanifa Shio) | Nyumba | Kibangu- Mtaa Mwongozo | 27/04/2019 | Champion A/Mart |
| Aidan Bernard Ndaona | Nyumba | Kitunda- Mtaa wa Kibeberu | 02/05/2019 | Emashi Auctioneer |
| David Teu Mbijiri ( Peter M. Mokoro) | Nyumba | Nata-Mugumu Serengeti | 30/04/2019 | Maseto Auctioneer |
| Peter John Peter | Kiwanja | Nyasura-Bunda | 02/05/2019 | Maseto Auctioneer |
| Pendo Samson Zoka | Kiwanja | Nyasura C-Bunda | 03/05/2019 | Maseto Auctioneer |
| Asha Hamis Kulwa | Kiwanja | Migongani-Bunda | 03/05/2019 | Maseto Auctioneer |
| Asha Hamis Kulwa | Kiwanja | Majengo-Bunda | 02/05/2019 | Maseto Auctioneer |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki zitakuwa juu ya Mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na;-**
**TUJIJENGE TANZANIA LTD**
**Emashi Auctioneer:0784208575; MOB:0767340054/0677001054 (Bunda)**
**Tausi A/Mart: 0719351040 ; /0718068335 (HQ).**
**Champion Auctioneer: 0654200448/0756761328.**

215181102


# Vyama 8 vyamvaa Ndugai

**Na Romana Mallya**

SAKATA la Spika wa Bunge, Job Ndugai na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, limeviibua vyama nane vya upinzani ambavyo vimemtaka Spika Ndugai ajiuzulu.

Vyama hivyo ambavyo vimeungana na sasa kutambuliwa kama Umoja wa Ushirikiano wa Vyama vya Upinzani ni Chadema, ACT-Wazalendo, NCCR-Mageuzi, DP, Chauma, UPDP, CCK na NLD.

Akitoa msimamo kwa niaba ya vyama hivyo jana, jijini Dar es Salaam, baada ya kukutana na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Taifa wa UPDP, Fahmi Dovutwa, alisema kitendo cha Ndugai kimesababisha mkanganyiko mkubwa baada ya kumtaka Prof. Assad aende kumwomba radhi Rais John Magufuli kutokana na mgogoro uliopo.

"Spika anataka kumchanganya Rais kwenye mgogoro wake, kitendo cha kumwingiza na kuligombanisha Bunge na Ofisi ya Rais maana yake Spika Ndugai ameshindwa kazi ajiuzulu," alisema.

"Labda Spika atuambie anataka Rais afanye nini, kinyume chake mambo kama hayo madogo ma-

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Wabunge upinzani wahoji kauli ya Mkuu wa Majeshi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wa upinzani, wamehoji bungeni kauli iliyotolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Mabeyo, kuhusu jeshi kufuatilia wanaotoa kauli zenye lengo la kuvuruga amani ya nchi.

Juzi, wakati Rais John Magufuli akizindua mji wa kiserikali Mtumba jijini Dodoma, Jenerali Mabeyo alisema jeshi linafuatilia kauli tata zenye lengo la kuleta uchochezi na kuvuruga amani ya nchi.

Wakichangia makadirio ya wizara mbili zilizoko chini ya Ofisi ya Rais (Tamisemi na Utumishi) kwa mwaka ujao wa fedha, baadhi ya wabunge wa upinzani walihoji sababu za Jenerali Mabeyo kutoa kauli hiyo wakidai si jukumu lake.

Mbunge wa Mbozi, Pascal Haonga (Chadema), alisema Jenerali Mabeyo hakupaswa kutoa kauli hiyo kwa kuwa ufuatiliaji wa wachochezi unafanywa na Jeshi la Polisi, hivyo ilipaswa kutolewa na mkuu wa jeshi hilo.

Mbunge wa Mlimba, Susan Kiwanga (Chadema), alihoji sababu za Mkuu wa Majeshi kuchunguza mambo ya uchochezi wa wanasiasa.

"Tumesikia kwenye vyombo vya habari kuwa Mkuu wa Majeshi anachunguza kauli za uchochezi zinazohatarisha amani. Sasa watu wa utawala bora nataka mnijibu, Mkuu wa Majeshi amekuwa DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka)? Nakemea kwa nguvu zote na ashindwe kwa jina la Yesu," Kiwanga alisema.

Wakati mbunge huyo akiendelea kuchangia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri, Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisimama kuomba kutoa taarifa bungeni.

Alipopewa nafasi hiyo, Mhagama ambaye pia ni Mnadhimu wa Serikali Bungeni, alisema Jenerali Mabeyo hakusema anawachunguza wanasiasa.

"Mheshimiwa Naibu Spika, alichozungumzia CDF (Mkuu wa Majeshi) ni masuala ya amani, ulinzi na usalama kwa ujumla. Hakusema wanasiasa, hili lazima tuliweke sawa," Mhagama alisema.

Kutokana na kauli hiyo ya Mhagama, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, ambaye alikuwa akiongoza kikao hicho cha Bunge, aliwataka wabunge wasitoe kauli ambazo hawana uhakika nazo.

"Tuwe waangalifu. Wakati mwingine tusitoe kauli ambazo hatuna uhakika nazo kwa sababu siku hiyo (Jumamosi) hata mimi nilikuwapo na (Jenerali Mabeyo) alisema wanafuatilia siyo wanachunguza," Dk. Tulia alisema.

Katika mchango wake kuhusu hoja ya makadirio ya bajeti ya wizara hizo mbili, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tamisemi, Mwita Waitara, alisema kama kuna chokochoko zenye kuashiria uvunjifu wa amani zi-

INAENDELEA UK 4



Mchuuzi wa nyama ya kuku akiuza kitoweo hicho, katika mazingira hatarishi kiafya, huku nzi wakiwa wamekizingira, jirani na Soko la Kinondoni B, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## TRA yakusanya trilioni 11/- kwa miezi tisa

**Na Enock Charles**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imefanikiwa kukusanya Sh. trilioni 11.96 katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2018/19 kuanzia Julai mwaka jana na Machi, mwaka huu.

Akizungumza katika makao makuu ya mamlaka hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipa Kodi, Richard Kayombo, alisema lengo la mamlaka hiyo ni kukusanya Sh. trilioni 18.1 kwa mwaka wa fedha 2018/19.

"Katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2018/19 TRA ilifanikiwa kukusanya Sh. trilioni 1.30 kwa mwezi wa Januari, Sh. trilioni 1.23 kwa mwezi wa Februari na kiasi cha Sh. Trilioni 1.43 kwa mwezi Machi 2019," Kayombo alisema.

Alisema mamlaka hiyo kwa sasa ina walipa kodi wapatao 2,800,000 nchi nzima na imeweka utaratibu wa kurahisisha upatikanaji wa namba ya utambulisho wa mlipa kodi TIN kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), TIN inaweza kutolewa katika ofisi zote za TRA katika ngazi ya mkoa na wilaya baada ya mwombaji kuwasilisha kitambulisho cha Taifa.

"Zamani ilikuwa lazima uje mkoani, lakini kwa sasa TIN inaweza kutolewa katika ofisi zote za TRA katika ngazi za mkoa na hata za wilaya," Kayombo alisema.

Akifafanua zaidi alisema makusanyo hayo kwa miezi tisa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 ni Sh. trilioni 1.2 kwa mwezi Julai 2018, Sh. trilioni 1.2 kwa mwezi Agosti 2018, Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi Septemba 2018 na Sh. trilioni 1.2 kwa mwezi Oktoba 2018.

Ilisema Sh. trilioni 1.2 zilipatikana mwezi Novemba 2018, Sh. trilioni 1.6 kwa mwezi Desemba

INAENDELEA UK 8

# Mtoto auawa kwa panga kitandani akiwa na mama

**Na Paul William,** MWANGA

MWANAFUNZI wa darasa la pili wa Shule ya Msingi Mbambua Kata ya Lembeni wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro, Sarafina William (8), ameuawa kikatili kwa kukatwa panga shingoni akiwa amelala kitandani na mama yake mzazi.

Haya hivyo, mama mzazi wa marehemu hakujeruhiwa na waliotekeleza mauaji hayo. Habari zilizopatikana na kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Hamisi Issah, zinaeleza watu watatu ambao hawakujulikana ndio waliotekeleza mauaji hayo usiku wa manane wa kuamkia Jumapili.

Inadaiwa mama mzazi wa mtoto huyo, Salome William, akiwa amelala na mwanae nyumbani kwake, ghafla waliona mwanga na wakati wakijiuliza mwanga huo unatoka wapi, ndipo watu hao watatu walipoingia ndani na kumpiga panga shingoni mtoto huyo.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, watu hao walimkata na panga mtoto huyo shingoni upande wa kushoto na kumsababishia jeraha kubwa, ambalo wakati anakimbizwa Hospitali ya Rufani ya KCMC, alifikwa na mauti njiani.

"Mtoto huyo kutokana na jeraha kubwa alilokuwa amelipata shingoni, hakuweza kufika Hospitali ya KCMC, badala yake alifia njiani, na mwili wake umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali hiyo kusubiri uchunguzi wa kitabibu," alieleza Kamanda Issah.

Aidha, Kamanda Issah alisema jeshi hilo linamshikilia mama mmoja (jina linahifadhiwa), kuhusiana na tukio hilo, huku uchunguzi zaidi ukiendelea ili kuwabaini wote waliohusika na tukio hilo.

Katika tukio jingine lililotokea Aprili 13, mwaka huu, majira ya saa 9:00 za usiku, Sofia Hamisi (32), aliuwa kwa kunyongwa na mtu anayetambulika kwa sura.

Kamanda Issah alisema tukio hilo lilitokea maeneo ya Longuo 'A' Manispaa ya Moshi, ambapo mwili wa marehemu huyo ulikutwa umelala chini, huku akiwa ameng'ata ulimi na shingoni kukiwa na mikwaruzo ya kucha.

Alisema walipoingia chumbani kwake walikuta kikionyesha kama kulikuwa na upekuzi uliofanyika katika droo za kabati na chini walikuta mipira ya kondomu ambazo zilikuwa zimeshatumika.

Alidai mwanamume huyo alifika katika eneo la Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Tiba cha KCMCo kilichopo ndani ya Hospitali ya Rufani ya KCMC na alipofika getini alijitambulisha ni mwanafunzi wa chuo hicho na kufanikiwa kuingia ndani ya chuo kisha kuruka ukuta na kutokomea kusikojulikana.

Mwili wa mwanamke huyo umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya KCMC.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 15/04/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe **17/04/2019** kampuni ya **SINO SHINE OVERSEAS CONSTRUCTION AND INVESTMENT EAST AFRICA** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **KABANGA** kuelekea **SUMBAWANGA** gari hilo lenye namba za usajili:

**T349 BNT/T 646 BCJ.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 20m
Upana - mita 3m
Kimo - mita 2.8m

3. NJia itakayotumika **KABANGA hadi SUMBAWANGA** kupitia **MPANDA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115179302

## TCRA yazionya redio 2 kukiuka agizo la serikali

**Na Beatrice Shayo**

KAMATI ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imetoa onyo kali kwa redio Magic FM na Free Africa kwa kitendo cha kusoma habari za magazeti kwa undani kinyume cha agizo la serikali.

Akisoma uamuzi wa Kamati hiyo baada ya kupitia maelezo ya utetezi kwa redio hizo mbili, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Valerie Msoka, alisema agizo la Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, limezuia kusoma habari kwa undani na badala yake inatakiwa kusomwa vichwa vya habari vya magazeti.

Alisema Kamati iliandika wito kwa uongozi wa Magic FM kuwataka kuwasilisha utetezi wao wa maandishi ni kwa nini wasichukuliwe hatua kwa kukiuka agizo la waziri.

"Katika kipindi chake cha Morning Magic tulikisikiliza kipindi walichokuwa wanapitia magazeti ili kujiridhisha walisoma habari za magazeti kwa undani kinyume cha agizo la serikali," alisema Msoka.

Msoka alisema katika maelezo yao Magic FM ilidai kuwa kosa hilo lilifanywa na uongozi uliopita.

Aliendelea kueleza kuwa ni kweli kipindi kilikiuka agizo la serikali na kwamba uongozi huo mpya hauna rekodi ya kupatiwa barua ya kukiuka agizo la serikali.

Alisema waliomba radhi na kudai kuwa kosa hilo halitajitokeza tena katika uongozi huu mpya watazingatia agizo la serikali.

Aidha, Msoka alisema Kamati yake imebaini kuwa walifanya kosa hilo kwa makusudi na utetezi wao hauna msingi na kwamba kubadilika kwa uongozi siyo sababu ya kuvunja agizo la serikali.

Alisema hata kama uongozi umebadilika wafanyakazi wa Magic ni wale wale, hivyo walitakiwa kuzingatia maagizo yaliyotolewa.

Alisema kutokana na udhaifu uliobainika wanatakiwa kuimarisha na kuboresha usimamizi wa vipindi vyao, wafanye matayarisho ya kutosha ya vipindi vyao na wawe mfano wa kufuata taratibu kutokana na hadhi waliyo nayo kwa sasa.

Aidha, alisema kwa Redio Free Africa walifanya kosa hilo kwa kusoma magazeti kwa undani jambo ambalo halitakiwi.

Alisema katika maelezo yao ya kujitetea, walikiri kosa na kuomba radhi huku wakieleza kuwa mtangazaji aliyetangaza kipindi hicho kwa dharura hakuwa na uzoefu baada ya wale wazoefu kuacha kazi.

"Kamati imebaini kukiukwa agizo la serikali na utetezi wake haukuwa wa msingi. Msimamizi wa kipindi alitakiwa kuwa makini na kumsimamia mtangazaji huyo hata kumkatisha asiendelee kutangaza maana alitumia muda mrefu huku akiwa anasoma habari kwa undani," alisema.

Aidha, Msoka aliishauri Redio Free Africa iimarishe na kuboresha vipindi vyake vya magazeti ili kosa kama hilo lisijirudie.

# CRDB UBA watoa trilioni 1.7/- ujenzi wa stieglers

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB kwa kushirikiana na Benki ya UBA zimetoa Sh. trilioni 1.7 kwa ajili ya kumdhamini mkandarasi katika ujenzi wa mradi wa umeme wa Rufiji wa Stieglers George.

Makubaliano hayo yalifikiwa jana jijini Dar es Salaam mbele ya waandishi wa habari, wawakilishi wa serikali, mkandarasi pamoja na watendaji wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco).

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA, Usman Isiaka, alisema kwa mujibu wa masharti ya mkataba huo, umoja huo unahitajika kutoa dhamana za benki za kigeni na za ndani zikiwa ni Sh. trilioni 1.7 kupitia utekelezaji wa mradi na dhamana ya malipo ya awali kwa mradi huo.

Alisema kwa kuanzia, Benki ya CRDB na UBA zimeshirikiana na Benki ya Africa Export-Import Bank (Afrieximbank) na benki nyingine za Misri kutoa dhamana za benki kwa Tanesco ambazo zilikabidhiwa jana.

Alisema kuwa baada ya kukamilika, mradi huo utazalisha umeme wa megawati 2,100 kuongezwa kwenye gridi ya taifa ambao ni zaidi ya mara mbili ya uwezo wa Tanesco na kusaidia kupunguza tatizo la kukosekana umeme nchini.

"Umeme utakaotokana na mradi huu, utatumia Kilovolti 400 mpya ambao utaunganishwa katika gridi ya umeme ya taifa," alisema.

Alisema serikali ilikuwa ni mikakati ya muda mrefu ya kuanzisha mradi huo wa umeme tangu miaka ya 1960 ambao ukishakamilika utakuwa mradi mkubwa Afrika Mashariki.

Mradi huo unatarajia kuiongezea nguvu serikali kukabiliana na upungufu wa umeme kwa kuwa uchumi wa nchi na idadi ya watu inaongezeka.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akikabidhi hati ya dhamana ya benki kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania, Dk. Tito Mwinuka, ikiwa ni kuunga mkono mradi wa umeme wa maji wa Rufiji mkoani Pwani, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. PICHA: SELEMANI MPOCHI

## DFID yatoa bilioni 14/- kusaidia wakimbizi Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Uingereza kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa (DFID), imetoa msaada wa Dola za Marekani milioni 6.38 (Sawa na Sh. bilioni 14.74) kwa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi Duniani (UNHCR) kusaidia wakimbizi zaidi ya 300,000 waliopo katika kambi za Kigoma Tanzania.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa DFID Tanzania, Beth Arhy ilieleza kuwa msaada huo utasaidia kuimarisha huduma za afya, elimu na maji salama kwa wakimbizi kutoka Burundi na Congo wanaotafuta makazi eneo hilo.

"Msaada huu kutoka serikali ya Uingereza utaendelea kuisaida Serikali ya Tanzania katika juhudi zao za kuwakaribisha wakimbizi wanaozikimbia nchi zao," alisema Arthy.

Alisema Serikali ya Uingereza itaendelea kuwekeza mkoani Kigoma kwa kusaidia shule, miundombinu, maendeleo ya kibiashara pamoja na kuwasaidia wakimbizi kutoka Burundi kurudi nchini kwao.

Naye Mwakilishi wa UNHCR Tanzania, Chansa Kapaya, aliishukuru serikali ya Uingereza kwa hatua ya kushirikiana na UNHCR.

"Msaada utaisaidia juhudi za UNHCR katika kuwasaidia wakimbizi 300,000 mahitaji yao na wale wanaotafuta makazi Tanzania, natanguliza shukrani zangu kwa serikali ya Uingereza kwa kuendelea kuisaidia UNHCR hususani kwenye operesheni Tanzania.

Alisema UNHCR na UK DFID zina historia ya muda mrefu katika kuwasaidia wakimbizi Tanzania, ambapo tangu mwaka 2015 Serikali ya Uingereza kupitia DFID imeshatoa Dola za Marekani milioni 43.3 (Sawa na Sh. bilioni 100.2).

Tanzania ina wakimbizi zaidi ya 300,000 katika kambi tatu eneo la Kigoma, ambapo asilimia 74 kati yao wanatoka Burundi na asilimia 26 wanatoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na nchi zinginezo.

## Upinzani wahoji kauli ya Mkuu wa Majeshi

INATOKA UK 3

nazofanywa na baadhi ya wanasiasa, Jenerali Mabeyo hapaswi kukaa kimya.

"Hivi Mkuu wa Majeshi anayeangalia ulinzi wa nchi hii, hautaki atoe kauli dhidi ya wachochezi?" Waitara alihoji. "Haiwezekani mbunge aseme patachimbika, huu mchezo hauhitaji dakika tisini, wao wapo na sisi tupo. Maneno kama hayo ya uchochezi na fujo, serikali haitayavumilia.

"Nashangaa sana hiyo demokrasia inayozungumzwa, wakati Mch. (Peter) Msigwa alipokuwa akigombea uenyekiti wa kanda wa Chadema, wagombea wote waliondolewa na akapata asilimia 48 ya kura ya hapana.

"Tunataka wanasiasa wa upinzani makini kama (Joseph) Selasini au James Mbatia, wamewasilisha hoja zao vizuri na kwenye maeneo yaliyokuwa na changamoto kama wakuu wa mikoa, tumeshazungumza nao na ile ya mfuko wa jimbo imeshatatuliwa.

"Alikuja Prof. Patrice Lumumba, anasema 'Magufulification of Africa', yaani Rais Magufuli ana sifa ya kuwa kiongozi wa Afrika kupitia miradi ya kimkakati anayoitekeleza."

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (aliyechuchumaa), akimwelekeza jambo Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, alipotembelea miradi ya ujenzi wa barabara, vituo vya afya na masoko, katika maeneo ya jiji hilo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Benki Uingereza yaaahidi makubwa kwa Tanzania

**Na Mwandishi Maalum,**

**WASHINGTON DC**

BENKI ya Credit Suisse ya Uingereza imeahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuikopesha ili kugharamia miradi ya maendeleo baada kuridhishwa na uaminifu wa urejeshaji mikopo kwa wakati.

Benki hiyo pia imesema imechukua uamuzi huo kutokana na kuridhishwa na ubora wa viwango vya miradi inayotekelezwa nchini.

Ahadi hiyo ilitolewa Mjini Washington D.C, Marekani na Mkurugenzi wa Masoko ya Kimataifa wa Benki hiyo, Elizabeth Muchemi, alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, katika mikutano ya kipupwe ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha na Kimataifa (IMF) inayoendelea mjini hapa.

Muchemi alisema uzoefu unaonyesha baadhi ya nchi zinazochukua mikopo hazitekelezi ipasavyo miradi iliyoombewa fedha, jambo ambalo ni tofauti kwa Tanzania ambayo miradi iliyoombewa mkopo inatekelezwa vizuri na kwa viwango.

Hivi karibuni, benki hiyo iliikopesha Tanzania mkopo wa dola za Marekani milioni 200 kwa ajili ya kutekeleza miradi mabalimbali ya maendeleo ikiwamo sekta miundombinu ya barabara na reli.

"Tuko tayari kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kwa kadri Serikali itakavyoona kwa sababu ya mipango mizuri ya Serikali pamoja na kulipa madeni kwa wakati. Benki ya Credit Suisse haijawahi kuwa na tatizo na Tanzania katika urejeshaji wa mikopo, jambo linaloongeza imani kwa Tanzania," alisema Muchemi.

Akizungumza na Muchemi katika Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nchini Marekani, katika kikao kilichohudhuriwa pia na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, Dk. Philip Mpango aliishukuru Benki hiyo kwa utayari wake wa kuendelee kushirikiana na Serikali katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo.

Amesema Taifa limejipanga kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo reli, barabara, umeme, maji, elimu, afya, mradi wa gesi kimiminika (LNG), usafiri wa anga na majini, bandari, elimu, ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania, mradi ambayo inahitaji uwekezaji mkubwa wa rasilimali fedha.

Waziri Mpango alisema Tanzania inataka kutumia uwapo wa nchi zisizopakana na bahari kama Burundi, Uganda, Rwanda, na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) kujenga mtandao wa reli ya kisasa na barabara utakaosaidia kuchochea biashara na kukuza uchumi wa nchi na ukanda huo kwa ujumla.

# Uagizaji gesi mitungi kwa pamoja mbioni

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema iko katika hatua za awali za kuandaa mpango wa uagizaji wa gesi ya mitungi (LPG) kwa pamoja kama ilivyo kwa mafuta ya petroli.

Imesema utaratibu huo utasaidia kudhibiti masuala mbalimbali ikiwamo bei ya gesi hiyo.

Akizungumza wakati wa semina kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyofanyika jijini Dodoma, Waziri wa Nishati, Dk, Medard Kalemani, alisema dhamira ya Serikali ni kuhakikisha wananchi katika maeneo yote nchini wanafikiwa na huduma hiyo, hivyo Serikali itaratibu usambazaji wa gesi hiyo badala ya kuwaachia wauzaji wenyewe kuamua maeneo wanayotaka kupeleka gesi.

"Serikali ikitangaza bei elekezi kulingana na soko, itawafanya wauzaji wafuate bei hiyo badala ya wao kujipangia, hii itasaidia wananchi kuuziwa gesi kwa gharama inayofanana katika maeneo mbalimbali ambapo gesi hiyo itauzwa." alisema Dk. Kalemani.

Alieleza kuwa suala la sasa la kila muuzaji kujiamulia sehemu anayotaka kupeleka gesi inafanya maeneo mengine kukosa kabisa nishati hiyo, hivyo Serikali itaweza kuwadhibiti wauzaji na kuhakikisha kuwa maeneo yote nchini yanafikishiwa gesi.

Aliongeza kuwa, utaratibu wa kuagiza gesi inayotumika majumbani kwa pamoja utasaidia taifa kutambua kiwango halisi cha gesi kinachohitajika nchini na kiasi cha gesi kinachoingizwa nchini, hivyo kusaidia pia katika shughuli za ukusanyaji wa mapato.

Akitoa taarifa kwa Wajumbe wa Kamati hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Erasto Simon, alisema Wakala huo kwa sasa unafanya tathmini ya namna bora ya kuanza uagizaji wa pamoja wa gesi ya mitungi kwa kuzingatia maoni kutoka kwa wadau.

Akizungumzia faida mbalimbali zinazotokana na uagizaji wa mafuta wa pamoja, Simon alisema ni kuweka mazingira sawa ya kibiashara kwa kuwa gharama za uagizaji wa mafuta ziko sawa kwa makampuni yote nchini na kuondoa mianya ya rushwa katika uagizaji wa mafuta kwa sababu ufunguzi wa zabuni hufanyika kwa uwazi na washiriki wote huridhika na matokeo ya zabuni.

Faida nyingine ni taifa kuwa na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta kwa muda wote na kuwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi za mafuta zinazosaidia katika ukusanyaji wa mapato na kupanga bei elekezi ya mafuta.

Aliongeza kuwa, mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja umewezesha nchi kudhibiti ubora wa mafuta yanayoingia nchini na pia kuongezeka kwa sehemu za kupokelea mafuta kama bandari ya Tanga na Mtwara, tofauti na ilivyokuwa awali kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam ndiyo ilikuwa ikitumika kwa shughuli hizo.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Hatua ya HESLB ni ya kupongeza*

**BODI** ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeanza kuendesha programu za elimu kwa wanafunzi wa shule za sekondari waliopo mikoani ili kuwaelimisha kuhusu sifa na taratibu za kuomba mikopo kwa usahihi.

Hatua hii muhimu imetangazwa na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, juzi wakati akizungumza na wanafunzi 1,166 wa kidato cha sita kutoka shule zote 12 za wilayani Maswa, mkoani Simiyu.

Ni hatua muhimu kwa sababu uendeshaji wa programu hizo unalenga kuondokana na changamoto wanazopata wanafunzi wakati wa kuomba mikopo ya elimu ya juu.

HESLB ilianza kuendesha programu hizo katika mkoa wa Dar es Salaam.

Mkurugenzi huyo katika maelezo yake alieleza kuwa programu hiyo imeanzishwa kutokana na maoni mbalimbali ya wadau kuhusu kuzikabili changamoto hizo ambazo zimekuwa ni kero kwa wengi.

Tunatambua kuwa mikopo hiyo hutolewa ili kuwawezesha wanafunzi wengi wanaotoka katika familia maskini kumudu gharama za masomo na malazi, wakati wanapokuwa katika jitihada zao za kutimiza ndoto zao za kufuzu masomo ya fani mbalimbali.

Kwa miaka kadhaa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya waombaji wa mikopo hiyo, hivyo tunaamini kwa elimu hii itasaida kupunguza kama si kuondoa kabisa changamoto zinazosababisha hali hiyo.

Taarifa zilizopo HESLB zinabainisha kuwa waombaji wa mikopo zaidi ya 57,000 ambao walipata udahili vyuoni mwaka wa masomo 2018/2019, maombi zaidi ya 9,000 yalikuwa na upungufu mkubwa.

Sasa katika program hiyo inaonyesha baadhi ya mambo ambayo yalionekana kuwasumbua waombaji wengi ni pamoja na wanafunzi kutoelewa sifa za kuomba mkopo huo.

Hivyo pamoja na mambo mengine sasa kupitia programu hiyo, wamejuzwa pia nyaraka zipi muhimu zinazotakiwa, namna ya kuomba na kuwasilisha kwa usahihi maombi hayo kwa njia ya mtandao.

Pia jinsi gani wanavyopaswa kuzingatia utaratibu na umuhimu wa kurejesha mkopo mara wamalizapo masomo.

Upungufu huo ni pamoja na kukosa nyaraka kama vyeti vya kuzaliwa, vitambulisho sahihi vya wadhamini, kutosainiwa na waombaji, wadhamini au serikali za mitaa au vijiji.

Tunaamini kwamba wanafunzi husika watahakikisha wanasoma kwa makini mwongozo utakaotolewa na HESLB ambao unaelezea jinsi ya kuomba mkopo huo hatua kwa hatua.

Jambo la kufurahisha ni kwamba HESLB wamechukua hatua hiyo wakati mwafaka kwa kuwa mwezi Mei wanafunzi wa kidato cha sita wataanza kufanya mitihani yao ya taifa ikiwa ni hatua ya kusaka tiketi ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Tunawasisitiza HESLB kuvuta kasi zaidi ili kuwafikia wanafunzi wote wenye sifa za kuomba mikopo hiyo, tukiamini kwamba itasaidia kuongeza idadi ya wasomi nchini.

Kuna faida kubwa ya kuongeza wasomi nchini, kwani watasaidia katika kuvuta kasi ya maendeleo kwa kufanikisha hamasa ya Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli ya kuwa nchi ya uchumi wa kati kupotoa ujenzi wa viwanda.

Tusipojipanga vyema kwa kuhakikisha tunazalisha wasomi wa kutosha tutaishia kuajiri wageni kwenye viwanda tunavyovijenga, hivyo HESLB vuteni kasi kupambana na changamoto hizo.

Ni matarajio yetu kuwa bodi hiyo itakuwa inachukua hatua za haraka kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika utoaji wa mikopo kama ilivyofanya kwa kutoa elimu hiyo katika shule za sekondari.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tuzo maalumu kwa walimu ziandaliwe ili kuwatia moyo

**KATI** ya kazi zenye changamoto nyingi ni ya ualimu.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba walimu wamekuwa wakikumbana na kila adha kwenye maisha yao ya kila siku.

Unaweza kukuta shule ina wanafunzi zaidi ya 200, lakini ina walimu wachache wasioweza kumudu wingi huo.

Hata hivyo, utakuta wanachapa kazi kama kawaida kwa vile wanatambua kazi yao ni ya wito.

Kwa kifupi walimu ni watumishi wanaokabiliwa na changamoto nyingi katika utekelezaji wa majukumu yao, ingawaje kuna baadhi ya wenzetu ambao wamekuwa wakiwaona kama si wa muhimu kwa jamii.

Ninaposema baadhi ya watu wanaiona kazi hiyo si ya muhimu, maana yangu ni kwamba wapo wanaowadharau na kuwaona wa kawaida na ndio maana kuna walimu waliowahi kuchapwa viboko hadharani.

Iliwahi kuripotiwa katika vyombo vya habari kuwa baadhi ya watu walikusanyika eneo la wazi na kuwachapa walimu mbele ya wanafunzi, wakiwatuhumu kuwapa adhabu watoto wao.

Tukio hili liliripotiwa kutokea kwenye moja ya mikoa ya kanda ya ziwa Viktoria, ambapo waliotumika kuwachapa walimu walikuwa ni walinzi wa jadi (sungusungu).

Changamoto za walimu hazishii hapo tu, kuna matukio ya mambo ya kishirikina ambayo wamekuwa wakidai kukumbana nayo katika maeneo ya kazi yao hadi kufikia kuomba uhamisho.

Kwa mazingira kama hayo na mengine ambayo yamekuwa yakiripotiwa ni wazi kuwa yanawakatisha tamaa, na ndiyo maana nasema kazi ya ualimu ina changamoto nyingi.

Muungwana anaona kuwa ni vyema basi kwa jamii kuwaheshimu, ili kuwatia moyo wafanye kazi yao kwa bidii pamoja na changamoto nyingi wanazokutana nazo.

Jamii iache maneno ya kejeli kwa walimu hawa, kwani wana umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya nchi, ingawa baadhi ya wenzetu, huwaona kama hawana lolote.

Ualimu ni taaluma muhimu na ya kuheshimiwa! hebu fikiria kwamba mtoto anaanza shule akiwa hajui kusoma na kuandika, lakini mwalimu anamsaidia kwa kila hali ili kuhakikisha anajua kusoma na kuandika.

Uandaaji wa watoto kitabia, kimaadili na kitaaluma ni kazi ya wito na ni ngumu ambayo inahitaji kuungwa mkono na jamii ili iweze kutoa matunda bora ya ustawi wa jamii.

Hivyo, inasikitisha pale mtaalamu huyu anapodharauliwa! Siyo vizuri kabisa.

Wale wanaodharau walimu watambue kuwa viongozi na watu wenye nafasi mbalimbali za uongozi wametoka kwa walimu hao hao kuanzia wale wa shule za msingi, hivyo heshima kwao ni muhimu sana.

Na nidhamu hujengwa kati ya walimu na wanafunzi na ndio maana miaka ya nyuma mwanafunzi akikutana na mwalimu njiani alikuwa akimpokea mzigo na kuufikisha kule mwalimu anakokwenda.

Cha kushangaza siku hizi heshima kama hiyo haipo tena, si wanafunzi wala wazazi, baadhi yao wanaona walimu kama si lolote kwao ndio maana wanafikia hatua hata ya kuwatukana au kuwaadhibu hadharani.

Ni rai ya Muungwana kwamba kama njia ya kuwamotisha walimu, wadau na serikali waanzishe tuzo maalumu ya kuenzi kazi nzuri inayofanywa na kada hiyo kwa ustawi wa taifa letu.

Hiyo ni kutokana na uvumilivu wao kwa kazi wanayoifanya katika mazingira magumu kama bila ya kuchoka.

Inaweza ikawa ni tuzo ambayo walimu wataishindania lakini lengo kubwa liwe ni kutambua na kuthamini kazi kubwa wanayoifanya ingawa ni katika mazingira magumu.

Tuzo za aina hiyo zinaweza kuwaongezea ari ya kufanya kazi yao kwa bidii wakitambua kuwa nyuma yao kuna watu wanathamini mchango wao katika maendeleo ya elimu nchini.

Hatua hii inaweza kusaidia kubadili mawazo ya hata wale ambao wamekuwa wakiwadharau walimu ili watambue kazi kubwa zinazofanywa na kundi hilo ambalo ni nguzo ya maendeleo ya kielimu kwa kila Mtanzania.

# Takukuru yataka mabaraza kata kupatiwa elimu

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

MABARAZA ya kata mkoani Kagera yametakiwa kupatiwa elimu ya utendaji na jinsi wanavyotakiwa kuyaendesha ili kuepuka ukiukwaji wa haki za binadamu.

Wito huo ulitolewa na Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kagera, Siabo Omary, wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi kwa mwaka wa fedha 2018|2019 kwa vyombo vya habari mjini Bukoba kuanzia mwezi Januari na Machi, mwaka huu.

Omary alisema Takukuru imebaini kuwapo kwa ukiukwaji mkubwa kwenye uendeshaji wa baraza za kata hasa katika kipengele cha gharama.

"Viongozi wa manispaa na halmashauri mkoani hapa wanapaswa kurekebisha kasoro zinazobainika kwenye vipengele vya gharama za mabaraza, kufungua mashauri, gharama za kutembelea eneo la tukio," alisema Omary.

"Kupata nakala ya hukumu na hata faini mabaraza yanatoza kiwango jinsi wanavyojisikia wakati wanapopata matatizo ya wananchi," alieleza Omary.

Aidha, alisema kwa kupindi cha mwezi Januari hadi Machi, mwaka huu takwimu za uchunguzi uliofanywa na Takukuru zinaonyesha kupokea malalamiko 188.

Alisema katika malalamiko hayo yalipokelewa, yaliyokamilika na uchunguzi ni 17, kesi zilizofunguliwa mahakamani ni tisa, zilizoshindwa ni nne zilizoshinda ni tatu.

Aliendelea kueleza idara na sekta husika zikiwamo Tamisemi, Mahakama, Polisi, Ardhi, Mifuko ya hifadhi ya jamii na Bima pamoja na elimu ni maeneo yanayolalamikiwa zaidi.

Jitihada za ufuatiliaji wa fedha za miradi ya maendeleo zinaendelea kufanyika na kuwa mkoa huo kuna ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Karagwe, Bukoba na Kyerwa.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 1.5 umebainiwa kuwa na matumizi tofauti na makusudio kwa wasimamizi kutumia vibaya.

"Tumebaini baadhi ya mapungufu kwenye miradi ya ujenzi wa hospitali mfano muundo wa kamati za ujenzi kwa baadhi ya wilaya haukufuata taratibu zinazotakiwa mfano mwenyekiti wa kamati ya ujenzi kuwa afisa ugavi badala ya mhandisi wa wilaya," alisema Omary.



Watalii kutoka Ulaya wakielekea Forodhani mjini Zanzibar jana, kupanda boti kuelekea kisiwa kidogo cha Changu kuangalia kobe wanaohifadhiwa hapo. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Marekani yaipa TZ bil. 26.5/- mradi wa afya

**Na Dege Masoli, TANGA**

MFUKO wa dharura wa Rais wa Serikali ya Marekani U.S. President's Emergency Plan for Aids Relief (PEPFAR) umeipatia Serikali ya Tanzania Dola milioni 11.9 (sawa na Sh. bilioni 26.5) kwa ajili ya mradi wa Afya Kamilifu unaendeshwa na Amref, Mkoa wa Tanga na Zanzibar.

Akitoa taarifa ya mradi huo kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga kabla ya uzinduzi wa mradi huo jana jijini hapa, Mkurugenzi wa Amref Health Africa, Dk. Florence Temu, alieleza kuwa mradi huo mpya umelenga kupanua juhudi za kutoa huduma za matunzo na matibabu ya kufubaza VVU Visiwani Zanzibar na Mkoa wa Tanga.

Dk. Temu alisema mradi huo wa miaka mitano unaungana na juhudi zinazoendelea duniani zenye lengo la kumaliza janga la Ukimwi ifikapo mwaka 2030 ikiwamo kupunguza mzigo wa nchi wa VVU na Ukimwi.

Utafiti wa athari za Ukimwi nchini Tanzania (THIS) wa 2016/2017 unaonyesha kuenea kwa asilimia tano kwa watu wa umri wa miaka 15-64.

"Hii inashabihiana na takwimu zinazoonyesha kwamba nchini Tanzania kuna watu takribani million 1.4 wanaoishi na VVU wenye miaka 15-64.

Zaidi ya hayo utafiti unaonyesha ukandamizaji wa mzigo wa virusi katika makundi rika nchini Tanzania ni asilimia 52," alisema Dk. Temu.

Alieleza kuwa mradi huo uliopewa jina la 'Afya Kamilifu' unafadhiliwa na mpango wa dharura wa Rais wa Marekani wa msaada katika kupambana na Ukimwi (PEPFAR) kupitia kituo cha kudhibiti magonjwa Centre for Disease Control (CDC) kilichopo nchini Tanzania.

Akitambulisha mradi huo, Dk. Edwin Kilimba, alieleza kuwa moja ya malengo ya mradi huo ni kuona uwezekano wa kuongeza muda wa utoaji wa dawa ya kufubaza VVU kwa wanaochukua kutoka mwezi mmoja wa sasa hadi kufikia miezi mitatu hadi sita.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella, alilishukuru Shirika la Amref kwa kuona umuhimu wa mradi huo kufanyika Tanga na kwamba umefika wakati muafaka ambao kuna changamoto kubwa ya maambukizi ya VVU.

Shigella alieleza tatizo la dhana ya unyanyapaa kwa wenye maambukizi kuwa bado ni kubwa ndani ya jamii kudhani maambukizi hayo yanatokana na kufanya ngono pekee na kuwaomba viongozi wa dini wanasiasa na makongamano mbalimbali mkoani humo kuwa na ajenda maalumu ya kuielimisha jamii umuhimu wakupima na athari za kuwanyanyapaa wagonjwa.

## Sababu kuporomoka tumbaku zaanikwa

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Stanley Mnozya, amesema uzalishaji wa zao hilo unaendelea kushuka kila mwaka kutokana na changamoto mbalimbali.

Miongoni mwa changamoto hizo ni wakulima kutong'oa mabua mashambani ambayo yamekuwa yakibaki na wadudu waharibifu.

Mnozya aliyasema hayo juzi wilayani Kahama kwenye semina ya ufunguzi wa mkutano uliokuwa kwa madhumuni ya kutathmini utekelezaji wa shughuli za uzalishaji na masoko ya zao hilo msimu uliopita ili kubaini ufikiwaji wa malengo, matatizo yaliyojitokeza na kupima mwelekeo kufahamu wingi na ubora.

Alisema changamoto ya sekta ya tumbaku ni kushuka kwa uzalishaji, ambapo msimu 2013/2014 wakulima walizalisha kilo milioni 105, na msimu 2014/2015 kilo 93,2015/2016, msimu 2016/2017 kilo milioni 60 na 2017/208 kilo milioni 50.5 Aidha, inasababishwa na kupungua kwa uhitaji wa tumbaku kwenye soko la dunia kwa kupinga kuongezeka kwa uzalishaji na matumizi ya bidhaa za tumbaku duniani, ambapo kwenye msimu wa mauzo utakaoanza mwaka huu kampuni za ununuzi zimeingia mkataba na wakulima kununua kilo 56.5. Mnozya alisema uzalishaji kwa zao la tumbaku umeonekana kushuka kila mwaka kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo wakulima kutong'oa mabua mashambani ambayo yamekuwa yakibaki na wadudu waharibifu wanapoanza msimu huingia kwenye zao jipya na ushambulia.

"Mnozya alisema kuwa changamoto ya kutong'oa mabua (magugu) mashambani imeanza kujitokeza kwa wadudu waharibifu wa zao la tumbaku wanaobaki kwenye mabua, hivyo kuongezeka kwa gharama za uzalishaji hata dawa ikinyunyuziwa kushindwa kuua wadudu hao," alisema Mnozya.

Hata hivyo alisema kuwa ushauri umekuwa ukitolewa kwa wakulima wang'oe mabua ili waondokane na athari ya utumiaji gharama kubwa katika uzalishaji. "Bodi ya Tumbaku na wadau ilifanya tathmini kwenye mashamba ya wakulima kwa kukagua miche ikiwa bado shambani, miundombinu iliyotumika, idadi ya stoo za kutunzia tumbaku na mapokezi ya pembejeo za kukaushia," aliongeza.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Wilaya ya Kahama(Kacu), Emanuel Charahani, alisema kuwa wapo kwenye mikakati ya kuhamasisha wakulima kuondoa mabua mashambani ili kuzalisha tumbaku yenye ubora na tija itakayoshindanishwa kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi. Katibu Tawala Wilaya ya Kahama, Timothy Ndanya, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, alisema ili kukabiliana na changamoto hizo, hakunabudi kuanzisha sheria ndogo zitakazowabana wakulima kung'oa magugu na kufuata taratibu zingine za zao hilo zilizowekwa.

# Vyama 8 vyamvaa Spika Ndugai

INATOKA UK 2

dogo kama aliona hasikilizwi, nadhani angejishusha yeye katika uspika, hiyo ndiyo hulka ya Watanzania," alisisitiza Dovutwa kwa niaba ya vyama nane.

Alisema viongozi wengi duniani wanapoona jambo lao halisikilizwi huwa wanashuka na siyo kugombanisha taasisi ili kutafuta huruma.

"Namtaka CAG asimame na msimamo wake, wananchi na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tuko pamoja naye, kile ambacho Spika kwa utashi wake ameona kimemkera, akereke kushuka katika jukwaa la uspika bungeni," alisema.

Alisema taifa linaingizwa katika msukosuko bila sababu za msingi na kwamba mgogoro unaoendelea umesababishwa na utashi wa Spika mwenyewe.

"Hatua ya kumkataa CAG ni jambo ambalo utekelezaji wake una utata kwa sababu Bunge linapaswa lisikilize na kupokea hoja zilizotolewa kwenye ripoti ya Prof. Assad na kuzifanyia kazi badala ya kuhangaika kupambana naye," alisema.

Alisema Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliamini na alikuwa muda mwingi akisisitiza viongozi wakubali kukosolewa na wasijisikie vibaya wanapokosolewa.

"Madhara ya msimamo wa Spika Ndugai ni makubwa sana, leo wamemkataa CAG kesho kukiwa na shauri mahakamani wanaweza kuleta hoja ya kumkataa Jaji Kiongozi, kesho kutwa wanaweza kuleta hoja ya kumkataa IGP na mwisho wa siku anaweza kuleta hoja ya kumkataa Mkuu wa Majeshi, taifa litaendaje katika mazingira haya, taifa halikulelewa katika misingi hii," alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, alisema siyo tu Spika ajiuzulu bali yapo mambo mengi ya msingi katika taifa yalitakiwa kufikiwa maamuzi magumu.

Akizungumzia kuhusu Sheria ya Vyama vya Siasa namba 1 ya mwaka 2019, ambayo imeanza kutumika mwaka huu, Mbowe alisema umoja huo wa vyama vya upinzani umeamua kufungua kesi katika Mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ) kuipinga.

Sheria hiyo ilisainiwa na Rais Magufuli Februari 13, na kuchapwa kwenye Gazeti la Serikali Februari 22.

Mbowe alisema kesi hiyo imesajiliwa katika mahakama, ambacho ndicho chombo cha juu chenye wajibu wa kutafsiri sheria na kuonyesha haki kutendeka.

"Kesi yetu imepewa namba 3 ya mwaka 2019 na walalamikaji ni Freeman Mbowe na wenzake wanne dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Tanzania," alisema.

Alitaja msingi wa shauri hilo ni kwamba Sheria namba 1 ya mwaka 2019 iliyotungwa kubadili na kuongeza vifungu kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa ni mbovu na inakiuka misingi ya uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Sheria hiyo inakiuka misingi ya uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki husani Ibara ya 6, 7 na 8 ya mkataba huo wa kuanzishwa jumuiya hiyo," alisema.

Alisema katika maombi yao wameiomba mahakama hiyo itamke kwamba vifungu wanavyovilalamikia havina hadhi ya kisheria.

Alisema maombi hayo yamepokelewa mahakamani na Mwansheria Mkuu wa Serikali amepewa siku 45 kujibu maombi hayo.

Alisema wameamua kuitafuta haki mahakamani kutokana na ukweli kuwa sheria hiyo ni mbaya ambayo inafanya shughuli za kisiasa kuwa jinai.

Mbowe alisema mbali ya ukiukaji wa mkataba wa EAC, vifungu vya sheria hiyo vinakiuka katiba na misingi ya utawala bora pamoja na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Tanzania imeitia saini.

Akizungumzia kanuni za uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi za serikali za mitaa kwa niaba ya umoja huo, Katibu Mkuu wa CCK, Renatus Muhabi, alisema walitoa maoni yao Dodoma na kuomba mapendekezo hayo waliyotoa wayapate mapema ili kuona kama maeneo yote waliyokuwa na mashaka nayo, yamefanyiwa kazi.

"Tunaiomba serikali ituletee mapitio ya kanuni ili waone ni maeneo gani yarekebishwe kama wanufaika," alisema.



Mjasiriamali Sara Jabula (kushoto), akiwahudumia juisi wateja wake, katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mnyukano washika kasi mtandaoni

INATOKA UK 2

"Spika Ndugai anajichukia, anajiogopa. Anasema watu wakisoma sana na kuitwa maprofesa wanadharau wengine. Hapa anasema Profesa Assad anamdharau kwa sababu ya uprofesa," alisema mmoja wa watu waliochangia kupitia ukurasa wa Facebook.

Mchangiaji mwingine Twitter alieleza kuwa Spika Ndugai amemwingiza Rais John Magufuli kwenye mgogoro huo ama kwa kujua au kutokujua.

"Katika taarifa yake, Spika anamtaka CAG amwombe radhi Rais Magufuli na kama atamsamehe Bunge nalo liko tayari kumsamehe. Hii inamaanisha kuwa tatizo halipo kwa Spika na Bunge bali lipo kwa Rais jambo ambalo si sahihi," alisema.

Mchangiaji huyo alisema Spika Ndugai anaposema Rais ni sehemu ya Bunge anakosea kwa sababu si wakati wote bali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Nchi, Rais ni sehemu ya Bunge pale linapokaa kutunga sheria.

Alisema Rais si sehemu ya Bunge linapokaa kwenye shughuli za kuisimamia serikali kwa niaba ya wananchi.

Naye mchangiaji mwingine kupitia ukurasa wa Instagram, alisema kupitia Bunge kuna kikundi cha watu wenye kuunga mkono serikali.

"Hili Bunge limepokea taarifa ya CAG yenye jina la Profesa Assad na picha yake na saini yake, lakini limegoma kuijadili. Sasa wanataka wawe kikundi cha kusifu tu, hapana," alisema.

Mwingine alidai kuwa kiti cha Spika ni dhaifu na kutojadili taarifa ya CAG ni kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia serikali.

Alisema Spika Ndugai anataka ubadhirifu unaotajwa kwenye taarifa ya CAG upuuzwe kwa sababu Profesa Assad katumia neno moja tu la kiswahili 'dhaifu'.

Alisema CAG ni taasisi inayojisimamia na hakuna haja ya Bunge ambalo ni muhimili unaojitegemea kuanza kupambana naye kwa kauli ambayo haina madhara kwa serikali.

Mchangiaji mwingine alisema Bunge limeshatoa maazimio yake kuwa halitafanya kazi na CAG, hivyo hakukuwa na haja ya Spika kuibuka tena na kuanza kushauri kuhusu hatua zinazotakiwa kuchukuliwa.

Alisema wakati CAG akikabidhi kwa Rais John Magufuli ripoti yake ya mwaka 2016/17, Rais alimwagiza CAG akafanye ukaguzi wa uhakika katika taasisi na idara zote za serikali ili kubaini madudu na hicho ndicho kilichofanyika.

"Badala ya Spika kumpongeza CAG kwa kazi aliyoifanya ya kubaini madudu mengi, yeye ameng'ang'ania hoja moja ambayo alishaifunga kwa azimio la Bunge," alisema mchangiaji huyo.

**ATAKA SULUHU IPATIKANE**

Mwananchi mmoja aliyejitambulisha kwa jina la Robert Mnyone, ametoa maoni yake akitaka suluhu baina ya Bunge na ofisi ya CAG ipatikane kwa kuwa malumbano yanayoendelea hivi sasa hayatakuwa na mshindi.

"Watanzania wote sasa tunafahamu kuwa kumetokea mgogoro wa kiutendaji kati ya Bunge na CAG. Vyombo vyote, yaani Bunge na CAG ni muhimu kiutendaji ndani ya serikali, hivyo nadhani si jambo la busara kwa wananchi kukaa kimya pembeni wakingojea kusikia leo Bunge linamwambia nini CAG na kesho CAG naye analijibu nini Bunge.

"Kusipokuwa na ushirikiano mzuri kati ya Bunge na CAG maana yake ni uzorotaji wa madhumuni yaliyosababisha vyombo hivi vikaundwa kikatiba," alisema.

Kwa mujibu wa Mnyone, hadhi ya vyombo hivyo ni ya juu kikatiba ikizingatiwa kuwa Rais ni sehemu ya Bunge, hivyo ni vyema wakuu wa nchi wastaafu, mawaziri wakuu wastaafu, majaji wakuu wastaafu wakisaidiwa na viongozi wa dini, wachukue jukumu la kuvipatanisha kabla mgogoro huo haujasababisha madhara makubwa kitaifa.

"Napendekeza hivyo kwa kuwa CAG wa sasa akiondolewa madarakani kwa msingi wa huu, mgogoro utasababisha kumfunga mdomo CAG mpya atakayeteuliwa na hilo likitokea, madhara yake kwa taifa ni makubwa," alisisitiza.

## TRA yakusanya trilioni 11/-

INATOKA UK 3

2018, Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi Januari 2019, Sh. trilioni 1.2 kwa mwezi Februari 2019 na Sh. 1.4 kwa mwezi Machi 2019.

Mamlaka hiyo iliwaonya wote wanaojishughulisha kughushi risiti za kielektroniki za EFD kwa kuwa ni kinyume cha sheria za nchi na imewataka wamiliki wote wa majengo nchini kujitokeza kulipia kodi za majengo haraka ili kuepuka usumbufu.

## CAG Assad bado gumzo

INATOKA UK 2

Aprili 2, mwaka huu, Bunge liliazimia kutofanya kazi na CAG Assad baada ya Kamati yake ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kumtia hatiani kutokana na kauli yake ya mwanzoni mwa mwaka jijini Newyork, Marekani kwamba anafikiri "huo ni udhaifu wa Bunge".

Prof. Assad alifika mbele ya kamati hiyo kuhojiwa na akasisitiza neno 'udhaifu' lililolalamikiwa, si tatizo kwa kuwa katika lugha yao ya kiuhasibu linamaanisha 'upungufu'.

Kwa mujibu wa kamati hiyo, Prof. Assad hakuwa tayari kujutia wala kuomba radhi kwa kulitumia neno 'udhaifu' dhidi ya Bunge na alisisitiza ataendelea kulitumia.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari ofisi kwake jijini Dodoma Jumatano iliyopita, Prof. Assad alisisitiza atendelea kulitumia neno 'udhaifu'.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka 2017/18, Prof. Assad pia amelitumia neno hilo dhidi ya taasisi mbalimbali ambazo alibaini zina dosari katika hesabu zake.

# Kampeni kuuwisha Msitu Pugu rasmi

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Wilaya ya Kisarawe, umeanza kampeni ya kuuwisha Hifadhi ya Msitu Pugu ambayo inadaiwa miaka ya 2000 iliharibiwa na wavamizi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kazi maalum ya upandaji miti, Kaimu Meneja wa TFS Kisarawe, Nanzia Shedula, alisema msitu huo ulikuwa umeharibiwa vibaya.

Alisema wameanza kampeni hiyo baada ya kufanikiwa kudhibiti wavamizi hao kwa kutumia vikosi maalum vya ulinzi kwa kushirikiana na maofisa wa wakala huo.

"Kipindi cha nyuma hali ya uvamizi na uharibifu wa misitu ilikuwa kubwa na ya kutisha sana, wananchi walikuwa wanaingia na kufanya uharibifu wa kila aina na hata kuichoma kabisa na msitu uliharibika na miti mingi ilipotea na hii ni kwa sababu misitu yetu imezungukwa na watu," alisema Shedula. Alisema lengo la kampeni hiyo ni kuhakikisha msitu huo unarudi katika hali yake ya awali na ikiwezekana kuuboresha zaidi.

Ofisa Misitu, Ugavi na Uenezi wa TFS, Shabani Kiula, alisema juhudi kubwa inayofanywa na wakala huo ni kuhakikisha inalinda kwa nguvu zote hifadhi zote za misitu nchini na kuiboresha zaidi ili iendelee kuwa na tija kwa taifa.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Ashton Media, Abbas Hirji, alisema wameamua kushirikiana na wakala huo kutoa elimu juu ya umuhimu wa misitu wake.

"Ukitaka kuona kwamba, watu wanaharibu misitu uwe kwenye ndege ndiyo utaona uchungu, na hawajui umuhimu wake, kwa hiyo sisi tukaona kwamba tushirikiane nao kuwaelimisha wananchi katika mikoa mbalimbali juu ya umuhimu wake," alisema Hirji.



Baadhi ya washiriki wakifuatilia mada kwenye mafunzo ya kuwajengea vijana uwezo katika kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye soko la ajira yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kwa kushirikiana na Kampuni ya Shell Tanzania mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Waelekezwa fursa za kujiajiri

**Na Enock Charles**

VIJANA wametakiwa kuchangamkia fursa zilizopo ili kujikwamua kiuchumi badala ya kukaa kusubiri ajira kutoka taasisi za serikali na mashirika binafsi.

Akizungumza katika warsha ya 24 ya watafiti wa masuala ya uchumi iliyowakutanisha watunga sera na viongozi wa serikali za mitaa iliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umaskini (Repoa), Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Agrey Mwanri, aliwataka vijana kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao ili kujikwamua kiuchumi.

"Tutatoa mikopo kwa ajili ya vijana, ila tunataka tusikie wanafanya nini? Opportunity are never given, they are taken (fursa hazitolewi bali zinachukuliwa)," Mwanri alisema.

"Mtu mvua ikinyesha anashangilia mvua mvua mvua, lakini unamuuliza una tikiti 'hapana', una muhogo 'hapana', sasa unashangilia nini?" Mwanri alihoji.

Alisema kazi ya serikali ni kujenga mazingira mazuri ili vijana wayatumie katika kujikwamua kiuchumi, na kwamba jukumu kubwa zaidi ni la wananchi wenyewe kuangalia mazingira yao na kuchangamkia fursa zilizopo na kutokutarajia watu wengine kufikiri zaidi kwa niaba yao.

Alieleza kuwa Serikali Mkoa wa Tabora inafanya jitihada za kuhakikisha fedha iliyoelekezwa katika kutengwa kwa ajili ya makundi maalum inatengwa kama ilivyoelekezwa ili kuwakwamua wananchi kiuchumi.

"Sasa hivi tunakwenda kwenye azimio la Kaliua, tumezungumzia sasa utaratibu ambao unahakikisha kundi hili la vijana linapata hiyo asilimia nne na kundi la kinamama linapata asilimia nne na kundi la walemavu linapata asilimia nne," Mwanri alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustin Kamuzora, alishauri kuangaliwa upya kwa mfumo wa elimu nchini tofauti na uliopo sasa ambao unawafanya vijana kujianda kisaikolijia kuajiriwa kuliko kutumia maarifa aliyonayo kujiajiri.

"Tuangalie upya mfumo wetu wa elimu kwa kuwa fikra wanazojengewa vijana sio sahihi," Prof. Kamuzora alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi, Dk. Avemaria Semakafu, alisema maendeleo ya sayansi na teknolojia yameleta mabadiliko mengi katika mfumo wa ufanyaji kazi, hivyo alitaka kufikiriwa upya kuhusu suala la ajira nchini kwa kuwa mazingira ya sasa ni tofauti na zamani.

"Tunahitaji kufikiria upya kuhusu hili neno ajira kutokana na ukuaji wa teknolojia hivi sasa, zamani mtu aliweza kualika vibarua wengi kulima shamba, kwa sasa trekta moja inaweza kufanya kazi ya watu wengi," Dk. Semakafu alisema.

## UDOM, Shell waandaa vijana

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WASHIRIKI kwenye warsha ya kuwaandaa vijana na maisha wamalizapo masomo yao ya shahada ili kwenda sambamba na soko la ajira wameipongeza Shell Tanzania kwa udhamini kwa kuwa imewajengea uwezo mkubwa.

Mafunzo hayo yalitolewa kwa washiriki 274 na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), ambapo wajasiriamali na wasomi wa kada mbalimbali waliwasilisha mada ili kuwapa vijana msukumo wa kupambana na soko la ajira ndani na nje ya Tanzania.

Kaimu Rais wa Ndaki ya Sayansi za Ardhi, Dk. Godlisten Kombe, aliishukuru Shell Tanzania kwa namna inavyosaidia jamii katika nyanja mbalimbali ikiwamo elimu.

Aidha, Dk. Kombe alisema mafunzo haya yamekuja katika wakati mwafaka ili kuwajenga wanafunzi na hasa tunapoelekea uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo 2025.

"Jitihada hizi zina maana kubwa sana kwetu kama chuo na taifa kwa ujumla kwa kuwa inawafanya vijana wawe chachu ya kutafuta na kufanya kazi kwa bidii, hivyo kuifanya sera ya uchumi wa kati na viwanda viweze kufikiwa kwa urahisi," alisisitiza Dk. Kombe.

Katika hatua nyingine Dk. Kombe alitoa wito kwa taasisi na kampuni mbalimbali nchini kujitokeza katika kuwasaidia Watanzania katika nyanja mbalimbali kama Shell Tanzania wanavyofanya.

"Nitoe wito kwa kampuni mbalimbali kujitokeza katika kuwasaidia vijana kuwajengea uwezo na hatimaye tukapata nguvu kazi ya kuzalisha katika sekta mbalimbali kama ambavyo Shell Tanzania wameguswa kwa vijana wa hapa Udom, ni matumaini yangu kuwa semina hii itawabadilisha vijana," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Oxford Policy Management Tanzania (OPM), Dk. Charles Sokile, aliwaasa vijana kutumia nafasi wanazozipata katika kujijengea uwezo ikiwamo semina hiyo kwa kuwa soko la ajira linaushindani mkubwa.

Pia aliwataka vijana kutokuwa na aibu wakati wakiwa katika mwelekeo wa kutafuta mafanikio ambayo wamekuwa wakiyaota tangu wakiwa wadogo.

"Vijana wetu wamekuwa na changamoto nyingi katika soko la ajira, lakini changamoto hizo baadhi zinatengenezwa na vijana wenyewe kwa kupuuza mambo ambayo wangekuwa na ujasiri wa kuyafanya wangefika mbali, hivyo lazima wawe na uthubutu," alisema Dk. Sokile.

Simon Jackson, mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika fani ya uchenjuaji na uchakataji wa madini aliishukuru kampuni hiyo kwa namna ambavyo wanaandaa semina hiyo kwa kuwa wao kama walengwa imewaongezea thamani kubwa.

Ofisa Utafiti na Uzalishaji kutoka Shell Tanzania, Marcus Luoga, alisema: "Tumewaalika wataalamu mbalimbali ili kuelezea namna nzuri inayoweza kuwasaidia wahitimu wa vyuo vikuu kufikia malengo yao."

# Ataka utafiti nyavu za kuvulia dagaa

MBUNGE wa Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi, ameitaka serikali kufanya utafiti utakaoainisha matumizi ya nyavu kutegemea aina ya dagaa wanaopatikana kwenye ziwa husika.

Akiuliza swali bungeni jana, Mkundi alihoji kwa nini serikali isifanye utafiti huo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) hufanya utafiti mara kwa mara ili kubaini athari za matumizi ya zana na mbinu mbalimbali za uvuvi kwa rasilimali za uvuvi na kisha kuishauri serikali.

Alisema wizara yake ina jukumu la kulinda, kuhifadhi, kuendeleza na kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi hapa nchini zinavunwa kwa busara ili ziwe endelevu kwa manufaa ya kuchumi, kijamii na taifa kwa ujumla.

Naibu huyo alisema kifungu cha 66(1) (k) cha kanuni za uvuvi za mwaka 2009, nyavu za dagaa zenye ukubwa wa macho chini ya milimita nane zimekatazwa kutumika kwa uvuvi katika maji baridi ikiwamo Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Aidha, alisema utafiti uliofanyika katika Ziwa Victoria, unaonyesha kuwa kuna aina moja tu ya dagaa anayejulikana kwa jina la kitaalamu 'Restrineobola argentea'.

Alisema utafiti pia unaonyesha nyavu zenye macho kuanzia milimita nane zikitumika kuvua dagaa wa Ziwa Victoria zitavua waliopevuka na matumizi ya nyavu zenye matundu chini ya milimita nane zikitumika zitavua dagaa wachanga na hiyo itaathiri uvuvi wa dagaa katika Ziwa Victoria.

"Sheria ya Uvuvi na Kanuni zake imezingatia aina ya dagaa katika maji baridi (Maziwa) na maji ya bahari," alisema.



# AG amtetea DPP uchunguzi kesi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) haizuii majalada ya uchunguzi kufikishwa mahakamani.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Dk. Adelardus Kilangi, alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akitoa majibu ya nyongeza kwenye swali la Mbunge wa Kasulu Mjini (CCM), Daniel Nsanzugwako.

Nsanzugwako katika swali lake alisema tatizo la ufisadi na wizi nchini limeachwa likiendelea kwa muda mrefu.

"Je, ni kwa nini Takukuru wasiachiwe kuendesha mashauri makubwa ya ufisadi na wizi mahakamani moja kwa moja bila kuomba kibali cha DPP? Na je, DPP amezuia majalada mangapi ya uchunguzi kufikishwa mahakamani na ni kwa nini?" Alihoji.

Pia alisema DPP anaweza kutumika kulinda maslahi ya viongozi ambao kwa kiwango kikubwa wanajihusisha na wizi na ufisadi pamoja na matumizi mabaya ya madaraka.

Akijibu maswali hayo, Dk. Kilangi alisema kwa mujibu wa Katiba, mamlaka ya DPP inampa uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote yanayohusu makosa ya jinai nchini.

Alibainisha kuwa DPP anaweza kutekeleza au kwa maelezo yake na kuhusu kuzuia au hazuii mafaili kwenda mahakamani, hajazuia.

Dk. Kilango alisema kinachofanyika ni kwamba DPP lazima apime ushahidi uliotolewa kwenye mamlaka ya uchunguzi hadi ajiridhishe kuwa ushahidi unajitosheleza.

Awali, akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala bora, Mary Mwanjelwa, alisema kwa mujibu wa kifungu cha 57(2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007, DPP anapaswa kutoa au kutotoa kibali kuwafikisha watuhumiwa mahakamani ndani ya siku 60 tangu jalada la uchunguzi kufikishwa.

Hata hivyo, DPP anapokea majalada ya uchunguzi kutoka vyombo mbalimbali vya uchunguzi, vikiwamo Takukuru, Polisi na Uhamiaji.

Kadhalika, alisema kwa siku DPP hupokea takribani majalada 10 kutoka Takukuru, hivyo kuna kila sababu kuongezewa rasilimali watu na fedha ili kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Naibu Waziri huyo alisema DPP ni ofisi inayojitegemea na mamlaka yake yako kwa mujibu wa Katiba na kwamba viongozi mbalimbali wa serikali, wakiwamo mawaziri, wanafikishwa mahakamani na kuhukumiwa kwenda jela.

Pia alisema kwa mujibu wa kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007, Takukuru inayo mamlaka ya kufikisha watuhumiwa waliotenda makosa ya hongo kinyume na kifungu cha 15 cha sheria hiyo moja kwa moja mahakamani bila kupitia kwa DPP.

Alifafanua kuwa makosa mengine yaliyosalia yanapaswa kupata kibali cha DPP kabla ya kupelekwa mahakamani kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu cha 57(1) cha sheria namba 11 ya mwaka 2007.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi ndogo ya Bunge, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2017/18. **PICHA: BUNGE**

# Madeni ya walimu yafikia bil. 61/-

SERIKALI imesema hadi sasa walimu wanaidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 61 ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya mshahara na likizo.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema hayo jana bungeni mjini hapa, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Kiza Mayeye.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema walimu wamekuwa hawapewi fedha za likizo na matibabu licha ya kuwa jambo hilo ni takwa la kisheria kwa mujibu wa kazi.

"Je, ni lini watapewa fedha hizo kwa wakati ili kujikimu pindi wanapokuwa likizo na wanapoumwa ili kupata matibabu?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali ina nia nzuri kuhakikisha walimu wanalipwa kwa wakati na kwamba wako walimu wa shule za msingi 86,000 ambao wanaidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 43.

Pia alisema wako walimu 40,000 wa shule za sekondari ambao wanaidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 18, huku wengine kutoka ngazi za wilaya na mikoa wakidai zaidi ya Sh. milioni 157.

"Hapa ukijumlisha fedha zote utapata jumla ni zaidi Sh. bilioni 61 ni wahakikishie kuwa serikali imefanya utafiti kuhusu madai hayo na watalipwa," alisema.

Awali, katika swali lake la msingi, mbunge huyo alisema serikali imekuwa ikiwapandisha madaraja walimu, lakini haitoi malipo stahiki kwa madaraja hayo mapya kwa kipindi kirefu tangu wanapopanda.

Kutokana na hali hiyo, alihoji serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba walimu wanapata stahiki zao mara wanapopandishwa daraja lao la kazi zao. Akijibu swali hilo, Waitara alisema serikali ilisitisha kupandisha walimu na watumishi wengine madaraja katika mwaka wa fedha 2015/16 na 2016/17 kutokana na uhakiki wa watumishi uliohusisha uhalali wa vyeti, elimu na ngazi za mishahara.

Waitara alisema lengo la uhakiki lilikuwa kuhakikisha serikali inabaki na watumishi wenye sifa na wanaostahili kulipwa mishahara.

Alisema kutokana na sababu hiyo, ni kweli wako watumishi ambao walipandishwa madaraja ambao hawajalipwa mishahara mipya na wako waliopata mishahara mipya na baadaye kuendolewa na wako ambao hawakupandiswa kabisa pamoja na kwamba walikuwa na sifa.

Naibu Waziri huyo alibainisha kuwa ili kurekebisha changamoto hizo, serikali ilitoa maelekezo kuanzia Novemba, 2017 kwa waajiri wote wakiwamo wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuhuisha barua za kuwapandisha madaraja watumishi hao ili walipwe stahili zao.

Hata hivyo, alisema kwa wale ambao walikuwa na barua, lakini taarifa zao zilikuwa hazijaingizwa kwenye mfumo, waajiri walielekezwa kuhuisha barua zao kuanzia Aprili Mosi, mwaka huu, ili waanze kulipwa.

## Watu 150 wajitolea damu kituo cha afya

**Na Mwandishi Wetu, MIRERANI**

WATU 150 wamepima afya zao na kujitolea damu kwa ajili ya wahitaji wa Kituo cha Afya cha Mirerani, wilayani Simanjiro.

Zoezi hilo lililoandaliwa na Taasisi ya Masjid Noor ya Mji Mdogo wa Mirerani, lilifanyika mwishoni mwa wiki na waamini wa dini ya Kiislamu ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 1,440 ya Maulid ya Mtume Muhammad S.A.W.

Mwenyekiti wa Maulid iliyofanyika kwenye taasisi hiyo, Mohamed Issa Mughanja, alisema damu iliyotolewa itawasaidia wajawazito wanaohitaji damu wakati wa kujifungua na majeruhi wa ajali.

Imamu wa taasisi hiyo, Sheikh Ramia Isanga, alisema waliamua kujitolea damu ili kutimiza mafundisho ya Mtume Muhammad S.A.W.

"Katika mafundisho ya Mtume Muhammad S.A.W alituusia kuumika yaani kupiga chuku au kujitolea damu, nasi tumefuata mwenendo wake kwa kujitolea damu salama," alisema Sheikh Isanga.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mirerani, Dk. Hassan Ishabailu, alisema kabla ya kutoa damu, wanafanya vipimo vya shinikizo la damu, kisukari, ushauri na maambukizi ya virusi vya Ukimwi, (VVU).

Dk. Ishabailu aliwashukuru wananchi wote waliojitokeza kwenye shughuli hiyo ya kuchangia damu salama ambayo itawasaidia wagonjwa wa kituo hicho.

Imamu msaidizi wa Taasisi ya Masjid Noor, Mohamed Hassan, alitoa wito kwa watu kushiriki kuchangia damu kwa kuwa viongozi wote wa taasisi hiyo wamejitolea damu salama wakiongozwa na Imamu wao Sheikh Isanga.

Mohamed alisema kupitia maadhimisho hayo wamedhamiria kujitolea damu salama katika kituo hicho kwa wahitaji wa sasa na baadaye.

Mmoja kati ya waliojitolea damu salama, Mariam Hamis, alisema kutoa huduma hiyo ni jambo zuri kwani mmoja anapotoa damu inaweza kumsaidia mwenyewe baadaye au ndugu na jamaa zake.

# Wanafunzi walilia uzio kujilinda na wanyama

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

USALAMA wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari Longido mkoani Arusha upo hatarini kutokana na kukosekana uzio wa kuwalinda dhidi ya wanyama wakali na watu wasiokuwa na nia njema wanaopita shuleni hapo wakati wa usiku.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na wanafunzi wa kidato cha sita wakati wa mahafali yao shuleni hapo, mbele ya Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, William ole Nasha.

Akisoma risala hiyo, mwanafunzi Frida Mumbai, alisema shule hiyo yenye wanafunzi 1,471 haina uzio hali ambayo inahatarisha maisha ya wanafunzi nyakati za usiku.

Shule hiyo pia ina wanafunzi wenye mahitaji maalum ambao ni walemavu wa macho, viungo, kusikia na wenye albino.

Alisema kutokana na ukosefu wa uzio, kunapelekea kushuka kwa ufaulu kwa wanafunzi shuleni hapa kwa kuwa wengi wao huwa na mashaka na maisha yao, hususani, wanafunzi wa kike na wenye ulemavu.

"Wiki tatu za nyuma hapa shuleni majira ya usiku walikuwa wakiingia watu wasioeleweka na kusababisha taharuki katika eneo la shule, wengine ni walevi wanakuja kutusumbua mabwenini majira ya usiku," alidai.

Mkuu wa shule hiyo, Daniel Temu, alikiri shule hiyo kutokuwa na uzio na kuelekeza kilio chao kwa serikali na wadau watakaoguswa ili kusaidia ujenzi wa uzio huo kukamilika.

Hata hivyo, pamoja na changamoto hiyo, alisema hali ya ufaulu kwa wanafunzi waliohitimu mwaka jana kidato cha sita ilikuwa nzuri kwa kutokuwa na ufaulu wa daraja la nne na sifuri.

"Mwaka jana ufaulu ulikuwa nzuri, daraja la kwanza walipata wanafunzi wanne, daraja la pili 102 na la tatu 123 hatukuwa na 0 wala daraja la nne," alisema. Aligusia pia kuwapo kwa wanafunzi maalumu katika shule hiyo kwa kuwa shule hiyo ni ya mchanganyiko, ikiwa na wenye ulemavu wa viungo ambao ni wawili, kusikia wawili, albino 32 na macho tisa.

"Tuna jumla ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, nikimaanisha walemavu 45," alisema.

Akizungumza katika mahafali hayo ya 13, Naibu Waziri Ole Nasha, alisema serikali kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa elimu kwa wananchi wake imeongeza mkopo wa elimu ya juu kwa wanafunzi wenye sifa za kupata mkopo kutoka Sh. bilioni 427 ya mwaka jana hadi Sh. bilioni 450 mwaka huu.

Aliagiza Bodi ya Mkopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu baada ya wiki mbili wafike katika shule hiyo na kutoa elimu kwa wanafunzi wa kidato cha sita juu ya ujazaji wa fomu hizo za mkopo.

Kuhusiana na ukosefu wa uzio, Ole Nasha, alisema, atashirikiana na Ofisi ya Mipango ya Wizara ya Elimu kuhakikisha shule hiyo inapata uzio kwa usalama wa wanafunzi.

"Shule hii itapata uzio, kwanza kuna wanafunzi maalumu hapa, ni lazima waishi na kusoma mazingira rafiki," alidai Ole Nasha.

Aliwataka wazazi kuwapeleka watoto shule na kuepukana na mila na desturi potofu kwa kuwaozesha watoto wa kike, na mzazi atakayebainika atamchukulia hatua kali za kisheria ikiwamo kufungwa jela.

"Akibainika mzazi anayemnyima mtoto haki ya elimu, kamata peleka Magereza," aliagiza.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Manyara, Sajini Chande Abdalah, akitoa elimu kwa umma juu ya majanga mbalimbali kwenye mkutano wa Kijiji cha Nakwa, Kata ya Bagara, Mjini Babati, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wamwagiwa mikopo ya mil. 40/-

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Longido imetoa Sh. milioni 40 ambazo ni sehemu ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa vikundi 14 kutoka kata 10 kati ya 18.

Akikabidhi hundi kwa vikundi hivyo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri, Nestory Dagharo, ambaye ni Ofisa Mifugo katika halmashauri hiyo, alisema fedha hizo ni asilimia 10 ya agizo la serikali kutolewa katika mapato ya ndani na kuwezesha vikundi maalumu.

Aliwataka walengwa wa fedha hizo kuzitumia katika kile walichokiombea na kurejesha fedha hizo kwa wakati ili ziweze kusaidia vikundi vingine vyenye uhitaji wa mikopo hiyo.

"Vikundi ni vingi ndani ya wilaya na wameomba mikopo, ninyi mmebahatika, kafanyieni kazi na mkumbuke kurejesha," alisema Dagharo.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Grace Mghase, alisema vikundi vilivyopewa mikopo ni 14, ambavyo sita ni vya wanawake, vitano vya vijana na vitatu vya watu wenye ulemavu.

Alieleza kwa mwaka wa fedha 2018/19 halmashauri imetoa jumla Sh. 92,630,000 hadi kufikia robo ya pili.

"Robo ya kwanza na ya pili tumetoa Sh. 92,630,000 na sasa robo ya tatu ya mwaka tunatoa Sh. milioni 40," alisema Grace.

Alieleza mchanganuo wa fedha hizo katika makundi ni vikundi sita vya wanawake watapewa Sh. milioni 18.5, za vijana watapatiwa Sh. milioni 14 na vikundi vitatu vya walemavu watapewa Sh. milioni 8.

Baraka Laize, mwenye ulemavu ambaye mnufaika wa mikopo hiyo alisema watatumia fedha hizo kununua mifugo na kunenepesha ili wajikwamue kiuchumi.

Alidai miaka ya nyuma walemavu walikuwa hawatambuliki na kuonekana ni watu ambao hawawezi, lakini kwa sasa anaona mabadiliko makubwa kwa serikali yao kuwajali.

Alieleza jamii ya kifugaji haina utaratibu wa kuwathamini watu wenye ulemavu, hivyo, wengi wao huishia kufungiwa ndani na kunyimwa haki zao za msingi.

"Sisi tunaishukuru halmashauri yetu kwa kutoa asilimia 2 ya walemavu, lakini pia tunamshukuru Rais Magufuli kwa kuwajali wanyonge," alisema.

## KESI YA MAUAJI YA MWANAFUNZI

# DAKIKA 120 ZAMALIZA UTATA MAHAKAMANI

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

UAMUZI mdogo uliochukua dakika 120 kutolewa na Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi kumaliza mtifuano wa kupinga kupokelewa kwa maelezo ya kukiri kosa la mauaji ya mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Scolastica, Humphrey Makundi, uliosababisha kuzaliwa kwa kesi ndani ya kesi, umehitimishwa kwa Jaji Firmin Matogolo kukubali kupokea maelezo hayo.

Jopo la mawakili wa utetezi katika kesi hiyo walipinga kupokelewa kwa maelezo hayo (Extra Judicial Statement) ya mshtakiwa wa kwanza Hamisi Chacha ambayo yaliandikwa na mlinzi wa amani, Irene Mushi, ambaye ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Moshi Mjini wakidai kuwa kulikuwa hakuna uhiari na kulikuwa na ukiukwaji wa sheria kwa kuchukua maelezo hayo nje ya muda.

Alipoanza kusoma uamuzi huo saa 4:36 asubuhi hadi saa 6:37 mchana, Jaji Matogolo anayesikiliza kesi hiyo namba 48 ya mwaka 2018, alieleza kwamba amepitia hoja zote za kisheria zilizoibuliwa na upande wa utetezi na majibu ya upande wa mashtaka na kujiridhisha kuwa hakuna ukiukwaji wowote wa kisheria uliofanywa katika uandishi wa ungamo hilo.

"Hakuna ukiukwaji wowote uliofanywa katika uandishi wa ungamo, tarehe ya kukamatwa kwake imeonyeshwa katika ungamo na suala la muda sio la lazima kuonyeshwa. Kwa msingi huo pingamizi lililotolewa na mawakili wa upande wa utetezi kwamba lilikiuka sheria halina msingi na nina litupilia mbali," alieleza Jaji Matogolo.

Zaidi alieleza kuhusu suala la uhiari," mshtakiwa wa kwanza (Hamisi Chacha), alijichanganya katika majibu yake wakati akitoa ushahidi wake. Mshtakiwa wa kwanza alitoa ungamo lake kwa amani na alikuwa huru. Hii haina maana kwamba kupokelewa kwa kielelezo hicho pekee kwamba ndio kitatumika kutoa hukumu. Natupilia mbali pingamizi hilo na maelezo hayo yanapokelewa na kuwa kielelezo cha ushahidi wa upande wa mashtaka."

Baada ya kupokelewa kwa maelezo hayo ya kukiri kosa kwa mshtakiwa wa kwanza, shahidi wa 14 wa upande wa mashtaka (Irene Mushi) aliongozwa tena na Wakili Mkuu wa Serikali, Joseph Pande, kujibu maswali machache na baadaye kutakiwa kuisomea mahakama hiyo kilichomo ndani ya ungamo hilo.

Wakati anasoma ungamo hilo, shahidi huyo alidai kuwa mshtakiwa alikiri mbele yake kwamba aliua, lakini hakufahamu kama aliyemuua alikuwa ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Scholastica na kwamba aliandika maelezo hayo kwa saa moja na nusu.

Alidai kuwa kabla ya kuandika maelezo hayo alimkuta mshtakiwa akiwa na alama ya fimbo mgongoni na alipomuuliza alimweleza kwamba alipigwa na Polisi.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, wakati wa usikilizwaji wa kesi ndani ya kesi (Trial within trial), shahidi huyo wa utetezi, Hamis Chacha alieleza mateso ya aina nane anayodai alifanyiwa na Polisi ili kuandika maelezo ya kukiri kosa la mauaji ya mwanafunzi wa Shule ya Scolastica, Humphrey Makundi.

Chacha alidai kuwa alipigwa kwa shoti ya umeme, kuunguzwa kwa pasi ya umeme, kuingiziwa sindano kwenye uume wake na kuingiziwa chupa ya bia sehemu ya haja kubwa.

Kesi hiyo ya mauaji inamkabili mmiliki wa Shule ya Scholastica, Edward Shayo, pamoja na mwalimu wa nidhamu, Laban Nabiswa na mlinzi wa shule hiyo, Hamis Chacha.

Chacha ambaye alimaliza kutoa ushahidi wake saa 2:20 usiku mbele ya Jaji Firmin Matogolo, alitaja mateso mengine kuwa ni kupigwa kwa bakora, kulazwa uchi, kunyimwa chakula na kulazwa chumba chenye maji.

Chacha, ambaye alikuwa akiongozwa na Wakili David Shillatu, alidai kuwa Novembа 17, 2017 akiwa shuleni Scolastica, alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi cha Himo akiwa na mlinzi mwenzake aliyemtaja kwa jina moja la Mchamungu na wakawekwa mahabusu.

Alidai ilipofika saa 2:00 usiku, walitolewa mahabusu na kupelekwa mapokezi ambako polisi mmoja alimpiga kwa bakora nyeusi na mwingine akimpiga kwa kitako cha bunduki.

Aliiambia mahakama kuwa muda huohuo walihamishiwa kituo cha kati ambako waliwekwa chumba kimoja, lakini baada ya muda alichukuliwa na kupelekwa eneo jiingine.

"Kwenye hicho chumba kulikuwa na pikipiki na redio ya subwoofer. Niliwakuta polisi watatu na yule aliyenichukua akawa wa nne. Niliambiwa nivue nguo zote nibaki kama nilivyozaliwa," alieleza.

Akiwa hapo, anadai alifungwa pingu miguuni na mikononi kwenye meza na polisi walianza kumpiga kwa bakora, kabla ya kumfungua na kuweka chupa ya bia ya kumlazimisha aikalie.

Shahidi huyo alidai wakati wakimtesa walimtaka akubaliane nao na aeleze kuwa Novemba 6, 2017 usiku wa saa 2:58 kuna mtu aliruka ukuta kutokea ndani ya shule na akamkurupusha kuelekea uraiani.

Kwa mujibu wa ushahidi wake, alitakiwa kueleza kuwa baada ya kumkimbiza alimpiga na mabapa ya panga hadi akafariki dunia na ndipo alimpompigia simu Laban na mmiliki wa shule hiyo.

Pia, alitakiwa aseme kwamba baada ya mmiliki kufika hapo aliagiza wachukue mwili huo na kuutupa Mto Ghona kwa madai kuwa usiku ule ulikuwa haujatambulika.

Hata hivyo, alidai aligoma kusaini maelezo hayo, ndipo polisi walipoendelea kumtesa kwa umeme na kumuunguza kwa pasi ya umeme, hiyo ikamfanya akubali kusaini maelezo hayo.

Alieleza kuwa Novemba 19, 2017, polisi hao walimchukua na kumweleza kuwa kesho yake wangempeleka kwa mtu walіyemuita ni "bosi wao" (mlinzi wa amani) na aeleze kama alivyoandika.



Wakati anasita, alitokea mtu aliyemtaja kuwa ni Godvictor Munisi aliyekuwa na sindano ndefu, na aliingiza katika uume wake na kutokana na maumivu makali aliyopata, alikubali kufanya walichotaka.

Mbali na Munisi, aliwataja polisi aliodai walikuwa wakimfanyia ukatili huo kuwa ni Inspekta Waziri Tenga, Inspekta Fredy Kisanga, Inspekta Leons, na polisi wengine wawili ambao hawafahamu majina.

Novemba 20, 2017 alipelekwa kwa bosi huyo na alitoa maelezo kama alivyoelekezwa na baadaye mtu mmoja alimshurutisha kusaini maelezo yanayodaiwa ni ya ungamo na kuweka dole gumba.

Baada ya kutoa ushahidi huo, upande wa Serikali wakiongozwa na Joseph Pande, pamoja na Abdalah Chavulla, Omary Kibwana na Wakili Lucy Kyusa walimuhoji shahidi huyo:

**Wakili Pande:** Kama nilikuelewa, umesema ulipelekwa kwa mtu anaitwa Irene Mushi kuandika maelezo yako, ni kweli?

**Shahidi:** Nilipelekwa kwake huyo waliyesema ni bosi wao.

Wakili Pande: Kwamba Irene Mushi alikuwa anaandika kile ulichokuwa unamueleza

**Shahidi:** Ndio mheshimiwa

Wakili Pande: Hiyo nyaraka (maelezo ya ungamo) aliyokuwa anaiandika wewe ulipata fursa ya kuipitia, kuisani na kuweka dole gumba?

**Shahidi:** Ndio niliweka

**Wakili Pande:** Kuna mtu aliyekushurutisha uweke saini na dole gumba?

Shahidi: Simfahamu kwa jina ila ni mwanaume. Alishika kidole changu na kukandamiza

**Wakili Pande:** Na vile vile ukasaini bila ridhaa yako?

Shahidi: Yule bosi wake ndio alimuamuru kuwa Chacha asaini hapo.

**Wakili Pande:** Umesema hapa ulipigwapigwa, kipi ambacho kilitangulia, kipigo au kile walichokitaka?

**Shahidi:** Walianza na kipigo na baadaye mateso.

Wakili Pande: Lakini, ulivyofika kwa mlinzi wa amani ukamuonyesha alama za fimbo tu?

**Shahidi:** Kwa mila na desturi zetu sisi Wakurya hatuwezi kumvulia nguo mwanamke ambaye sio mke wako.

**Wakili Pande:** Tukubaliane kwamba yale ambayo hakimu aliandika ni yale tu uliyoelekezwa na Inspekta Tenga, si ndio?

**Shahidi:** Ndio.

**Wakili Pande:** Hata suala la kusema ulipigwa na askari wengi ni Tenga alikuambia pia?

**Shahidi:** Hayakuwa maelekezo ya Tenga.

**Wakili Pande:** Inspekta Tenga alipokuwa anatoa ushahidi hapa asubuhi hukumuuliza swali lolote kwamba wamekuonea?

**Shahidi:** Ndio aliulizwa.

Wakili Pande: Kwamba aliulizwa wewe Tenga ndio ulimwelekeza Leons akuchome na pasi.

**Shahidi:** Hilo swali hakuulizwa

**Wakili Pande:** Irene alipokuwa anatoa ushahidi hapa aliulizwa wewe ndio uliomshurutisha Chacha aweke saini na dole gumba?

**Shahidi:** Hakuulizwa.

**Wakili Chavulla:** Uliiambia mahakama uliingiziwa chupa ya bia, ilikuwa na ukubwa gani?

**Shahidi:** Inaanza nyembamba (akionyesha) halafu inaongezeka unene.

**Wakili Chavullah:** Kwani ile chupa ilipakwa mafuta?

**Shahidi:** Haikuingia kwa raha bwana yalikuwa mateso.

**Wakili Chavullah:** Ilikuwa mara yako ya kwanza kuingiziwa kitu kigumu na bado una ujasiri wa kusimama na kutembea?

**Shahidi**: Mheshimiwa Jaji, hata mwanamke anafanyiwa na anatembea itakuwa mwanamume ashindwe kutembea?

**Wakili Kibwana:** Tarehe 6.11.2017 usiku (siku ya tukio la mauaji) ulimpigia simu Mzee Shayo na mwalimu Laban?

**Shahidi:** Ni kweli.

**Wakili Kibwana:** Ni kweli kwamba Mzee Shayo naye alikupigia usiku huo huo?

**Shahidi:** Nilimpigia kweli hatukuelewana ndio akanipigia.

**Wakili Kibwana:** Ni kweli mwalimu Laban naye alikupigia usiku huo.

**Shahidi:** Alinipigia.

**Wakili Kyusa:** Ni kweli kwamba katika walinzi wanne wa Scolastica ni wewe tu umeshtakiwa?

**Shahidi**: Ndio.

**Wakili Kyusa:** Ni kweli kwamba tarehe 27.11.2017 ulifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza na kusomewa shtaka hili la mauaji?

**Shahidi:** Ndio na niliambiwa hakuna kujibu chochote.

**Wakili Kyusa:** Ni kweli hukuona umuhimu wa kumwambia hakimu kuhusu mateso na vidonda ulivyovipata?

**Shahidi:** Niliambiwa hakuna kujibu chochote.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi leo Jumanne wakati itakapoendelea tena kusikiliza mashahidi wa upande wa mashtaka katika kesi hiyo.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo inayovuta hisia za wakazi wengi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini unaongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Joseph Pande, Wakili Mwandamizi wa Serikali Abdalah Chavullah, Wakili wa Serikali, Omary Kibwana na Lucy Kyusa.

Wakati jopo la mawakili wa utetezi linaongozwa na mawakili wasomi Elikunda Kipoko, Wakili David Shilatu, Wakili Gwakisa Sambo na Wakili Patrick Paul.

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 16, 2019
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?

TEMBE ZA UZAZI WA MPANGO KWA WANAUME ZAPITA JARIBIO LA AWALI



## Mnyamakale mwingine apatikana Rukwa, jina lake latolewa kitaaluma, si Kiswahili

Ukurasa 19



# Wazazi, walezi wilayani Mbeya wanyooshewa kidole cha lawama

Ukurasa 16



# TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

## Maneno halisi ya Kiswahili hayafai?

KUJUA lugha zaidi ya moja ni kuongeza utajiri wa lugha ngeni. Wahenga walisema "Kitu chako wadidimiza shingo cha wenzako wanyosha shingo." Maana yake kitu chako hutaki kitumiwe au kiwafaidi wengine ilhali cha wengine unakitamani.

"No way out! Pochettino anahusika Man United" Ni kichwa cha habari kilichoandikwa na gazeti maarufu la michezo nchini.

Imekuwa kawaida ya magazeti ya Kiswahili kuchanganya maneno ya Kiingereza na Kiswahili ilhali yapo ya Kiswahili!

Hapa nafasiri (kitendo cha kuhamisha maana ya matini ya lugha moja na kuyapeleka kwenye lugha nyingine; tarjumi) maana ya neno moja moja: Maana ya 'No' ni hapana, hakuna, hamna. 'Way' maana yake ni njia, barabara. 'Out' ni nnje.

Kwa hiyo inaposemwa "No way out" maana yake ni 'hakuna njia,' 'hakuna uwezekano,' 'haiwezekani.' Kwa hiyo "No way out! Pochettino anahusika Man United" Kiswahili chake ni "Haiwezekani! Pochetino anahitajika; husika Man United."

"Ishu ya Kakolanya yatikisa." Kichwa hiki cha habari kiliandikwa kwenye gazeti la michezo kuhusu suala la mlinda mlango wa Yanga, Beno Kakolanya. 'Ishu' ni neno lililotoholewa (badilishwa matamshi au tahajia ya neno la lugha moja ili lilingane na matamshi au tahajia nyingine) kutoka Kiingereza.

"Ishu ya Chilunda huko Tenerife ipo hivi" ni kichwa kingine cha gazeti la michezo. Je, kulikuwa na sababu ya kutohoa neno hilo? Maana ya 'issue' kwa muktadha huu, ni 'suala.' Hivyo kichwa kingeandikwa: "Suala la Kakolanya latikisa" na "Suala la Chilunda Tenerife liko hivi."

"Wakati Yanga wakiwasili kwa mbwembwe, kocha wa Mbao, Ally Bushiri 'Benitez' alikuwa bize kuwanoa wachezaji wake huku kukiwa na mvua." Neno 'bize' limetoholewa kutoka neno 'busy' la Kiingereza, lenye maana ya -enye kazi, mashughuli, -a shughuli nyingi, jishughulisha.

Sentensi ingeandikwa: "Wakati Yanga wakiwasili kwa mbwembwe, kocha Ally Bushiri 'Benitez' wa timu ya Mbao alikuwa akijishughulisha na wachezaji wake bila kujali mvua iliyokuwa ikinyesha."

Waandishi wa magazeti pia hutumia maneno ya Kiswahili kwa maana tofauti na maudhui yake. Kwa mfano: "Mastaa Yanga waoga noti." Neno 'oga' lina maana mbili: 1. Safisha mwili mzima kwa kutumia maji na sabuni; 2. -enye kuogopa au kutishika kufanya jambo, -enye kuwa na hofu. Je, mastaa wa Yanga wataogaje noti badala ya maji na sabuni?

"Kumbe Sinta alimpa ulaji Kagere buana" ni kichwa cha gazeti mahiri la michezo nchini. Lugha ya Kiswahili haina neno 'buana' ambalo siku hizi latumiwa sana na magazeti yetu badala ya maana halisi - Bwana!

Kwani neno 'bwana' halieleweki ambalo ndilo sahihi kwa Kiswahili? Kichwa cha gazeti hilo kingeeleweka vizuri kama kingeandikwa: "Sinta alimpa Kagere ulaji." Sinta alimpa nani? 'Kagere.' Kitu gani? 'Ulaji.'

"Wabunge wamwaga noti Yanga" ni kichwa cha habari kilichoandikwa ukurasa wa mbele wa gazeti maarufu la michezo nchini. 'Mwaga' ni toa kitu cha majimaji, punjepunje au unga ndani ya kitu kingine na kukitawanya; kitendo cha kutawanya kitu chini kama vile maji na punje za nafaka. 'Mwagia' ni kitendo cha kumimina kitu juu ya kingine. Noti zamwagwaje? Ingeandikwa: "Wabunge waipa Yanga hela."

"Yanga yaliamsha" ni kichwa kingine cha gazeti ninalolijadili. Wakati mwingine huandikwa: "... yaliamsha dude." Maana ya 'amsha' ni toa mtu usingizini; zindua; inua mtu aliyekuwa nyuma kimawazo na kiuchumi. Maana ya 'dude' ni kitu kikubwa kisichojulikana; dubwana. Pia ni mtu anayedharauliwa; lakabu (jina la kujibandika au kupewa la utani, jina la kupanga; msimbo) kuonesha dharau kwa mtu mwingine.

"John Terry ampandisha mzuka dogo" kadhalika ni kichwa cha gazeti maarufu la michezo nchini. 'Mzuka' kwa maana sahihi ya neno hilo ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na huweza kumtokea mtu; pepo. "Monalisa afurahia mambo ya dogo." 'Dogo' ni mtu mwenye umbo dogo (ingawa si rasmi); siokuwa kubwa; katiti, saghiri. Siokuwa nyingi; chache, haba.

Tatizo la waandishi wengi, hasa wa magazeti ya michezo ni kutumia maneno ya kihuni yasemwayo mitaani na wahuni badala ya kutumia maneno halisi ya Kiswahili.

"ANASEPA: miguu ya Msuva iko tayari kutua Ulaya." Neno la kwanza la (anasepa) halimo kwenye lugha ya Kiswahili bali ni baadhi ya maneno yanayoanzishwa mitaani na wahuni. Ingetosha tu kuandika "Miguu ya Msuva ipo tayari kutua Ulaya" na ingeeleweka badala ya msomaji/wasomaji kuuliza maana ya 'anasepa.'

"Simba ya MO noma ... yavuna Bil. 2 kwa kina Okwi." Maana halisi ya neno 'vuna' ni ondoa mazao yaliyokomaa shambani; kitendo cha kuchuma mazao; sega. Kwa kawaida fedha hazivunwi kama mazao ya shambani bali hupatikana kwa kufanya kazi, biashara au kupewa. Kwa hiyo ingeandikwa: "Simba ya Mo yapata Bil. 2 kwa kina Okwi." 'Pata' ni kitendo cha mtu kumiliki vitu au kufikwa na jambo; pata msiba. Kitendo cha kitu kama vile kisu kuwa na makali.

Soma jinsi sentensi zinavyoandikwa ovyo kwenye magazeti yetu ya michezo: "Walichofanya Simba ni kufungua mfuko na kuchomoa senti kidogo kutoka kwenye mauzo ya Kichuya na kumnyakua straika huyo mwenye mabao saba katika Ligi Kuu na fasta kutuma jina lake CAF sambamba na beki Zana Oumar Coulibaly ili kukinukisha kwenye Ligi ya Mabingwa."

'Senti'ni sarafu ya thamani ya chini yenye sehemu moja ya mia ya shilingi. Siku hizi haitumiki kama zamani. 'Nyakua' ni kuchukua kitu kwa haraka sana na kuondoka nacho; pora, kwapua, bakua. 'Straika' ni mshambulizi na 'fasta' ni haraka.

**Methali: Likitoka liote**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

# ELIMU KUTOKA POLISI




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP, Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**

## FAHAMU MAMLAKA YA UPEKUZI

UPEKUZI ni kitendo cha kuingia aidha maungoni kwa mtu, ndani ya nyumba au kwenye makazi ya mtu kwa nia ya kutafuta kitu, vitu vilivyofichwa au vitu ambavyo vinahusiana na kosa la jinai.

Kwamba kitu au vitu hivyo vinaweza kusaidia katika upelelezi wa Polisi, au katika kesi inayoendelea mahakamani kama sehemu ya ushahidi wa kuthibitisha au kukanusha kosa linalojadiliwa.

Upekuzi unaweza kufanyika kwa namna mbili kwa kutumia hati ya upekuzi au Upekuzi unaofanyika bila hati ya upekuzi kulingana na mazingira husika.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kifungu cha 24 kinampa mamlaka na uwezo Ofisa wa Polisi kufanya upekuzi maungoni mwa mtu yeyote aliyemkamata na upekuzi huo unafanyika mara baada ya mtu kukamatwa na kuwa chini ya ulinzi.

Sheria hiyo pia, inampa uwezo wa kuchukua toka maungoni mwa mtu huyo kitu chochote cha hatari au kitakachosaidia upelelezi wa tuhuma zilizosababisha kukamatwa.

Aidha, sheria hiyo imetoa umuhimu wa kipekee kwa wanawake pale tendo la upekuzi linapotakiwa kufanyika dhidi yake. Aidha iwe maungoni au hata kwenye makazi yake.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, kifungu cha 26 kinatoa ufafanuzi wa jinsi mwanamke atakavyopekuliwa, kwamba upekuzi huo lazima ufanywe na Polisi Mwanamke au mwanamke yoyote ambaye anaaminika.

### MAMBO YA KUZINGATIWA

Mambo muhimu ya kuzingatiwa katika upekuzi, kulingana na unyeti wa tendo la Upekuzi, ni vyema kabla na baada ya upekuzi kufanyika Ofisa wa Polisi au mtu mwingine anayefanya upekuzi akawa na mashahidi wa kushuhudia upekuzi huo.

Ni haki ya msingi kwa mmiliki wa nyumba, jengo au eneo linalotakiwa kupekuliwa kuonyeshwa na kuona hati inayoidhinisha upekuzi, pia ni muhimu mashahidi waione hati hiyo kabla ya utaratibu wa upekuzi kuanza.

Aidha, jamii na wananchi kwa ujumla wana haki ya kutambua Mamlaka zilizopewa uwezo wa kuidhinisha upekuzi, ambazo ni Mkuu wa Kituo cha Polisi na Hakimu.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, inampa uwezo na mamlaka ofisa wa Polisi ambaye ni Mkuu wa Kituo cha Polisi (OCS) anapokuwa amepokea taarifa za kuaminika kwamba ndani ya nyumba, jengo au eneo fulani au kwenye chombo cha usafiri kuna vitu ambavyo anavitilia shaka ambavyo kwa sababu ya msingi vinasadikiwa kutumika kutenda kosa.

Mkuu wa Kituo anaweza kuidhinisha upekuzi kama anaamini kwamba ucheleweshaji wowote wa kufanyika upekuzi unaweza kusababisha utoroshwaji au uharibifu wa kitu au vitu vinavyotafutwa au vinaweza kuhatarisha maisha ya binadamu au mali.

Kwa upande wa Hakimu naye ana uwezo na mamlaka ya kuamuru upekuzi ufanyike kwenye nyumba, jengo au eneo lolote baada ya kupokea malalamiko au taarifa za kuaminika kwamba kwenye nyumba, jengo au eneo fulani kuna kitu au vitu visivyo halali au vielelezo muhimu.

Amri hii hutolewa kwa maandishi na hujulikana kama hati ya upekuzi.

Pia kifungu cha 43 cha sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai kinampa uwezo Ofisa wa Polisi kuvunja na kuingia kwenye nyumba au jengo au mahali popote kwa madhumuni ya kufanya upekuzi, iwapo patakuwa pamefungwa na mmiliki anakataa kutoa idhini baada ya kuonyeshwa hati ya kuamuru upekuzi ufanyike.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inampa uwezo Ofisa wa Polisi kufanya upekuzi kwa dharura kwenye nyumba, jengo au mahali popote endapo anazo sababu za msingi za kutaka kufanya upekuzi wa dharura.

Upekuzi wa dharura ufanyika bila hati ya kuidhinisha upekuzi yaani search order au search warrant. Upekuzi huu hufanyika baada ya mazingira kulazimu uharaka na kwamba kutokufanya hivyo kutasababisha uharibifu au utoroshwaji au kitu au vitu au mtu anayetafutwa kuhusiana na shaka au tuhuma.

Ni vizuri jamii ikaelewa kuwa, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai haitamki saa ya kufanya upekuzi, ila inasema upekuzi utafanyika kuanzia mawio hadi machweo ya jua na chini ya kifungu cha 42 upekuzi unaweza kufanyika hata usiku.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

ELIMU

NA ANTHONY GERVAS, MUSOMA

# Idara ya Uhamiaji na mwarobaini janga wahamiaji haramu nchini- 2

WIKI iliyopita, tulianza kuona namna Idara ya Uhamiaji inavyokabiliana na changamoto mbalimbali katika mipaka, hasa za wahamiaji haramu wanaoingia nchini bila vibali vya kuishi, kinyume cha sheria.

Tuliishia pale ambapo Msemaji Mkuu wa Idara hiyo Ally Mtanda, alipofafanua athari za wahamiaji haramu kwa taifa baadhi zikiwa ni kuhatarisha usalama wa wananchi na ongezeko la uhalifu kama vile ujambazi.

Leo msemaji huyu anazungumzia aina za uraia katika sehemu hii ya mwisho.

**AINA TATU ZA URAIA WA TANZANIA**

Akizungumzia aina za uraia, Mtanda anasema kwamba uraia wa Tanzania unasimamiwa na sheria za nchi za uraia Namba 6 ya mwaka 1995 pamoja na kanuni zake za mwaka 1997.

Anabainisha kuwa kwa mujibu wa sheria hiyo, zipo aina tatu za uraia nchini:

"Kuna uraia wa Tanzania wa kuzaliwa, uraia wa Tanzania wa kurithi na uraia wa Tanzania wa Tajinisi," anasema.

**URAIA WA KUZALIWA**

Msemaji huyo wa idara anasema kwamba kwa mujibu wa sheria ya Tanzania ya uraia Namba 6 ya mwaka 1995, mtu yeyote anayefuzu kuwa raia wa Tanzania wa kuzaliwa ni yule aliyezaliwa nchini na ambaye wakati wa kuzaliwa kwake, mmoja wa wazazi wake ni raia wa Tanzania.

**URAIA WA KURITHI**

Mtanda anasema, mtu yeyote aliyezaliwa nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, siku ya Muungano au baada ya Muungano anahesabika kuwa raia wa Tanzania wa kurithi.

"Hiyo ni kuanzia tarehe ya kuzaliwa kwake, kama siku ya kuzaliwa kwake, mama au baba yake ni raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kuzaliwa au tajinisi," anasema na kuongeza:

"Hiyo ina maana kwamba wazazi wake walikuwa ni raia wa Tanzania wa kurithi, wakati wa kuzaliwa kwake... mtu huyo hawezi kuwa raia wa Tanzania wa kurithi."

**URAIA WA TANZANIA WA TAJINISI**

Kwa upande wa uraia wa Tanzania wa Tajinisi, Mtanda anasema kwamba mtu yeyote ambaye si raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuzaliwa au kurithi anaweza kuomba uraia wa Tanzania wa tajinisi.

"Hiyo ni kwa mujibu wa vifungu vya sheria Namba 8 na 9 (1) vya sheria ya Tanzania ya uraia ya mwaka 1995," anasema.

Mtanda anabainisha, kwa mujibu wa sheria hiyo, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya uraia ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, ambaye ndiye mwenye mamlaka ya mwisho ya kutoa au kutotoa uraia wa Tanzania, kwa wageni walioomba uraia.



Baadhi ya wahamiaji haramu kutoka Ethiopia waliokamatwa nchini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Lakini akifikisha umri wa miaka 18, anatakiwa kuukana uraia wa nchi nyingine kama anapenda kuendelea kuwa raia wa Tanzania na akishindwa kukana uraia wa nchi nyingine atakoma kuwa raia wa Tanzania pale atakapozidi umri wa miaka 18,"



Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala (mwenye kipaza sauti).

**SIFA ZAKE NI ZIPI?**

Mtanda anasema, mgeni anayetaka kuomba uraia wa Tanzania anapaswa kuwa na sifa zinazotakiwa.

"Kwanza, mwombaji awe na umri wa miaka 18 au zaidi na awe na uwezo wa kufanya maamuzi yanayokubalika kwa mujibu wa sheria za nchi...awe ameishi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda wa miezi 12 mfululizo kabla ya kutuma maombi ya uraia," anasema na kuongeza:

"Katika muda wa miaka 10 kabla miezi 12, awe ameishi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda usiopungua miaka saba."

Sifa zingine anazozianisha ni pamoja na mwombaji awe anaelewa vizuri lugha ya Kiswahili au Kiingereza lakini pia awe na tabia nzuri.

Aidha, Mtanda anabanisha kuwa awe pia amechangia na ataendelea kuchangia katika kukuza uchumi, sayansi, teknolojia na utamaduni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Na awe amekusudia kuishi moja kwa moja ndani ya nchi ikiwa ombi lake la uraia litakubaliwa," anafafanua.

**TARATIBU ZA KUOMBA URAIA WA TAJINISI**

Kwa upande wa utaratibu wa kuomba aina hii ya uraia, Mtanda anasema kuwa mgeni ambaye ana umri wa miaka 18 na kuendelea anatakiwa kujaza fomu za maombi ya uraia zinazopatikana katika ofisi zote za uhamiaji za wilaya, mikoa, ofisi kuu Zanzibar na Dar- es Salaam.

"Anatakiwa kutoa matangazo ya nia yake ya kuomba uraia mara mbili mfululizo, kwenye gazeti lililosajiliwa Tanzania,"anasema.

**MCHAKATO KUSHUGHULIKIA MAOMBI YA URAIA**

Ili kuhakikisha kuwa wageni wanaopewa uraia ni wale wenye manufaa kwa Taifa, Mtanda anasema maombi yote yanapaswa kupitia na kujadiliwa katika vikao vya kamati za ulinzi na usalama.

"Hiyo ni katika ngazi ya shehia kwa Zanzibar au kata kwa upande wa Tanzania bara...kwamba kata anayoishi mwombaji atahojiwa na ombi lake kujadiliwa na kikao hicho, hatimaye litapelekwa ngazi ya wilaya kwa hatua zaidi," anasema na kuongeza:

"Wilayani, maombi yake yatawasilishwa katika kikao cha ulinzi na usalama cha Wilaya ambacho hujadili maombi ya uraia, hatimaye kutoa maoni na mapendekezo yake katika ngazi ya mkoa,"anasema.

**NGAZI YA MKOA**

Mtanda anasema kwamba katika ngazi ya Mkoa kamati ya ulinzi na usalama ya Mkoa hujadili maombi yaliyowasilishwa na ngazi ya wilaya na kutoa maoni na mapendekezo yake kuhusiana na maombi hayo.

"Hatimaye maombi hayo kwa upande wa Zanzibar hutumwa kwa Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, ambaye hutoa ushauri na mapendekezo yake kwa kamati ya kujadili maombi ya uraia," anasema.

**OMBI LA URAIA WA TAJINISI KWA MTOTO**

Kwa upande wa aina hii ya maombi, Msemaji huyu wa idara anasema waziri mwenye dhamana ya uraia anaweza kuruhusu mtoto wa raia yeyote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupata uraia wa tajinisi.

Anafafanua kuwa hiyo ni baada ya maombi rasmi kuwasilishwa na mzazi au mlezi wa mtoto huyo.

**URAIA WA TAJINISI KWA MWANAMKE ALIYEOLEWA**

Mtanda anabainisha kuwa mwanamke aliyeolewa na raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wowote wa uhai wa mumewe, anaweza kuwasilisha maombi ya uraia wa Tanzania wa tajinisi.

Anasema ombi la uraia kwa mwanamke aliyeolewa linapaswa kuwasilishwa pamoja na viambatanisho vya vielelezo.

"Viambatanisho hivyo ni pamoja na cheti cha ndoa kilichosajiliwa na mamlaka husika nchini, pasipoti ya taifa lake ambayo haijaisha muda wake," anasema na kuongeza:

"Hiyo ni pamoja na uhalali wake wa kuwepo nchini, yaani kibali cha kuishi nchini, pamoja na vielelezo vingine vinavyothibitisha kuwa mume wake ni Mtanzania.

**URAIA WA NCHI MBILI**

Kwa upande wa uraia wa nchi mbili, Mtanda anasema mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18 ambaye ni raia wa Tanzania, anaweza kuwa na uraia wa nchi nyingine.

"Lakini akifikisha umri wa miaka 18, anatakiwa kuukana uraia wa nchi nyingine kama anapenda kuendelea kuwa raia wa Tanzania na akishindwa kukana uraia wa nchi nyingine atakoma kuwa raia wa Tanzania pale atakapozidi umri wa miaka 18," anasema.

**Mwandishi wa Makala haya anapatikana Kanda ya Ziwa kupita namba 0682 869 244**

## ELIMU

NA GRACE MWAKALINGA, MBEYA

# Wazazi, walezi wilayani Mbeya wanyooshewa kidole cha lawama

## ■ Ni kwa kutowapatia wanafunzi wa kike mahitaji yao
## ■ Wakitaka wanafunzi hao wajinunulie wenyewe

WALIMU wa Shule ya Sekondari Nsongwe Juu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamewalalamikia baadhi ya wazazi wa wanafunzi wa Shule hiyo kwa kushindwa kuwapatia watoto wao wa kike mahitaji muhimu, zikiwamo nguo za ndani.

Walimu hao wamedai kuwa asilimia 90 ya wanafunzi wa kike shuleni hapo hawavai nguo za ndani, jambo linalohatarisha afya zao, lakini pia linawafanya wasisome kwa utulivu pale wanapokuwa kwenye siku zao za hedhi.

Mwalimu wa Afya shuleni hapo, Ramla Lui, anasema wazazi wengi wananunulia watoto wao mahitaji ya shule kwa maana ya darasani, lakini hawajali kuwanunulia mahitaji yao binafsi, hususan mavazi.

Anasema hali hiyo inaathiri mazingira ya watoto hao kusoma kwa utulivu na inawaweka katika hatari ya kukumbwa na maradhi ya aina mbalimbali.

"Changamoto ya watoto wa kike kutovaa chupi tuliibaini baada ya binti wa kidato cha kwanza kuadhirika mbele ya darasa akiwa katika hedhi," anasema na kuongeza:

"Sisi walimu wa kike tulifanya jitihada za kumsitiri lakini tukagundua hana utamaduni wa kuvaa chupi, na tulipomuuliza alisema mama yake alimshamwambia ajitegemee kwani ameshakua mtu mkubwa."

**WAANZA UKAGUZI**

Mwalimu Ramla anasema walichukua uamuzi wa kuanzisha ukaguzi wa nguo za ndani kwa mabinti shuleni hapo baada ya tukio la binti huyo.

"Tulibaini wengi kutokuvaa chupi na hata kwa waliokuwa nazo baadhi hazikuwa katika hali ya ubora, tukatoa maagizo kwa wazazi kuhakikisha kila binti ananunuliwa nguo za ndani zisizopungua tano na taiti tano na pia wahakikishe wanaoga walau mara mbili kwa siku," anasema na kuongeza:

"Wazazi wamekuwa mbali na watoto wao, hawawapatii elimu ya kujisitiri hasa pale wanapoanza kupata hedhi kutoka[...] na kutokuwa na nguo za ndani na p[...]

Anasema utaratibu wa ku[...] watoto wa kike mara kwa [...] saidia kubaini changamoto mbalimbali zinazowakabili watoto hao, ikiwemo ya kubeba jukumu la kujitafutia mahitaji ya shule kwa kufanya vibarua.

"Tumeweka utaratibu wa kuwakagua watoto wa kike kila wiki... tumeona wengi wao hawavai chupi na badala yake wanavaa kaptula ambazo ni kubwa," anasema na kuongeza:

"Tulipobaini hali hii, tuliwaita wazazi ili kuwaeleza lakini mwitikio wake umekuwa mdogo, kwani wengi hawajatekeleza maagizo tuliyowapa na badala yake wamewaachia watoto wajinunulie wenyewe nguo hizo," anasema.

Mwalimu Ramla anabainisha kwamba baadhi ya wanafunzi wanasema kuwa wazazi wao hawana muda wa kuwa karibu nao kusikiliza au kujua mahitaji yao, badala yake wamejikita zaidi kwenye shughuli za uzalishaji kama vile kilimo.

> "Kampeni hii imelenga kuwafikia watu wote kulingana na mazingira yao... jamii bado inawajibu wa kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia... hii ni kwa mujibu wa sheria ya mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 na mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya watoto na wanawake,"



Walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Nsongwe Juu, wakipata elimu ya kampeni ya ulinzi wa mtoto yenye kaulimbiu isemayo, 'Mtoto Afurahie Utoto Wake, Ujana Wake na Uzee Wake" kutoka kwa Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa, Flora Mlowezi (aliyesimama) akieleza juu ya Kampeni ya Mtoto wa Kike inayoratibiwa na TGNP. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**



Mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza Shule ya Sekondari ya Nsongwe Juu Wilayani Mbeya, Elementia Mashazo (aliyesimama kushoto), akionyesha matumizi ya Pedi mbele kwa wanafunzi na Walimu.

**WANAFUNZI WANENA**

Elemetia Mashazo ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule hiyo.

Anasema wazazi wake hawajawahi kumnunulia nguo za ndani na badala yake hulazimika kufanya vibarau ili apate fedha za kujinunulia mahitaji yake hayo muhimu.

Anasema hulazimika kufanya vibarau kwasababu wazazi wake hawana utaratibu huo.

"Kwa mwaka huu tayari nimekwishajinunulia mwenyewe nguo za ndani, lakini hazitoshi...nitajitahidi kuongeza zingine ili kukidhi mahitaji kama walimu walivyoelekeza kuwa kila mwanafunzi wa kike awe na chupi tano na taiti tano," anasema.

**FAINES JACKSON**

Kwa upande wake Faines Jackson ambaye ni Mwanafunzi wa Kidato cha tatu katika shule hiyo anasema wazazi wengi kwa sasa hawako karibu na watoto wao kwa sababu ya kujikita zaidi kwenye shughuli za uzalishaji mali na baadhi yao kuendekeza ukali.

Anasema upungufu huo upande wa wazazi husababisha binti kujiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi na wanaume ili apate fedha za kukidhi mahitaji yake ikiwa ni pamoja na kununua nguo za ndani.

Aidha, Fainess ambaye pia ni Mwenyekiti wa Klabu ya Genda katika shule hiyo anazungumzia vilevile vitendo vya ukatili wa kingono vinavyowapata baadhi ya wanafunzi wa kike.

Anasema vitendo vya ukatili wa kingono bado ni changamoto kwa sababu vimesababisha baadhi ya wanafunzi wenzao kukatishwa masomo.

"Nina imani kupitia klabu hii tutaweza kupeana elimu vilevile ya masuala mbalimbali yakiwamo ya ukatili wa kijinsia, lakini pia kuungana pamoja kukemea vitendo hivi," anasema.

**OFISA ELIMU KATA**

Ofisa Elimu Kata ya Ijombe, Ntabuli Mwakifuna, anasema utandawazi umesababisha wazazi kusahau wajibu wao wa kuwatimizia watoto wao wa kike mahitaji yao muhimu.

"Wanaamini kuwa kutokana na teknolojia binti akikua atajifunza mwenyewe namna ya kujihudumia na kujisitiri akiwa hedhi...matokeo yake ni kwa mabinti kushawishika na zawadi au fedha kutoka kwa wanaume ili waweze kupata fedha za kununulia nguo za ndani pamoja na pedi," anasema na kuongeza:

"Naomba wadau na serikali tuendelee kuwaelimisha wazazi kuwatimizia mabinti mahitaji yao muhimu...hii itasaidia kupunguza majanga ya mimba za utotoni na ukatili wa kingono, hivyo kuwezesha watoto wetu kuzifikia ndoto zao."

**WAZAZI**

Magreth Mwalizi ni Mkazi wa kijiji cha Nzongwe Mandaji.

Anakiri baadhi ya wazazi na walezi kushindwa kuwanunulia mabinti zao nguo za ndani wakidai hawana fedha.

"Kwa upande wangu ninawajibika kumnunulia nguo cha ndani binti yangu lakini si kwa kiwango kinachotakiwa kutokana na umaskini nilionao," anasema.

Anabainisha kwamba anatambua umuhimu wa mtoto wa kike kununuliwa mahitaji yake lakini changamoto ni hali ya kipato hasa kwao wanaoishi maeneo ya vijijini.

Anachosema Magreth ndicho anachokibainisha Betina Anthony, Mkazi wa Kijiji cha Nzongwe Mandaji.

Anasema ni jukumu lake kama mama kumnunulia nguo za ndani mtoto wake, ila tu ukata wa fedha unaosababishwa na hali ya maisha umekuwa kikwazo cha kutimiza jukumu hilo licha ya kutamani kufanya hivyo.

**KAMPENI YA ULINZI WA MTOTO**

Kwenye siku ya Maadhimisho ya Wanawake Duniani, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), uliadhimisha siku hiyo kwa kutoa Elimu na kuzindua Kampeni ya Ulinzi wa Mtoto dhidi ya Ukatili wa kingono kwenye shule za Sekondari wilayani Mbeya.

Sababu ya kuzindua kampeni hiyo ni kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto, ambapo katika ripoti iliyotolewa Juni 2018 na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) inaonyesha kuwa wastani wa watoto 394 walibakwa kila mwezi katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi, anasema ripoti hiyo inaonyesha kuwa vitendo vya ulawiti kwa watoto vimeongezeka kutoka matukio 12 kwa kipindi cha Mwezi Januari hadi Juni 2017 hadi matukio 533 mwaka 2018 katika kipindi hicho.

Na mikoa inayoongoza kwa matukio hayo ni Dar es Salam na Iringa.

Lilian anasema kampeni hiyo inachangia jitihada za Serikali kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya watoto kupitia Mpango wa Taifa wa Kutokomeza vitendo hivyo kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), kwa asilimia 50 ifikapo 2022.

Anasema jukumu la TGNP ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za ukatili wa kingono kwa watoto na umuhimu wa kuwalinda, kutathmini na kuibua mijadala katika jamii juu ya hali halisi ya vitendo hivyo.

"Kampeni hii imelenga kuwafikia watu wote kulingana na mazingira yao... jamii bado inawajibu wa kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia... hii ni kwa mujibu wa sheria ya mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 na mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya watoto na wanawake," anasema Lilian.

Anabainisha kuwa TGNP inaamini kila mtu atatimiza wajibu wake vizuri wa kumlinda mtoto na kwamba wanaitaka jamii kuchukua hatua za kumlinda mtoto popote alipo.

**VITUO TAARIFA NA MAARIFA**

Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa wilayani Mbeya, Flora Mlowezi, anasema vituo hivyo ambavyo vimejengewa uwezo na TGNP vimekuwa chachu kubwa ya kuleta mabadiliko katika jamii.

Anasema miongoni mwa mabadiliko wanayoendelea kuyafanya ni vita dhidi ya ukatili wa kingono kwa watoto hususani wa kike.

"Tumeamua kuanzisha kampeni hii ili kumlinda mtoto wa kike dhidi ya

vitendo vya ukatili,\' anasema na kuongeza:

"Tuna imani itasaidia kuibua na kuripoti masuala hayo pindi yanapotokea na lengo letu ni kuhakikisha jamii inaguswa na tatizo la ukatili wa kingono dhidi ya watoto wakiwa ndani na nje ya shule."

---

JIELIMISHE



Watu wengi hutumia huduma za intaneti kama anavyoonekana raia huyu. **PICHA: MTANDAO**

# Serikali za Kiafrika na intaneti

## ■ Si Facebook, Twitter wala WhatsApp

NI jambo linalozidi kuwa la kawaida katika baadhi ya mataifa ya Afrika, ambako serikali zimezima mara kwa mara intaneti au kuzuia mitandao ya kijamii.

Mwaka mmoja umepita tangu Chad ilipobana mitandao maarufu ya kijamii na miezi kadhaa baada ya mawasiliano ya intaneti kufungwa katika miji muhimu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) baada ya uchaguzi mkuu.

Sudan ilibana nafasi ya raia kuingia katika mitandao wakati wa maandamano dhidi ya serikali kama ilivyokuwa nchini Zimbabwe.

Wanaharakati wa dijitali wanasema hilo ni kubana taarifa, lakini serikali zinadai inasaidia kuimarisha usalama. Basi serikali inafanikiwa vipi kufunga au kubana mitandao?

Serikali inaweza kubana matumizi ya intaneti kwa kuagiza kampuni zinazotoa huduma za intaneti (ISPs) kudhibiti au kubana uwezo wa wateja kuingia katika mitandao. Mara nyingi huwa kuna kizuizi kinachowekwa kwa wateja kutofika katika mitandao ya kijamii inayotumika sana.

Kama hatua kali zaidi, serikali inaweza kuagiza kufungwa kabisa huduma nzima ya intaneti.

Mnamo mwaka 2018, kulikuwa na visa 21 ambapo intaneti ilifungwa kwa kiwango fulani au kabisa, ikilinganishwa na visa 13 mnamo mwaka 2017 na visa 4 mwaka 2016, kwa mujibu wa kundi la uangalizi la kujitegemea Access Now.

Ivory Coast, DRC, Chad, Cameroon, Sudan, Ethiopia, Mali, Nigeria na Sierra Leone zilibana intaneti mwaka jana. Ni mtindo unaodhihirika duniani kote. Mnamo 2018, kulikuwa na visa 188 vya intaneti kubanwa ikilinganishwa na 108 mwaka 2017 na 75 mwaka 2016.

Katika kila nchi, ni uamuzi wa kampuni zinazotoa huduma hiyo ya intaneti kutekeleza maagizo ya serikali kubana intaneti.

Mfumo mmoja unaotumika unafahamika kama URL-based blocking. Huu ni mfumo unaohusisha kuweka kizuizi kinachozuia wateja kuingia katika mitandao iliyopigwa marufuku. Mteja anayejaribu kuingia katika mitandao hiyo hupata ujumbe "server not found" au mtandao haupatikani, umezuiwa na msimamizi wa mtandao.

Mfumo mwingine unafahamika kama 'throttling'.

Mbinu hii huzuia kwa kiwango kikubwa idadi ya wateja wanaotembelea mtandao maalum, na kutoa hisia kwamba kasi ya huduma ni ndogo na kuwafanya wateja waelekee kwingine.

Hili ni la afueni, kwasababu ni vigumu kutambua iwapo mitandao inazuia wazi au ni kutokana na upungufu wa miundombinu duni.

Kama hatua ya mwisho, kampuni za mawasiliano zinaweza kutakiwa kufunga kabisa huduma kwa ujumla na kuzuia wateja kupokea data yoyote.

**JE KAMPUNI ZINAWEZA KUSEMA 'HAPANA?**

Uwezo wa serikali kubana intaneti unategemea uwezo wao kudhibiti kampuni za mawasiliano nchini. Kampuni za kutoa huduma ya mawasiliano zinapewa vibali na serikali, jambo linalomaanisha kwamba huenda wakatozwa faini au wakapoteza mikataba.

Huenda wateja wakawa na haki ya kukata rufaa mahakamani, lakini kiuhalisi ni aghalabu kuona hilo likifanyika. Mapema mwaka huu Mahakama nchini Zimbabwe, iliamua kurudishwa huduma ya intaneti baada ya serikali kuagiza ibanwe.

Kwa upande wake serikali ya Zimbabwe imeidhinisha sheria mpya zinazoipa udhibiti mkubwa katika matumizi ya intaneti.

Waziri wa Habari Zimbabwe, Monica Mutsvangwa anasema hili "litahakikisha kwamba intaneti na teknolojia zinazohusika zinatumika kwa manufaa ya jamii, na sio kukiuka usalama wa kitaifa."

Lakini kuna mifano pia ambapo serikali zinazotaka kufunga intaneti zinakuwa na urahisi wa kulitekeleza hilo.

"Kuna mataifa kama Ethiopia ambapo sekta ya mawasiliano ya simu bado iko chini ya serikali," anasema Dawit Bekele, Mkurugenzi wa Ofisi za Afrika za Jamii ya Intaneti.

"Kama intaneti imefungwa kabisa kuna namna ambazo wateja wanaweza kutumia kuepuka vizuizi vilivyopo na kuingia katika mitandao," anaongeza.

Mbinu inayofahamika sana ni ya kutumia mitandao inayoruhusu kuruka vizuizi (VPNs).

Mitandao hii huwa kama njia, inayofanya kuwa vigumu kwa kampuni ya kutoa huduma za intaneti kuweka vizuizi kwa mitandao iliyopigwa marufuku. Serikali zinaweza pia kuzuia VPNs, lakini si sana kushuhudiwa kufanya hivyo kwasababu hutatiza shughuli za wanadiplomasia na kampuni kubwa zinazotegemea intaneti kwa shughuli zao.

Baadhi ya mataifa yametaja sababu ya kusambaa kwa 'habari za uongo' katika mitandao kama sababu ya kuidhinisha vikwazo hivyo.

Lakini wachambuzi na viongozi wa upinzani wanataja hii kuwa sababu ya kukandamiza makundi yanayozikosoa serikali, ambayo hutumia mitanda kama Facebook na WhatsApp kujipanga. **BBC**

RIPOTI

# Utekelezwaji adhabu ya kifo wapungua duniani

RIPOTI ya kila mwaka ya Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Binadamu la (Amnesty International-AI), inaonyesha kuwa hukumu za kifo zilizotekelezwa zimepungua.

Chiara Sangiorgio, ni wakili anayepinga adhabu ya kifo katika shirika la Amnesty International na anasema kuwa kulikuwa na matukio machache sana ya kutekelezwa hukumu za kifo katika nchi kama vile Iran, Pakistan na Iraq mwaka uliopita, ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Mafanikio hayo hata hivyo yametiwa doa na tamko la karibuni la Sultan Hassanal Bolkianah, kuwa watu wanaopatikana na hatia ya kufanya vitendo vya kishoga au uzinzi nchini Brunei watahukumiwa kifo kwa kupigwa mawe.

Desemba mwaka jana, mataifa 121 kati ya 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN), yalipiga kura ya kusitishwa adhabu ya kifo.

Ni mataifa 35 pekee yaliyopinga muswada huo, huku 32 yakijiepusha kupiga kura.

Hatua hiyo ya kutia moyo imelifanya shirika la Amnesty International kutangaza kuwa adhabu ya kifo inakaribia kuondolewa kabisa duniani.




Mwaka jana, Burkina Faso ilifuta adhabu ya kifo. Gambia imetangaza sheria ya kuzuia utekelezwaji wa hukumu ya kifo na inatafakari kuondoa kabisa adhabu ya kifo.

Serikali mpya ya Malaysia imesitisha utekelezwaji wa adhabu ya kifo, japo bila kuthibitisha hatua hiyo.

Jimbo la Washington nchini Marekani, limepitisha uamuzi kuwa adhabu ya kifo ni kinyume cha katiba.

AI iligundua kuwa Iran iliwanyonga watu 253 katika mwaka wa 2018, ikiwa ni zaidi ya nusu ya idadi ya mwaka wa 2017.

Sababu kuu, kwa mujibu wa shirika hilo, ni kuwa sheria iliyofanyiwa marekebisho ya Iran kuhusu dawa za kulevya, kumaanisha kuwa watu sasa lazima wapatikane na dawa nyingi za kulevya ili kuhukumiwa adhabu ya kifo.

Nchini Pakistan watu 14 waliamriwa kunyongwa, ukilinganisha na watu 250 walionyongwa mwaka wa 2017.

AI kwa mara nyingine inaiorodhesha China kuwa nchi inayotekeleza idadi kubwa ya hukumu ya kifo duniani.

Shirika hilo linakadiria kuwa China huwanyonga maelfu ya watu kila mwaka.

Idadi kamili hata hivyo haipatikani kwa urahisi kwa sababu China inayafanya matukio hayo kisiri.

Mwaka jana, Saudi Arabia ilitangaza kuwanyonga watu 149, wengine wao kwa kukatwa vichwa hadharani.

Taifa hilo la kifalme linasema linachapisha takwimu hizi ili kuwazuia watu wanaopanga kufanya uhalifu.

Wakati huo huo, Misri iliwanyonga watu 43 mwaka wa 2018 na kuwahukumu kifo watu 717, wengi wao kwa makosa yanayohusiana na machafuko ya kuchochewa kisiasa na ugaidi.

Kwa mujibu wa serikali ya Vietnam, watu 85 walinyongwa mwaka jana nchini humo.

Na Japan na Singapore zikawanyonga watu 15 na 13, ikiwa ni idadi kubwa kuliko miaka ya nyuma.

Kulikuwa na nchi nne tu kutoka Kusini mwa jangwa la Sahara ambazo zilitekeleza hukumu ya kifo mwaka jana.

Somalia, Sudan Kusini, Sudan na Botswana. Nchi 17 za kiafrika zimeondoa aina hiyo ya adhabu.

**DW**

JE, WAJUA?

# Tembe za uzazi wa mpango kwa wanaume zapita jaribio la awali

TEMBE ya kupanga uzazi ya wanaume imepita majaribio ya awali kwa matumizi ya binadamu, wataalamu katika mkutano mkuu wa afya wamearifiwa.

Tembe hiyo ya kutumiwa mara moja kwa siku, ina homoni zilizoundwa kusitisha uwepo wa manii au shahawa.

Inaongeza njia za ziada za kupanga uzazi kwa wanaume, mbali na matumizi ya kondomu na upasuaji wa mirija ya uzazi, mbinu za pekee zinazotumika sasa kwa wanaume.

Hata hivyo madaktari katika kongamano la mwaka la Endocrine Society wameelezwa kwamba huenda ikachukua mwongo mmoja kabla ya dawa hizo kuwa madukani.



Daktari akitoa ufafanuzi juu ya uzazi wa mpango kwa wanaume. **PICHA: MTANDAO**

**SINTOFAHAMU**

Kwa nini tembe ya wanaume inaonekana kuwa ngumu kuidhinishwa wakati tembe ya kupanga uzazi kwa wanawake ilizinduliwa Uingereza miaka 50 iliyopita?

Jibu linalotolewa na baadhi ya watu wanasema kwamba hakujawa na azma ya kijamii na kibiashara kushinikiza uzinduzi wake.

Hata hivyo, matokeo ya utafiti wa maoni yanaashiria wanaume wengi wangependa kuitumia iwapo ingepatikana.

Mjadala ni iwapo wanawake watawaamini wanaume kumeza tembe hizo kama inavyostahili.

Kibaiolojia, changamoto ya kuunda tembe ya homoni kwa wanaume ni katika kuhakikisha kwamba haiathiri hamu ya tendo la ndoa au kupunguza uwezo wa mwanamume kushiriki tendo hilo.

**UWEPO WA MANII**

Kwa wanaume walio na uwezo wa kuzalisha, seli mpya za manii zinaundwa katika sehemu nyeti za wanaume kutokana na homoni.

Hivyo kuzuia kwa muda hali hii bila ya kupunguza viwango vya homoni kwa kiwango stahili kiasi cha kuonekana madhara yake ni muhimu.

Lakini tembe hii ya wanaume, inayofanyiwa majaribio na watafiti kutoka taasisi ya LA BioMed na Chuo Kikuu cha Washington, inatarajiwa kufikia lengo hilo, watafiti wanasema.

Majaribio ya awali ya 'awamu ya kwanza' yaliyofanywa kwa wanaume 40 yalikuwa na matokeo mazuri, wataalamu hao waliwaeleza wajumbe katika mkutano huo uliofanyika New Orleans.

Katika utafiti huo wa siku 28, wanaume 10 walikunywa mfano wa tembe hiyo na 30 walikunywa tembe hiyo ya majaribio ya kupanga uzazi kwa wanaume, 11-beta-MNTDC.

Na miongoni mwa waliokunywa dawa ya androgen, viwango vya homoni inayohitajika kuunda manii ilipunguwa pakubwa, ikilinganishwa na waliokunywa mfano wa tembe hiyo, na walirudi kwenye hali ya kawaida baada ya kumalizika majaribio.

**MATATIZO YA KUSHIRIKI TENDO LA NDOA**

Madhara yake kwa upande mwingine yalikuwa machache na madogo.

wanaume watano waliokunywa tembe hiyo waliarifu kupungukiwa na hamu ya kushiriki tendo la ndoa, huku wengine wawili wakieleza kukabiliwa na matatizo ya kuweza kushiriki tendo hilo, lakini shughuli yenyewe haikupungua.

Hakuna mshiriki aliyeacha kunywa dawa kutokana na madhara na ilipitia viwango vyote vya usalama wa matumizi.

Watafiti walioshughulika, Prof Christina Wang na wenzake, wamefurahia hatua hiyo lakini wana tahadhari kuhusu matokeo yake.

"Matokeo yetu yanaonyesha kwamba tembe hiyo inayojumuisha mifumo miwili ya homoni kwa pamoja itapunguza utengenezaji wa manii huku ikilinda uwezo wa kushiriki tendo la ndoa," anasema.

Lakini majaribio makubwa na ya muda mrefu zaidi yanahitajika kuangalia iwapo zitafanya kazi kama dawa za kupanga uzazi zinavyohitajika.

**KUBADILIKA TABIA**

Wanasayansi wengine wamekuwa wakishughulika kuunda dawa ya upangaji uzazi kwa wanaume kupitia sindano watakayochomwa wanaume kila baada ya miezi miwili.

Lakini waliachana na mpango huo na hawakuendelea na awamu ya pili ya utafiti huo kwa kuangalia usalama na ufanyaji kazi wa sindano hiyo baada ya baadhi ya wanaume waliojitolea kuripoti madhara, ikiwemo kubadilika tabia au msongo wa mawazo.

Kwa wanaume ambao hawapendi kumeza dawa za homoni, watafiti wamekuwa wakitafuta njia ya kuzuia mbegu kusafiri na kuzisitisha kutoka kwenye uume, katika mbinu ya kudumu, isiyohusisha upasuaji wa mishipa ya uzazi kwa wanaume.

**SOKO LA UUZAJI DAWA**

Prof. Richard Anderson, wa Chuo Kikuu cha Edinburgh, anaongoza utafiti huo Uingereza utakaofanya majaribio ya matumizi ya mafuta ya kupakwa mwilini mwa mwanamume.

Anasema sekta ya famasia imejivuta kukubali mbinu mpya ya kupanga uzazi kwa wanaume ambayo itapokewa vizuri na wanaume wenyewe na hata wanawake.


"Nadhani sekta hiyo haijashawishika kuhusu wateja katika soko hilo...imekuwa hadithi ndefu kwa kweli sehemu ya tatizo ikiwa ni ukosefu wa uwekezaji," anasema.

**BBC**

SAYANSI

NA MICHAEL ENEZA

# Mnyamakale mwingine apatikana Rukwa, jina lake latolewa kitaaluma, si Kiswahili



Aina ya 'dinosaur' (wanyama kale wenye maumbile makubwa), kama aliyegunduliwa Rukwa. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI bado baadhi ya wahafidhina au wapigadebe katika Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) wakifurahia kutolewa jina la Kiswahili kwa aina moja ya 'dinosaur' (wanyama kale wenye maumbile makubwa wanaosadikiwa kisayansi kuwa waliteketea zaidi ya miaka milioni 60 iliyopita) kuna ugunduzi mwingine umeripotiwa hivi karibuni.

Ni wa mnyama wa aina ya 'dinosaur' wa kundi la wanyama wanaonyonyesha (mammals) aliyegunduliwa katika eneo la Bonde la Ufa mkoa wa Rukwa na kupewa jina linaloendana na hapo alipogunduliwa.

Ila mnyambuliko mzima wa jina hilo unaoainishwa na aina ya 'dinosaur,' sifa zake, alipokutwa.

Wakati baadhi ya wachunguzi wa habari wakitazamia kuwa mnayamakale aliyegunduliwa mapema mwaka huu hapa nchini na kupewa jina la Kiswahili angebadilishiwa jina hilo liendane na yale ya kisayansi, inaelekea kuwa wataalamu katika Chuo Kikuu cha Ohio nchini Marekani, walioshirikiana na wenzao hapa nchini katika utafiti na ugunduzi huo, hawana haraka kubadilisha jina.

Taarifa au matumizi ya jina lililowekwa awali hazijabadilika, licha ya kuwa bado si muda mrefu tangu ugunduzi huo ufanyike mwezi Februari mwaka huu na jina kutolewa.

Ni mnyama kale 'dinosaur' mwenye mkia unaofanana na moyo (yaani jinsi moyo unavyochorwa, si jinsi ulivyo).

Wanyama wote wawili waliogunduliwa hivi karibuni wanatoa picha tofauti kwa upande mmoja na zinazofanana kwa upande mwingine kuhusu kilichotokea zama hizo katika kusambaa kwa wanyama kale, walivyokuwa wanaishi na kuweka vielelezo zaidi vya kuharibika kwa mazingira yao na kupotea.

Ni sehemu ya nadharia ya 'evolution' yaani mabadiliko ya maumbile ya wanyama na baadaye kutokea watu, licha ya kuwa dhana hiyo bado inapingwa na wanaopendelea mapokeo ya dini kuhusu uasili wa binadamu kuwa hawezi kutokana na wanyama.

Ugunduzi wa Tanzania wa sasa hivi hauhusiani na ubishi huo, tofauti na ule wa Olduvai Gorge, mwaka 1959.

Ugunduzi wa Olduvai Gorge ulifanywa na wanandoa Richard na Mary Leakey, watalaamu wa chuo kikuu waliohisi kuwa maeneo ya Bonde la Ufa yana mabaki muhimu halafu wakaanza kufukua taratibu eneo lenye viashiria karibu na mapango yenye michoro kale ya Kondoa Irangi.

Ugunduzi huo ulichangia kwa kiasi kikubwa kuinua dhana ya 'evolution' (mabadiliko kimaumbile) iliyowekwa wazi rasmi miaka 100 iliyotangulia, 1859 wakati mtafiti mimea/wayama wa Uingereza Charles Darwin alipotoa kitabu 'Origin of Species by Natural Selection' au kwa kifupi 'The Origin of Species.'

Kuanzia wakati huo sayansi ikaenda njia moja; udhanifu/dini njia nyingine.

> "Hivyo mnyamakale mpya aliyegunduliwa Rukwa anaitwa Galulatherium jenkinsi, ambako Galula ni eneo la miamba ya mabaki hayo yalipopatikana, wakati 'therium' inaonyesha kundi la wanyamakale kwani 'therium' ni mnyama kwa Kilatini.

Kutokana na hisia kwamba Bonde la Ufa la Afrika lina hazina ya mtawanyiko na mazingira ya kuishi kwa wanyamakale tofauti, na hata binadamu wa awali na mabadiliko ya maumbile yao, si jambo la kushangaza kuwa Tanzania, yenye eneo la Bonde la Ufa refu kuliko Kenya au Ethiopia kwa upande mwingine, imekuwa ikifuatiliwa kwa kina na wataalamu.

Chuo Kikuu cha Ohio nchini Marekani ni moja ya vyuo vyenye idara kubwa za utafiti wa mambokale, kuhusu wanyama, binadamu, mimea, miamba, wadudu, n.k.

Ndiyo waliotoa jina la Kiswahili la mnyama aliyegunduliwa Februari, kuwa anaitwa 'Mnyamawamtuka moyowamkia' ambako Mtuka ndiyo eneo alipogunduliwa mnyamakale huyo, na 'mnyama' ikasimama badala ya 'dinosaur' au kielelezo chake.

Kutoa jina kunahusiana na kutoa picha inayoeleweka kitaaluma, kama jinsi ukisikia jina la mtu haraka unapata picha ya mambo kadhaa, ikiwamo jinsia, utaifa au kabila anakotoka, na mara nyingine unapata picha haya ya dhehebu la dini, kwani majina mengine hayarudiwi kwingine, ila kwa nadra.

Jarida la utafiti la chuo kikuu hicho lilizungumzia 'dinosaur mpya anayefaa moyo wake mkiani' katika utafiti uliokuwa hasa unafuatilia mabadiliko ya taya la chini la aina hizo za wanyama wa kipindi hicho, hasa katika Bonde la Ufa na Afrika nzima kwa jumla.

Kuna kundi la wanyama wa Kusini ya Ikweta waliokuwa wananyonyesha, wakiitwa kitaalam 'gondwanatherians,' yaani wanyama wa dunia ya gondwana (therians ni kama earth-erians, waliokuwa duniani wakati wa gondwana).

Dhana ya gondwana ni kuleta ubishi mkubwa miongoni mwa wanataaluma na si rahisi kusema kama kuna tamati halisi au ubishi uliendelea, kwani ilionekana kuwa kuna miingiliano ya wazi kijiografia na hata maumbile ya miamba kwa mabara yaliyo mbali sana, kwa mfano Brazil Kaskazini Mashariki na Cameroon.

Mwingilio wa umbo la mabara hayo unaashiria kuwa yalikuwa pamoja katika dude kubwa la 'gondwana' halafu yakatengana.

Baadhi wanakataa nadharia hiyo wakisema kuwa dude (bara moja kubwa la gondwana) lisingegawanyika kwani likikatika vipande, hayo mabara kadhaa yanayoundwa 'yasingeweza kwenda popote,' yaani hakuna nafasi hiyo.

Hata hivyo, suala la msingi hapa ni uoanishaji wa jina la mnyamakale na sifa kadhaa za utambulisho wake, ambako sehemu aliyopatikana ni sifa mojawapo tu na siyo ya msingi kuliko zote.

Halafu kuna suala la uhalisia wa lugha ya kitaaluma kuwa lazima ibaki na msingi mmoja.

Hivyo vianzio vya lugha hiyo ni Kiyunani (kwani mchunguzi wa kwanza wa wanyama na mimea, kutoa orodha ya aina zake na tofauti zao kwa kina) alikuwa Aristotle, mfikiriaji na mtafiti wa Uyunani ya kale, takriban miaka 300 kabla ya Kristo.

Ni lugha ambayo pia imeingiliana na Kilatini (lugha ya Rumi ya kale) na kusambaa kama chembe kwenye lugha tofauti barani Ulaya.

Eneo lingine ambalo jina linasaidia kutambua ingawa si muda wote ni kipindi alichoishi mnyamakale husika, ingawa upana wa muda wa uwepo wa aina hiyo ya wanyama tayari ni kielelezo muhimu cha muda na pia aina ya miamba ambako mnyamakale alipatikana.

Mara nyingi miamba hiyo inakuwa ndiyo kielelezo cha muda wa huyo mnyamakale, na pia mgunduzi wa mnyama huyo anaweza kuingizwa katika jina kwa utambulishuo.

Ina maana kuwa mnyamakale alipoonekana ni chembe mojawapo ya utambulisho, lakini mara nyingi aliyemgundua anaacha alama muhimu zaidi, kwa mfano mtaalamu aitwaye Jenkins atakumbukwa zaidi kuliko tarafa ya Mtuka.

Hivyo mnyamakale mpya aliyegunduliwa Rukwa anaitwa Galulatherium jenkinsi, ambako Galula ni eneo- la miamba ya mabaki hayo yalipopatikana, wakati 'therium' inaonyesha kundi la wanyamakale kwani 'therium' ni mnyama kwa Kilatini.

Halafu mgunduzi anaingizwa, ila jina lake litamkwe kwa mtiririko huo wa Kiyunani na Kilatini kwa kuongeza herufi moja tu inayoendana na mtiririko wa jina lake, kwa mfano jenkinsi.

Ila huyu mtajwa katika ugunduzi huu siyo aliyegundua bali ni kwa kumbukumbu ya mwanasayansi na mwalimu wa muda mrefu aliyekwishafariki, akiacha wataalamu maridhawa aliowafundisha, yaani Profesa Farish Jenkins aliyekuwa Chuo Kikuu cha Harvard nchini Marekani na anayesifiwa kwa kuunga mkono kwa dhati utafiti huko Rukwa.



WADAU
SABATO KASIKA

# ELIMU ya uhusiano na jinsia ni muhimu kwa watoto ili waweze kujitambua na kujua nini wanachotakiwa kukifanya. Je, muda umefika sasa iingizwe katika mitaala shuleni?

Wadau wanajadili.



**JUDITH MREMI (MWALIMU MNAZI MMOJA SEKONDARI, DAR)**

ZAMANI wazazi walikuwa wanasubiri hadi watoto wao wavunje ungo au wabalehe ndipo wapewe elimu ya jinsia, lakini kwa dunia ya leo, ninadhani ipo haja kwa watoto kupata elimu wakiwa na umri wa kuanzia miaka saba.

Ninasema hivyo kwa sababu utandawazi umeleta mambo mengi ambayo watoto wanafahamu vitu vingi bila wazazi kujua kupitia televisheni na hata simu.

Hivyo kuendelea kusubiri hadi mtoto avunje ungo au abalehe ndipo apewe elimu hii, hapa mzazi atakuwa amechelewa sana. Kubalehe au kuvunja ungo ni hatua muhimu ambayo mtoto anapitia kuelekea kwenye utu uzima.

Sasa kama atafikia hatua hiyo bila kuwa na elimu ya mahusiano na jinsia anaweza kujikuta katika mazingira mabaya hapo baadaye. Wastani wa kubalehe na kuvunja ungo kwa wasichana ni miaka 9 hadi 12 kwa sasa, ingawa miaka ya zamani ilikuwa kuanzia miaka 12-14.

Baada ya kuvunja ungo, binti anakuwa na uwezo wa kushika mimba, japokuwa uwezekano huongezeka zaidi kati ya miaka 20-30. Watoto wanatakiwa kufikia umri huo wakiwa wanajitambua au wanaelewa kila kitu, hivyo ni wajibu wa wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao wanaanza kupata elimu hii wakiwa na umri wa kuanzia miaka saba, ambao kwa maoni yangu ninaona ni sahihi kabisa kwa kizazi hiki cha Sayansi na Teknolojia.

Vilevile sioni tatizo elimu hii kuingizwa kwenye mitaala kwa ajili ya kupanua uelewa wa wanafunzi zaidi. Siku hizi tunaweza tukapotoshwa zaidi, tena kwa makusudi, na vipindi kwenye vyombo vya upashanaji habari vinavyopuuzia msimamo sahihi upande wa jinsia na uzazi, ukiwa ni pamoja na usafi wa moyo na hata uhai wa watoto.

Hivyo ni muhimu kulenga kwenye ukomavu na uadilifu kwa bidii zote na kwa kujiombea msaada wa neema ya Mungu.



**EZEKIEL NICHOMBE (MWALIMU MKUU S/MCHANGANYIKENI DAR)**

ELIMU hii ikiingizwa kwenye mitaala inaweza kuwa na mchango mkubwa wa kuwasaidia watoto tofauti na ilivyo sasa.

Kwa sasa ni kwamba wanafunzi wamekuwa wakisaidiwa na walimu wa nidhamu kwenye mambo ya elimurika na ushauri nahasa hasa kwa wale waliopevuka.

Lakini kama itaingizwa kwenye mitaala itafundishwa kwa upana zaidi ili waweze kuelewa. Kadiri mtoto anavyozidi kukua anahitaji kujifahamu kijinsia aweze kukomaa na hatimaye kuzaa kadiri ya mpango wa Mungu.

Ndiyo sababu ni muhimu kupata elimu ya jinsia mapema na ikiwezekana kuanzia utoto na kukamilishwa kabla mtu hajajichagulia jinsi ya kuishi ili aweze kujua anafanya nini au anaacha nini.

Ingawa ni suala pana la kijamii, lakini kimsingi kama nilivyosema elimu hii inatakiwa kuingizwa kwenye mitaala na pia wazazi wana wajibu mkubwa katika jambo hili kwani baadhi ya wazazi familia zao huwatendea wavulana na wasichana namna tofauti. Imeshakuwa kawaida kufanya hivyo, na wanaona hakuna sababu ya kubadilika.

Matokeo yake, tabia hii yenye msimamo usiobadilika imesababisha, hususan wasichana, kuamini kwamba hivyo 'ndivyo namna mambo yalivyo' na hakuna chochote kinachoweza kufanyika hapo. Wavulana pia wanaikubali hali hii kwa sababu inaelekea kuwanufaisha.

Mwalimu anaweza kuchunguza tofauti hizi pamoja na wanafunzi wake kwa kufanya kazi katika makundi ya jinsia moja ili kuwasaidia wazungumze kuhusu tabia na imani zao.

Kimsingi malezi ya kijinsia na hata elimu ya jinsia ni sehemu muhimu ya malezi inayolenga kumsaidia mtoto kukabili vyema hali yake ya kuwa mwanamume au mwanamke ili jinsia imjenge badala ya kumvuruga.

Wavulana wanaongelea siri zao wasitake wasichana wazijue, na wasichana wanafanya vilevile kati yao.



**FARES KAJIRU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**


NIFAFANUE hili neno jinsia kwamba ni mahusiano ya kijamii na kiutamaduni yanayozingatia mgawanyo wa majukumu kwa kuangalia jinsia ya kike na kiume. Jinsia inachangia kuwapo kwa tofauti kati ya mwanamume na mwanamke katika mgawanyo wa majukumu kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Kwa njia hii majukumu, kazi, matarajio, haki, vikwazo, nafasi, fursa pamoja na huduma mbalimbali zinatambuliwa kwa kutegemea jinsia ya mtu.

Labda nigusie uchambuzi wa kijinsia kwamba unahusisha aina na mbinu mbalimbali zinazotumika katika kufuatilia na kuelewa tofauti za kimaisha kati ya wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, na mahusiano kati yao yanayojumuisha upatikanaji wa fursa na rasilimali, majukumu yao, pamoja na changamoto zinazowakabili. Ikumbukwe kuwa kuna tabia fulani katika jamii, ambazo mara nyingi huonekana kama ni hafifu kwa ama wavulana au wasichana, lakini si kwa kila mmoja.

Kwa maana hiyo elimu ya jinsia ni muhimu na hasa wakiipata mapema wakiwa wadogo. Yaani wazazi wachukue nafasi yao na pia elimu hii iingizwe kwenye mitaala ili watoto wetu wafundishwe shuleni.

Katika dunia ya leo watoto wanajua mambo makubwa mapema sana, hivyo mzazi usipokuwa makini na pia elimu hii isipoingizwa kwenye mitaala tunaweza kukuta wameharibika. Ndani ya jamii yetu wapo wale ambao hawataki kabisa kusikia watoto wakipata elimu ya jinsia.

Wanadai kwamba kufanya hivyo ni sawa na kuwaharibu, lakini niwaambie kuwa kukaa kimya bila kumpa mtoto elimu hii ni hatari kwa maisha yake ya baadaye. Wazazi wana wajibu mkubwa wa kuelimisha watoto wao kutambua jambo hili muhimu.



**BATULI MANGALA (MKAZI WA BAGAMOYO MKOANI PWANI)**

KATIKA jamii yetu kuna aina nyingi za tabia ya udhalilishaji na ni wanawake na watoto ambao mara nyingi ndio waathirika wakubwa. Hii haina maana kwamba wavulana hawawezi kudhalilishwa, lakini kwamba wasichana na wanawake wameelekea kuwa na majukumu hafifu katika jamii, wakati wanaume wamechukua yenye nguvu na madaraka zaidi.

Kwa wenzetu walimu kama wanataka kuchunguza sehemu hii pamoja na wanafunzi wao darasani, wanatakiwa kufanya maandalizi kwa uangalifu sana ili waweze kuwasaidia wanafunzi kwa vile baadhi ya hoja zinaweza kuwafanya wasijisikie vizuri na kuwasuta.

Wanaweza pia kujikuta wanatoa hadharani baadhi ya matukio ya udhalilishaji, ni lazima walimu wajiandae kuwasaidia wanafunzi kwa umakini mkubwa wa namna ya kuzungumza na kwa uchaguzi mkubwa wa maneno ya kusema. Lakini kikubwa zaidi ni kuwapo kwa elimu inayohusu mambo hayo ya mahusiano na jinsia.

Yaani ikiingizwa kwenye mitaala ya shule itapendeza zaidi kwani itasaidia kuwafanya wanafunzi kutambua kwamba udhalilishaji unaweza kuwa wa kiakili, kimwili na kijinsia. Jamii nayo itambue kuwa elimu hiyo pia inatakiwa kutolewa kuanzia nyumbani.

Watoto waipate maeneo yote. Wakiwa nyumbani wanaipata na wakiwa shuleni pia wanaipata na hata wale ambao bado hawajaanza shule, wakilelewa katika maadili wanaweza kuwa watoto wema ambao wataendeleza maadili hayo hata shuleni.

Ni muhimu kutambua kwamba ndani ya jamii kuna baadhi ya watoto ambao wamedhalilishwa na wazazi wao, wanafamilia wengine na wengine wengi. Hii yote inatokana na ukosefu wa elimu ya mahusiano na jinsia.



**DEBORAH MASANGURA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SERIKALI ikichukua hatua ya aina hiyo ya kuingiza elimu ya mahusiano na jinsia itakuwa imefanya jambo la maana, kwani nionavyo ni kwamba elimu hii inatakiwa kutolewa kwa watoto wote wenye umri wa kuanza shule, kwa sababu ndiyo miaka ambayo anaanza kujitambua na kuacha kutembea uchi na hata kutolala kitanda kimoja na mtu ambaye siyo wa jinsi yake.

Bahati mbaya katika jamii yetu kuna hali ya kutofautiana kabisa kijinsia katika upatikanaji wa elimu, fursa za kiuchumi na huduma za afya. Kuna upendeleo wa kutoa elimu kwa wavulana, pamoja na masuala ya mimba za utotoni, matokeo yake ni kiwango kikubwa cha kuachishwa shule kwa wanafunzi wa kike.

Elimu hiyo ikizingatiwa inaweza kusaidia tofauti hata kwenye ajira hapo baadaye. Nifafanue kwamba watu wanazaliwa kama wanawake au wanaume, lakini wanajifunza kuwa wasichana au wavulana, ambao hukua na kuwa wanawake au wanaume.

Wakati mwingine katika makuzi hayo wamekuwa wakifundishwa tabia na mitazamo isiyofaa kuhusu majukumu na shughuli zinazowastahili, na jinsi wasivyotakiwa kuhusiana na watu wengine.

Tabia hii siyo nzuri kwani wote hawa wanatakiwa kujifunza na kuelekezwa kuwa wote ni sawa kwani hali hiyo ndiyo inayojenga utambulisho wa kijinsia na inayoamua kuhusu majukumu ya kijinsia.

Kwa lugha nyingine niseme kuwa sisi wazazi pia tuna jukumu kubwa la kuhakikisha watoto wetu wanapata elimu ya jinsia mapema hasa wanapofikia umri wa kujitambua kuliko kusubiri hadi wakutane na mambo yanayoweza kuwaharibia malengo yao ya baadaye.





## Paroko awafananisha wala rushwa na Pilato

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

PAROKO wa Parokia ya Simike Jimbo Kuu Katoliki la Mbeya, Emmanuel Meza, amewafananisha viongozi wanaopokea rushwa na mfalme Pilato ambaye aliamuru Yesu asulubiwe, huku akijua hakustahili hukumu hiyo.

Meza alitoa kauli hiyo juzi wakati akihubiri kwenye misa ya Dominika ya Matawi iliyofanyika katika Parokia ya Simike, ambapo alisema viongozi wanaopokea ama kutoa rushwa wana tabia ya uoga kama alivyokuwa Mfalme Pilato.

Alisema Pilato aliamuru Yesu asulubiwe msalabani ili kulinda madaraka yake mbele na hivyo hata watoa rushwa wa sasa hasa viongozi wanafanya hivyo ili kulinda madaraka yao.

Paroko Meza alisema katika miaka ya sasa wapo viongozi ambao wanafanana na mfalme huyo ambapo wamekuwa wakitumia gharama kubwa kulinda madaraka yao na hata wakati mwingine hujihusisha na vitendo vya rushwa.

Alisema mwenendo wa viongozi hao ambao umejikita kulinda maslahi yao umekuwa ukipelekea wananchi kukosa haki zao za Msingi kutoka kwao kwa kuwa wamekuwa hawawajibiki ipasavyo katika kutoa haki na kuzingatia misingi ya kazi zao.

Aidha, alisema hata Mfalme Pilato ambaye alikuwa amepewa dhamana ya kuongoza kwa wakati huo alikuwa anafahamu kuwa hatendi haki kutokana na hukumu aliyotoa kwa Yesu, lakini alilazimika kufanya hivyo kwa ajili ya kuweka heshima kwenye nafasi yake.

"Tunaona jinsi huyu Pilato alivyojaa na woga na ndio maana aliamuru Yesu asulubiwe kwa sababu ya shinikizo la watu waliokuwa wamekusanyika, alijua kabisa kwamba hatendi haki, lakini alifanya hivyo ili kuwaridhisha," alisema Meza.

Aliwakumbusha watumishi kufanya kazi zao kwa kuzingatia misingi ya taaluma zao walizosomea kwa kuhakikisha wanawajibika ipasavyo ikiwa ni pamoja na kutoa haki kwa wananchi na kwamba huo ndio msingi mkubwa wa uwajibikaji.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema wananchi hususani wanyonge wamekuwa wakikosa haki zao za msingi na wakati mwingine hulazimika kuzinunua kwa sababu tu waliopewa dhamana wamekuwa wanaangalia maslahi yao na kuwasahau wananchi.

Aliwataka Watanzania kila mmoja kwa nafasi yake kutafakari kama kazi anayofanya ni halali na haina viashiria vya rushwa ili kuhakikisha taifa linaenda vizuri.

**"Tunaona jinsi huyu Pilato alivyojaa na woga na ndio maana aliamuru Yesu asulubiwe kwa sababu ya shinikizo la watu waliokuwa wamekusanyika, alijua kabisa kwamba hatendi...**

# Wanawake washauriwa kuchangamkia mikopo

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WANAWAKE mkoani Mbeya wameshauriwa kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali, ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ikiwamo mikopo ya halmashauri inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani yanayotengwa kwa ajili ya kundi hilo.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Biashara wa Wilaya ya Mbeya, Elizabeth Iyombe, alipokuwa anafunga mafunzo ya miezi mitatu ya ujasiriamali kwa zaidi ya wanawake wajasiriamali 100 wa Jiji la Mbeya ambao wanazalisha bidhaa mbalimbali.

Mafunzo hayo yalikuwa yanatolewa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Mandela Washington Fellowship (MWF) kwa kushirikiana na ubalozi wa Marekani nchini, ambapo yalilenga kuwawezesha wanawake hao kuwa na uelewa juu ya njia za kufanya biashara zao kuwa endelevu.

Iyombe alisema kwa sasa kuna fursa nyingi za wanawake wajasiriamali hasa ambao tayari wamejiunga kwenye vikundi kwa madai kuwa kwa sasa kila anayetaka kuwasaidia anataka wawe kwenye vikundi. Alisema pamoja na kwamba serikali imetenga asilimia nne ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya wanawake, lakini mwamko wa kundi hilo kujitokeza kukopa fedha hizo ni mdogo kutokana na kutojiunga na vikundi.

"Hongereni kwenu mliopata fursa ya kushiriki mafunzo haya naamini mtakuwa mabalozi wazuri wa kuhamasisha wenzenu kujiunga kwenye vikundi, halmashauri zetu zinatenga fedha kwa ajili yenu, lakini pia wapo wadau wanaojitolea kuwezesha vikundi," alisema Iyombe.

Pia aliwataka kutumia vizuri elimu waliyoipata ili kuinua kipato cha familia zao na kuwa na uwezo wa kujitegemea katika maisha yao huku biashara zao zikiendelea kustawi. Mratibu wa Mradi huo, Margret Simalenga, alisema mradi huo ulikuwa unawalenga zaidi wanawake ambao tayari wana biashara zao na kwamba yalilenga kuwapa mbinu za matumizi sahihi ya fedha za miradi yao.

Alisema miongoni mwa vitu ambavyo wajasiriamali hao wamefundishwa kwa siku hizo ilikuwa ni kuwa na madaftari ya kuandika vitu wanavyonunua na lingine kwa ajili ya kuandika vitu wanavyouza ili iwe rahisi kujua faida ya biashara zao.

Alisema walibaini kuwa baadhi ya wanawake wanaanzisha biashara ambazo zinakuwa sio endelevu kwa sababu wanashindwa kutofautisha fedha za biashara na fedha za matumizi ya nyumbani.

"Tilibaini kuwa baadhi ya biashara za wanawake zinakufa kwa sababu hawana tabia ya kuandika mapato na matumizi na hivyo wanajikuta wanachukua fedha za biashara wanazitumia kwenye matumizi mengine ya nyumbani na hivyo kuingia hasara," alisema Simalenga.

Baadhi ya wajasiriamali waliohudhuria mafunzo hayo walisema yatawasaidia kubadili mwelekeo wa biashara zao kwa madai kuwa mafunzo hayo yamewasaidia kuwa na mtazamo tofauti.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Amina Mwambopo ambaye ni mfanyabiashara wa nguo za mitumba katika Soko la Sokomatola jijini Mbeya, alisema mara nyingi wanawake wanashindwa kuendelea kwa sababu wanakuwa na tamaa ya kununua kila kitu. Alisema wakati mwingine wanajikuta wanatumia fedha za biashara kwenye matumizi mengine ikiwamo kununua nguo na vyakula.

Vilevile wajasiriamali hao walishauriwa kurasimisha biashara zao kwa kuwa na leseni za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kwa wale ambao mitaji yao bado midogo wanatakiwa wawe na vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na Rais.



Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa wa Tigo Pesa, James Sumari (katikati), akiwapongeza kwa kuwanyanyua mikono juu washindi wa Promosheni ya Mawakala wa Tigo Pesa, iliyokuwa inajulikana kama 'Cash In Promotion'. Kulia ni Mojelwa Mlinga kutoka Dar es Salaam na Said Khatibu kutoka Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana watakiwa kuepuka kushawishiwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

VIJANA nchini wameshauriwa kupima kila aina ya ushawishi wanaopewa ili wasitumike kuvuruga amani ya taifa na badala yake wanapaswa kuwa walinzi imara wa amani itakayochochea maendeleo ya taifa.

Ushauri huo ulitolea juzi na Askofu wa Kanisa la Anglican Jimbo la Mbeya, Julius Lugendo, wakati wa tamasha la uzinduzi wa kampeni ya kusambaza amani nchini lililofanyika jijini Mbeya ambapo alisema amani ndio msingi wa maendeleo.

Tamasha hilo liliwahusisha viongozi mbalimbali wa dini, viongozi wa mila na wa vyama mbalimbali vya siasa ambapo walitakiwa kuachana na tofauti ya itikadi zao za kisiasa na kueneza amani.

Askofu Lugendo aliwataka vijana kupima matokeo yanayoweza kutokea kabla ya kuanza kutekeleza ushauri wanaopewa na mtu au kikundi chochote cha watu, huku akisisitiza kuwa wanatakiwa wawe chachu ya kueneza amani nchini.

Alisema taifa likiendelea kuwa na amani kuna uwezekano mkubwa wawekezaji kushawishika kuwekeza nchini na hivyo kusaidia vijana kupata ajira ambazo zitawapatia kipato na kuliongezea taifa kipato.

"Vijana wetu hasa wa Mbeya, ukikuta ushawishi unaopewa ni wa kuvuruga amani ya mkoa wetu, nchi ama mahali ulipo basi mwambie anayekushawishi kuwa ushawishi wake hauna faida kwako na achana naye," alisema Askofu Lugendo.

Mwandaaji wa tamasha hilo la kusambaza amani nchini ambaye pia ni mmiliki wa Shule za Patrick Mission za jijini Dar es Salaam na mdau wa maendeleo mkoani mbeya, Ndele Mwanselela alisema amani iliyopo nchini inatokana na maono ya viongozi wa taifa hili tangu awamu ya kwanza. Aliwataka Watanzania kuwaenzi, kuwatii na kuheshimu viongozi na serikali iliyopo madarakani ambayo inaendelea kufanya kazi ya kuleta maendeleo pamoja na kuendeleza amani ya taifa iliyoasisiwa na watangulizi wake.

Mwaselela alisema bila kuwa na viongozi imara na wenye maono mazuri amani ya nchi haitakuwapo na hivyo akasisitiza viongozi wote bila kujali itikadi zao za kisiasa, tofauti za dini zao wala jinsia washiriki kueneza amani ya taifa.

"Kwa sasa tunafurahia maendeleo yanayoletwa na viongozi wetu, lakini tujuwe kuwa wanafanya hivyo kwa sababu ya amani, endapo amani isingekuwapo hata haya maendeleo tusingeyapata hata kidogo, angalieni mataifa yenye migogoro yalivyo," alisema Mwaselela.





# Wenye ulemavu waomba mawasiliano ya alama

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

KATIBU wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Dodoma (CHAVITA), Amina Issa, amesema kukosekana kwa mawasiliano ya lugha ya alama kati ya watoa huduma katika sekta mbalimbali na watu wenye ulemavu wa kutosikia kunawafanya wakose haki zao za msingi.

Issa alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na umuhimu wa mawasiliano ya lugha za alama kwa watumishi kwenye maeneo wanayotoa huduma za kijamii ikiwamo kwenye benki, taasisi za kifedha, hospitali, mahakamani, polisi na ofisi za kiserikali.

Akizungumza jijini hapa alisema changamoto hiyo ya kukosekana kwa lugha hiyo ya alama, kwa upande wao inawafanya kuendelea kukosa mahitaji yao muhimu kwenye sekta hizo kama wanavyopatiwa watu wengine wasiokuwa na ulemavu.

Alisema kuwa kwenye taasisi hizo wanashindwa kupata haki zao za msingi kutokana na watoa huduma hizo kukosa elimu ya lugha hiyo ya alama, hivyo ni wakati sasa kwa serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kuwaelimisha watumishi hao.

"Tunaiomba serikali kutenga bajeti kwa ajili ya watumishi wao ili waweze kujifunza lugha ya alama, ambayo itakayowawezesha kuwa na mawasiliano na sisi pindi tunapohitaji kupatiwa mahitaji mbalimbali kwenye taasisi husika zikiwamo za kibenki, hospitali, mahakamani, polisi na katika majengo ya serikalini," alisema.

Katibu huyo alisema kuwa pamoja na changamoto hiyo pia kwa upande wao wanakabiliwa na tatizo la kutopatiwa taarifa kwa wakati zinazohusu ushiriki wa kwenye jamii, suala ambalo limekuwa likisababisha kukosa haki zao za kimsingi.

Aidha, amewataka vijana wa chama hicho cha viziwi Mkoa wa Dodoma kuunda vikundi ili waweze kukopeshwa na taasisi za kifedha zitakazowawezesha kujiinua kimapato zaidi badala ya kutegemea ufadhili ambao hauna uhakika kwa asilimia kubwa.

Aliongeza kuwa wakiungana kwa pamoja itakuwa rahisi kwa upande wao kuibua miradi ambayo itakayoweza kuondokana na dhana ya utegemezi kwa watu na wafadhili, ambapo kwa asilimia nyingi umekuwa ukitufanya kuwa masikini kila wakati.

Alisema kuwa hivi sasa serikali imetoa fursa nyingi za kujiajiri wenyewe ikiwamo na vitambulisho ambavyo vitakavyotufanya kufanya shughuli mbalimbali za kujipatia kipato bila kubuguziwa pale tutakapokuwa na vikundi hivyo vya ujasiriamali.

# Askofu atoa angalizo utoaji elimu bora

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

ASKOFU wa Kanisa la Wadventista Wasabato Jimbo Kuu la Kusini mwa Tanzania, Mark Malekana, ameyataka mashirika ya dini, watu binafsi pamoja na taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikianzisha shule kuzingatia ubora ili kuweza kuinua elimu nchini.

Aliyasema hayo juzi, wakati wa uzinduzi wa shule binafsi ya awali na msingi ya Ellen White iliyopo Nzuguni nje kidogo ya Jiji la Dodoma.

Alisema watu ambao wamekuwa wakianzisha huduma za shule nchini wanatakiwa kuzingatia ubora ili kuweza kukuza viwango vya elimu nchini.

Aidha, alisema watu wengi ambao wanaanzisha utoaji wa elimu katika taasisi za dini, watu binafsi pamoja na taasisi binafsi wanatakiwa kubadilika katika mitazamo yao ili wanapotoa huduma hiyo iwe katika ubora wa hali ya juu.

"Nitoe wito kwa wote wanaotaka kuanzisha shule kuacha kufanya vitu vya ovyo ovyo eti tu kwasababu ni mashirika ya dini, lazima tuzingatie ubora katika uanzishwaji wa shule zetu ili elimu inayotolewa iwe bora, hivi sasa Watanzania siyo watu wa vitu vya ovyo ovyo tena," alisema Askofu Malekana.

Aidh, alimpongeza mkurugenzi wa shule hiyo kwa kuunga juhudi za serikali katika kuboresha elimu na kupambana na adui ujinga ikiwa ni sehemu ya wale maadui watatu.

"Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alitueleza kuwa maadui wa taifa letu ni watatu ambao ni umaskini, ujinga na maradhi, lakini adui ambaye ni mama yao ni ujinga kama tukipata elimu bora basi haya yote ikiwamo umaskini hatutakuwa nao tena," alisema.

Alisema kutokana na rasilimali zilizopo nchini Tanzania haikutakiwa kuwa maskini kama ilivyo, lakini sababu kubwa iliochangia ni ukosefu wa elimu iliyo bora kwa Watanzania.

"Kama tutakuwa na elimu iliyobora basi rasilimali tulizonazo tungeweza kuzitumia ipasavyo ili kuweza kuondokana na umaskini tulionao hivi sasa," alisema.

Naye Meneja wa shule hiyo, Phien Maiko, alisema kuwa lengo la shule hiyo ni kuleta ushindani katika ngazi ya mkoa na hadi kitaifa katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

"Tumeanzisha shule hii kutokana na mahitaji makubwa yalipo hivi sasa katika Jiji la Dodoma kufuatia kuongezeka kwa watu baada ya serikali kuhamia hapa Dodoma," alisema Maiko.



Askofu Mkuu wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, Jimbo Kuu la Kusini mwa Tanzania, Mch. Mark Malekana (kushoto), akikata utepe kuzindua Shule ya Awali na Msingi ya Ellen White, iliyopo Nzunguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Rais Magufuli amwagiwa sifa kufungua mji

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MBUNGE wa Vijana, Mariam Ditopile, ameibuka na kumpongeza Rais Magufuli kutokana na kufungua ujenzi wa mji wa kiserikali ambao umesaidia kutoa ajira kwa vijana.

Pongezi hizo zimetolewa na mbunge huyo katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika mji wa Kibaigwa wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

Mariam alisema vijana wana kila sababu ya kumpongeza Rais kutokana na kufungua mji huo, pili kuwapatia vijana wote ajira watakaoshiriki katika kazi hiyo ya ujenzi.

Alisema vijana wanatakiwa kuishukuru serikali ya awamu ya tano kwa sababu imefanya mambo makubwa.

Alifafanua kuwa Rais Magufuli amefanya mambo makubwa ambayo serikali nyingine zilizopita hazikuweza kuyatenda.

"Wana Dodoma tunampongeza Magufuli, kwa stahili hii lazima tumpigie kura," alisema Mariam. Alisema yeye mbunge wa vijana Tanzania basi atawashawishi vijana wenziwe kuhakikisha wanaiga maendeleo yanayofanywa na Rais Magufuli.

Aliongeza kuwa hivi sasa wanajivunia kile kilichofanywa na Rais Magufuli na kuwataka vijana kutobweteka na badala yake wajipange kuonyesha uwezo wao.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Billy Chidabwa, alisema vijana wote wapo imara mkoani hapa na wanaikubali serikali ya awamu ya tano kutokana na utendaji wake.

Chibwada alisema lengo lao ni kuona maendeleo katika Mkoa wa Dodoma yanafanywa kupitia vijana ambao wako tayari kutoa ushirikiano kwa serikali ya awamu ya tano. Alisema vijana ni nguvu kazi kwa hiyo wajenge ushirikiano ili CCM ibaki kuwa juu katika Mkoa wa Dodoma.

Aliongeza kuwa lengo lao ni kuona wanatekeleza Ilani ya CCM kwa utendaji wa kazi wanazonya kwa ajili ya kuinua maendeleo ya Mkoa wa Dodoma.



# ADC sasa yajiweka kando vurugu, kuheshimu sheria

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), Hamad Rashid Muhammed, amesema ADC ni chama kisichopenda shari, ugomvi wala vurugu na kitahakikisha kinalinda na kuheshimu sheria za nchi.

Akifungua mkutano mkuu wa chama hicho huko Bweni nje kidogo ya mji wa Zanzibar, mwenyekiti huyo alisema kwa kuwa kipindi cha uchaguzi mkuu kimekaribia ni busara serikali kuruhusu kufanyike kwa shughuli za kisiasa kama mikutano ya hadhara, makongamano na uhamasishaji wa vyama.

Alisema serikali kuzuia shughuli za kisiasa kama mikutano ya hadhara ni kikwazo kwa demokrasia kwa kuwa ni haki ya kikatiba hivyo ni vyema jambo hilo likaangaliwa upya.

"Chama kinachoruhusiwa kufanya mikutano ya kisiasa ni kile chenye wabunge na madiwani kwa tafsiri nyepesi ni kwamba ADC imenyimwa haki ya kufanya mkutano wa hadhara, eneo hili halijakaa sawa," alisema Hamad.

Alieleza kuwa serikali lazima itafute namna ya kudhibiti wanasiasa wakorofi, lakini si sawa kudhibiti vyama vya siasa kutofanya shughuli za kisiasa.

Akizungumzia hali ya chakula nchini, mwenyekiti huyo alisema utafiti walioufanya wamebaini kuwa hali ya chakula sio nzuri sana kwa mwaka ujao, hivyo aliiomba serikali isiuze chakula katika ghala la taifa ili kuwa na chakula cha akiba.

Alisema kutokana na mvua kuchelewa kunyesha katika maeneo mengi na pale inaponyesha huwa ni kubwa kuna weza kukaharibu mashamba.

Aidha, mwenyekiti huyo aliwataka wananchi kutumia chakula kwa tahadhari kubwa ili wasikubwe na njaa kwa mwaka huu kwa kuwa hali haijatulia kama miaka yote iliyopita.

Alieleza kuwa bado kilimo Zanzibar hakijatumika vizuri katika kuinua maisha ya Mtanzania kutokana na serikali kutoonyesha nia na mpango madhubuti wa kumuinua mwananchi kupitia sekta ya kilimo na kukifanya kilimo kama kazi ya mateso na kusababisha vijana kukikimbia.

"Tunaishukuru serikali ya awamu ya tano itilie mkazo suala la kilimo, ili kukuza uchumi wetu hasa katika harakati za kuelekea katika uchumi wa kati na viwanda," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Queen Cuthbert Sendiga alisema licha ya ADC kuwa na lengo la kuwapo madarakani katika Uchaguzi Mkuu wa 2020, lakini watahakikisha wanawake wanashiriki ipasavyo katika kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi huo.

Alieleza anajiandaa kugombea nafasi ya urais kupitia chama hicho ili kuweza kuwapa fursa wanawake waweze kufikia malengo yao ya kujikwamua na umaskini.

Chama hicho kimefanya uchaguzi wa viongozi ambapo kimemchagua tena Hamad Rashid Muhammed kuwa mwenyekiti wa chama hicho.

## Baraza la Maulamaa lapewa kibarua kutoa elimu

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

MUFTI Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, amelitaka Baraza la Maulamaa kuwaelimisha waumini wa dini ya kiislamu kuvumiliana katika tofauti zao na kuipatia ufumbuzi migogoro ya kidini ili amani na utulivu iendelee kutawala nchini.

Aliyasema hayo katika kikao cha tatu cha baraza la tano la Maulamaa Zanzibar.

Aliwataka Maulamaa hao kuwa na hofu ya Mungu kwa vile wanabeba dhima ya wanaowaongoza. "Macho na imani za waumini wa dini ya kiislamu yanawatazameni nyie, hivyo msiridhike na elimu mliyonayo na ndio maana tunaambiwa tutafute elimu ili mtakapotowa hukumu ziwe zinazoendana na misingi ya dini yetu," alisema.

Aidha, aliwataka Maulamaa hao kuhakikisha maeneo wanayoyasimamia yako salama ikiwamo kuwaelewesha maimamu namna ya kuepuka mizozo inayojitokeza ndani ya nyumba za ibada. "Pia ni lazima kuwatahadharisha wageni wanaokuja kwa ajili ya kuja kutoa elimu ya dini (daawa), kufuata sheria za nchi na sio kufarakanisha waumini kutokana na madhehebu," alisema.

Alieleza kuwa hivi karibuni kumezuka tabia kwa baadhi ya kikundi cha watu kukashifu viongozi wa dini, masheikh na maulamaa, ambapo wengine wanaokashifiwa wameshafariki dunia jambo ambalo si la kupendeza. Baraza la Maulamaa kwa kauli moja limewaagiza walimu wa madrasa zote Zanzibar kutowapeleka katika sherehe na shughuli za Maulid watoto walio chini ya umri wa miaka 18 wakati wa usiku.



Mkuu wa Bidhaa wa Vodacom, Linda Riwa (wapili kulia) na Devota Kijogoo (kulia), wakifurahia uzinduzi wa duka la Vodacom Masaki, jana. Kampuni hiyo inaendelea kutanua upatikanaji wa huduma zake ili kuhakikisha wateja wake wanapata huduma bora. **PICHA: VODACOM**

# Watakiwa kuongeza ushirikiano kutimiza wajibu

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WANACHAMA wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa Zanzibar (J-SMZ) wametakiwa kuongeza ushirikiano ili kutimiza wajibu wao na kuongeza kasi ya maendeleo ya jamii.

Wito huo umetolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib, Ayoub Mohammed Mahmoud, alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa tatu wa jumuiya hiyo inayoundwa na Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji na Manispaa za Zanzibar uliofanyika katika ukumbi wa manispaa ya Magharibi 'B', Unguja.

Alisema iwapo watazingatia lengo la kuanzishwa kwa jumuiya hiyo kuna nafasi kubwa ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao na kukabiliana kikamilifu na changamoto zinazowakabili.

Aliwaomba wajumbe wa mkutano huo ambao ni wakurugenzi, wenyeviti na mameya kuwa Zanzibar ina nafasi kubwa ya kuchochea kasi ya maendeleo ya jamii kupitia jumuiya hiyo kwa kuwa ni daraja litakalounganisha serikali kuu na serikali za mitaa nje ya mfumo wa kawaida wa kiserikali.

"Iwapo mtakipa umuhimu chombo hiki kwa kuwajibika kikamilifu kama katiba yenu inavyoelekeza, kitasaidia kupatikana kwa fursa mbalimbali za kustawisha maendeleo ya maeneo yenu na jamii kwa ujumla," alisema Ayoub.

Alisema Serikali ya Zanzibar itaendelea kuzipa umuhimu asasi zisizo za kiserikali (NGO), kwa kuwa zina mchango mkubwa katika maendeleo na kutatua changamoto zinazojitokeza katika jamii.

Aidha, aliwataka watendaji wa jumuiya hiyo kuandaa ratiba ya utekelezaji wa majukumu yao kwa lengo la kuwawezesha wanachama kutekeleza wajibu wao kikamilifu likiwamo suala la kulipa ada kwa wakati.

"Mkizingatia wajibu huu (wa kulipa ada ya uanachama) mtaweza kukutana kwa wakati na kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili jumuiya, lakini pia taasisi zenu pamoja na kufungua fursa za maendeleo na kujiendeleza," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Khatib Abrahman Khatib, alieleza kwamba kuanzishwa kwa jumuiya hiyo kunaenda sambamba na dhana ya ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda serikali za mitaa na kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili katika maeneo yao ya kazi.

Abrahman ambaye pia ni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Mjini, alimuomba Mkuu wa Mkoa kuisaidia jumuiya hiyo kupata utambulisho katika ngazi ya serikali kuu ili iweze kuanzisha miradi ya pamoja baina ya halmashauri au manispaa moja na nyingine.

"Tukiweza kufanya hivyo kutasaidia kuimarisha nguvu za serikali za mitaa sambamba na kuwa na uwezo wa kujiunga na taasisi nyengine za kitaifa na kimataifa ambapo kuna fursa nyingi za maendeleo," alieleza Khatib.

Kwa upande wake mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa mradi wa Engine kutoka makao makuu Dar es Salam, William Mjema, alieleza kuwa shirika hilo litaendelea kushirikiana na serikali za mitaa ili kufikisha maendeleo kwa jamii.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 15 April**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 16 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 17 April**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 18 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 19 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 20 April**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 21 April**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima — WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 15 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 16 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 17 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 18 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 19 April**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 20 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 21 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## RADIO One — WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11.00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |


EATV

NIRVANA

LEO USIKU SAA 3:00

JUMANNE
11:00 DADAZ (live)
13:30 Kali Za Wana
14:00 Dakika10 Za Maangamzi
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Nirvana
21:30 Wakilisha
22:00 Grace Na Asili Yangu
22:30 Bongo Hits



*NIRVANA ni kipindi cha kisasa kinachoongelea mitindo, sanaa, urembo na staili za maisha. NIRVANA inawalenga wale wanao ongoza kuonyesha mitindo mipya kwenye jamii na wale wanaofuatilia*

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## HABARI KIMATAIFA

## Vikosi vyawasaka madaktari waliotekwa

**NAIROBI,** Kenya

HATIMA ya madaktari wawili, raia wa Cuba bado haijajulikana baada ya kutekwa nyara na watu wanaodaiwa kuwa magaidi wa kundi la wanamgambo wa Kiilsamu la Al Shabab, Kaskazini Mashariki mwa Kenya.

Vikosi vya polisi na jeshi vinaendelea na operesheni ya kuwatafuta madaktari hao. Kwa mujibu wa vyanzo kadhaa kutoka Jeshi la Polisi Kenya, huenda madaktari hao wamevushwa hadi nchi jirani ya Somalia.

Madaktari hao ni miongoni mwa kundi la madaktari zaidi ya 100 kutoka Cuba waliowasili nchini Kenya kwa ombi la serikali, kufanya, kazi kuziba pengo la uhaba wa madaktari nchini humo.

Msemaji wa Jeshi la Polisi la Kenya, Charles Owino amebaini kwamba mlinzi wa madaktari hao aliuawa na watekaji nyara, ambao walitoroka na gari na kuingia nchini Somalia.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Owino akihojiwa na vyombo vya habari alieleza kuwa gari lililokuwa likitumiwa na madakatari hao limepatikana na dereva wake anahojiwa na polisi.

Madaktari hao walitekwa nyara siku ya Ijumaa, Kaskazini Mashariki mwa Kenya, katika Kaunti ya Mandera, karibu na mpaka wa Somalia. **RFI**

## Wafanyakazi Msalaba Mwekundu watafutwa

**DAMESKI,** Syria

SHIRIKA la Msalaba Mwekundu limesema linafuatilia taarifa za wafanyakazi wake watatu ambao walitekwa na kundi la Islamic State IS Nchini Syria miaka mitano iliyopita.

Wafanyakazi wa shirika hilo waliotekwa ni Louisa Akavi, Alaa Rajab na Nabil Bakdounes ambao walitekwa Oktoba 2013 walipokuwa wakisafiri jimbo la Idlib kaskazini mwa Syria.

Taarifa za kuaminika zinaeleza kwamba Louisa Akavi alikuwa hai hadi mwaka 2018 akiwa mikononi mwa kundi hilo la IS, huku Alaa Rajab na Nabil Bakdounes ikiwa haijulikani kama wapo hai ama la.

Akavi, ambaye ni Rais wa New Zealand, mwenye umri wa miaka 62 ni muuguzi ambaye alifanya kazi kwa miaka 17 katika maeneo ya kutoa misaada.

Alaa Rajab na Nabil Bakdounes, wote wawili ni raia wa Syria waliokuwa madereva na waliofanya kazi ya kutoa misaada ya kibinadamu nchini humo. New Zealand imesema kuwa kikosi maalumu cha jeshi kimekuwa kikijaribu kutafiti ili kujua ni wapi alipo Akavi.

Hata hivyo, wasiwasi umezidi kuongezeka iwapo Akavi atapatikana kufuatia kusambaratika kwa ngome ya mwisho ya wapiganaji wa IS mwezi uliopita karibu na mpaka wa Iraq. **BBC**

# Maofisa wa zamani Sudan matatani

**KHARTOUM,** Sudan

**Baraza la Kijeshi pia lilitangaza baadhi ya maamuzi yakiwamo, Vingozi wapya wa jeshi na polisi, Mkuu mpya wa Kitengo cha ujasusi, Kamati za kupambana na rushwa na kuchunguza chama tawala kilichoondoka.**

BARAZA la mpito la kijeshi nchini Sudan limewakamata waliokuwa maofisa wa serikali na kuahidi kutowatawanya waandamanaji.

Maandamano ya miezi kadhaa nchini Sudan yalisababisha kujiuzulu kwa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Omar Al-Bashir ambaye alitawala kwa muda mrefu.

Lakini licha ya kujiuzulu wa Rais Bashiri, raia bado wanaendelea kuandamana na wamepiga kambi nje ya makao makuu ya wizara ya ulinzi katika mji mkuu Khartoum.

Katika mkutano na waandishi habari siku ya Jumapili, Msemaji wa Jeshi Meja Jenerali Shams Ad-din Shanto alieleza kuwa baraza la kijeshi lipo tayari kuidhinisha serikali yoyote ya kiraia itakayoidhinishwa na vyama vya upinzani.

"Hatutomteua Waziri Mkuu. Watamchagua," alisema Meja Jenerali Shams akimaanisha upinzani na makundi yanayoandamana.

Alieleza pia jeshi halitowaondoa waandamanaji kwa lazima lakini alitoa wito kwa waandamanaji hao kuruhusu maisha yaendelee kama kawaida na waache kuweka vizuizi kinyume cha sheria, na kwamba kushika silaha hakutoruhusiwa.

Baraza la Kijeshi pia lilitangaza baadhi ya maamuzi yakiwamo, Vingozi wapya wa jeshi na polisi, Mkuu mpya wa Kitengo cha ujasusi, Kamati za kupambana na rushwa na kuchunguza chama tawala kilichoondoka.

Pia kuondolewa kwa sheria kali za kuzibana vyombo vya habari, kuachiwa kwa maafisa wa polisi na jeshi waliozuiwa kwa kuunga mkono waandamanaji.

Ukaguzi wa wajumbe wa kidiplomasia na hatua ya kutimuliwa kwa balozi wa Sudan nchini Marekani na Uswis.

Maandamano ya kupinga kupanda gharama ya maisha yalianza Desemba mwaka jana, lakini punde tu yakageuka kuwa wito mkubwa wa kumpinga Rais Bashir na utawala wake.

Jeshi nchini humo lilimng'oa na kumzuia kiongozi huyo wa muda mrefu Sudan baada ya kuhudumu kwa miaka 30 madarakani.

Aliyeongoza mapinduzi hayo, Waziri wa Ulinzi, Awad Ibn Auf, alitangaza kwamba jeshi litasimamia serikali ya mpito kwa kipindi cha miaka miwili kitakachofuatwa kwa uchaguzi na akaidhinisha miezi mitatu ya hali ya dharura.

Lakini wandamanji waliapa kusalia mitaani hata baada ya hatua hiyo, wakitaka maguezi na kuidhinishwa kwa serikali ya kiraia mara moja.

Ibn Auf himself alijiuzuliu ziku ya pili baada ya jeshi kutoa tamko kama alivyojiuzulu Mkuu wa Usalama anayeogopwa na wengi Jenerali Salah Gosh.

Luteni Jenerali Abdel Fattah Abdelrahman Burhan baada ya hapo alitajwa kuwa kiongozi wa baraza la mpito la kijeshi. **BBC**



Waandamanaji nchini Sudan wakipaza sauti mbele ya vikosi vya ulinzi wakati maandamano yakiendelea mjini Khartoum, Sudan. **PICHA: REUTERS**

## Marekani yashinikiza Maduro aachie ngazi

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo yuko katika ziara ya siku nne katika mataifa washirika wa Marekani katika Amerika ya kusini ambapo ujumbe wake zaidi umelenga mgogoro wa Venezuela.

Pompeo alimuita Maduro dikteta ambaye amesababisha kuharibika kwa Venezuela na kuwaathiri vibaya raia wake.

Katika kikao na Rais wa Paraguay, Mario Abdo Benkitez katika Mji Mkuu wa Asuncion ambapo walizungumzia suala la uchumi na mgogoro wa kisiasa nchini Venuzuela, uimarishaji wa demokrasia na namna ya kukabiliana na uhalifu nchini humo, Pompeo alimlaumu Maduro kwa kuharibika kwa taifa hilo.

Alisema Marekani itashirikiana na Paraguay na mataifa mengine kuhakikisha ustawi na demokrasia inarudishwa Venezuela.

Pompeo alimtaka Maduro kubadilisha mbinu zake na kuliachia taifa hilo pamoja na kumtaka kufungua madaraja na mipaka mara moja kama njia ya kuwajali raia wake wanaokumbwa na hali mbaya.

"Kuna mpango wa uchaguzi wa haki na uwazi ndani ya Venezuela na mpango wa kurudisha ukuaji wa biashara na hali ya kawaida ya maisha na nafasi za kiuchumi kwa ustawi wa Venezuela na kabla haya kufanyika ni lazima uongozi mbaya wa Maduro ukomeshwe," alisema Pompeo na kuongeza:

"Marekani itaendelea kutumia kila njia ya kisiasa na kiuchumi kuwasaidia watu wa Venezuela, kwa kutumia vikwazo vya kiuchumi na kufutilia mbali vibali vya kusafiri" alisema Pompeo.

Waziri huyo wa Mambo ya Nje wa Marekani alisema Paraguay ni mojawapo ya nchi 12 zilizounda kundi la Lima la kuhakikisha amani inarudi nchini Venezuela.

Alisema Marekani inamtambua rais wa nchi hiyo na viongozi wengine wa Lima katika kuipigania demokrasia kwa Rais Maduro kuondoka Madarakani.

Pompeo aliweka bayana kwamba Paraguay ni mshirika wa Marekani katika jitihada za kumtoa Maduro na kumuweka madarakani kiongozi wa upinzani, Juan Guido ambaye alijitangaza mwenyewe kuwa rais wa mpito na kuungwa mkono na mataifa mbali mbali. **DW**

# Wanafunzi wenye ulemavu wawezeshwa kwa gari

**Na George Tarimo,** IRINGA

SHULE ya Msingi Kipera ambayo ni maalumu kwa watoto wenye ulemavu katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, imekabidhiwa gari kwa ufadhili wa Shirika lisilo la kiserikali la Ibo kutoka nchini Italia kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Akikabidhi msaada huo mwakilishi wa Shirika la Ibo katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Paola Ghezzi, alisema pamoja na msaada huo wa gari, shirika hilo pia limetoa mafunzo kwa walimu 60 na kujenga njia wezeshi kwaajili ya wanafunzi kuingia na baiskeli zao darasani kwa lengo la kuhudhuria masomo.

Ghezzi alisema kuwa kuna shule nyingi hazina mazingira rafiki kwa ajili ya watoto wenye ulemavu na wanaendelea na ujenzi wa njia hizo maalumu, kutoa baiskeli za walemavu.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Steven Mhapa, aliahidi kuhakikisha gari hilo linatumika kwa ajili ya kazi iliyokusudiwa katika shule hiyo yenye jumla ya wanafunzi 100.

Ofisa Elimu, elimu maalumu katika halmashauri hiyo Wesket Mlagulwa, alisema katika kuhakikisha wanafunzi wa shule hiyo wanakuwa na mazingira bora ya kujifunzia serikali imetoa zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya huduma mbalimbali ikiwamo ujenzi wa mabweni, bwalo la chakula na matundu ya vyoo.

Mlagulwa alisema kuwa awali walikuwa na shida ya mabweni, lakini kwa bahati nzuri serikali imetoa Sh. milioni 221 kwa ajili ya ujenzi wa bwalo, bweni, madarasa mawili pamoja na matundu sita ya vyoo, lakini Ibo wamejenga jiko la kisasa.



Meneja Huduma za Jamii wa NBC, Irene Peter (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa Chuo cha Uhifadhi Wanyamapori (MWEKA), wanaosoma kwa ufadhili wa benki hiyo, wakati wa mafunzo ya kuwaandaa kufaulu masomo na ujuzi mwingine wa kimaisha yaliyofanyika mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Vifaa vya kubaini mionzi mizigo ya vyakula Namanga

**Na Novatus Makunga,** NAMANGA

TUME ya Nguvu za Atomiki nchini, imefunga vifaa vya kisasa vya maabara vinavyoweza kupima na kubaini mionzi katika mizigo ya vyakula inayoingizwa au kutoka nchini katika mpaka wa Tanzania na Kenya katika Kituo cha Forodha cha Pamoja cha Namanga, (OSBP).

Akizungumza na waandishi wa habari mpakani hapo, Ofisa Mfawidhi wa Tume ya Atomiki nchini katika Kituo cha Forodha Namanga, Fadhiri Msumari, alisema upimaji huo licha ya kudhibiti afya ya walaji, lakini pia unawasaidia wafanyabiashara katika uhakika wa soko.

Akifafanua Msumari, alisema, katika kuuza vyakula vya binadamu na mifugo katika nchi mbalimbali duniani moja ya vigezo vinavyotakiwa ni uthibitisho wa kutokuwa na mionzi hatari.

"Sisi hapa Namanga tunapima kila mzigo wa chakula unaosafirishwa kwenda nje ama kuingizwa nchini na kutoa vyeti maalumu vya uthibitisho wa usalama wa mzigo husika na hivyo kusaidia katika uhakika wa soko," alifafanua.

Alisema mbali na vyakula pia hupima mizigo yote inayopita Namanga ambapo kwa siku ushughulikia wastani wa magari 1,200.

Alisema kufuatia kuanzishwa kwa OSBP, Oktoba 2017, maabara hiyo pia imekuwa ikiinufaisha nchi ya Kenya ambayo haina taasisi inayohusika na suala la mionzi.

Aidha, kituo hicho cha mpaka wa Namanga kipo katika mchakato wa kuteketeza mizigo mbalimbali ya aina ya kemikali ambayo imehifadhiwa baada ya kuonekana haifai kuingizwa nchini.

Mkaguzi Mfawidhi wa kemikali katika mpaka wa Namanga, Busigara Mkama, alisema sheria inamtaka mwagizaji wa mzigo wa kemikali lazima awe amesajili na kutambulika na Ofisi ya Mkemia Mkuu.

Alisema katika Januari, mwaka huu, kati ya mizigo ya kemikali 89 iliyokuwa inaingizwa nchini ni 87 ilikidhi vigezo, Februari kati ya mizigo 150 iliyokidhi vigezo ni 105 na katika mwezi uliopita kati ya mizigo 98 iliyokidhi vigezo ni mizigo 90.

Aidha, kwa upande wa mizigo ya vitenganishi, dawa, chakula na vipodozi inayopitia katika mpaka huo na kukaguliwa imeongezeka baada ya kuanzishwa na huduma za pamoja katika mpaka huo.

Mkaguzi Mfawidhi wa Mamlaka ya Dawa, Chakula na Vipodozi nchini, (TFDA), katika kituo cha Namanga, Elia Nyaura, alisema katika mizigo inayohusiana na vitendanishi, dawa, chakula na vipodozi iliongezeka kutoka 750 kwa mwaka 2016 na kufikia 1,060 kwa mwaka 2017, huku mwaka jana kukiwa na mizigo 1,220.

Nyaura alisema kutokana na huduma katika kituo hicho kuboreshwa mizigo iliyokamatwa ikiingizwa kupitia njia zisizokuwa halali ilipungua kutoka yenye thamani ya Sh. milioni 630 kwa mwaka 2015/16 na kufikia Sh. milioni 24 kwa mwaka wa fedha wa 2017/18.

"Hivi sasa tunafanya ukaguzi hapa mpakani Namanga kwa saa 24 ingawa bado elimu zaidi inahitajika kwa wafanyabiashara wanaoingiza nchini vyakula, dawa, vitenganishi na vipodozi," alisema.

# Wavuvi wapigwa msasa uvuvi bora na sheria

**Na Mwandishi Maalum,** MAFIA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amezindua mafunzo kwa wavuvi yenye lengo la kuzifahamu zana za uvuvi zinazoruhusiwa kwa mujibu wa sheria na kutambua fursa zilizopo katika sekta hiyo na hatimaye kuleta tija kwa maisha yao na ukuaji wa uchumi wa taifa.

Amesema licha ya Tanzania kuwa na eneo kubwa la uvuvi, katika kipindi cha mwaka 2016/17 Tanzania ilitumia Sh. bilioni 56 na mwaka 2017/18 imefikia Sh. Bilioni 150 kwa ajili ya kuagiza samaki kutoka nje ya nchi fursa ambayo ingetumiwa na wavuvi wa Tanzania kukuza uchumi wao.

Akizindua mafunzo hayo kitaifa kwa wavuvi katika mwalo wa Kilindoni, Mafia mkoani Pwani juzi, Waziri Mpina alisema kutokana na wavuvi wengi kukumbwa na changamoto nyingi, wizara yake imeanzisha mafunzo hayo ili kujenga uelewa wa pamoja na kuondoa kasoro zilizopo.

Mpina alisema pia watafundishwa juu ya matumizi ya zana bora za kisasa za uvuvi, namna ya kuandaa samaki na kuwahifadhi ili kupunguza hasara ya mavuno pamoja na fursa za masoko, utunzaji wa mazingira ili kulinda ikolojia na bioanuai zilizopo majini ili kuwa na uvuvi endelevu.

Pia alisema wavuvi watafundishwa namna ya kuanzisha vikundi vya wavuvi ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo, watafundishwa ufugaji wa samaki kwenye mabwawa na vizimba na biashara zingine mbadala ili kuongeza kipato na kupunguza nguvu ya uvuvi.

Aidha kwenye mafunzo hayo wavuvi watafundishwa kuzielewa Sheria za Uvuvi ikiwemo Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Namba 29 ya mwaka 1994 na Kanuni zake za mwaka 2009 pamoja na Sheria ya Bahari Kuu Cap 388 na Kanuni zake za mwaka 2007 na 2016 ili kufahamu kwa kina mambo yanayoruhusiwa na yasiyoruhusiwa.

Kutokana na mafunzo hayo, alisema watafahamu pia suala la urefu na uzito wa samaki anayeruhusiwa kuvuliwa, vipimo vya nyavu zinazoruhusiwa na taratibu nyingine kwa mujibu wa sheria ili kuepuka kuingia kwenye mkono wa sheria.

Waziri Mpina aliwahimiza wavuvi kote nchini kuchangamkia mafunzo hayo kwa kuwa ndiyo yatakuwa mkombozi kwao baada ya kwa sababu zaidi ya miaka 50 sasa walishindwa kunufaika na fursa za uvuvi kutokana na kutokuwa na elimu juu ya shughuli hiyo hivyo serikali imedhamiria kwa dhati kuwakomboa kutoka kwenye unyonge huo.

Mbali na uzinduzi huo wa mafunzo pia Waziri Mpina alikabidhi hundi ya Sh. milioni 153 iliyotolewa na Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu kama gawio kwa Halmashauri ya Mafia pamoja na kugawa mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya Kijiji cha Jimbo kisiwani humo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**CIVIL CASE NO. 16 OF 2017**
**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED.......................................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**PROMOTION OF RURAL INITIATIVES AND DEVELOPMENT ENTERPRISES LIMITED..........DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION**

**TO: PROMOTION OF RURAL INITIATIVES AND DEVELOPMENT ENTERPRISES LIMITED**
**P.O. Box 13900**
**ARUSHA.**

TAKE NOTICE that the above case has been fixed for mention in the High Court at Arusha on 30th day of April, 2019 at 09:00am in the forenoon.

YOU may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend you rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for mention, the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT THIS 20th day of March, 2019.**

115181302

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ATHUMANI BAKARI MAUYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 939 CBR TOYOTA GALA.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MAG/RB/1398/2019.**

115181402

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**APOSTOLOS VASILI VASILIKAKIS** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya ISUZU yenye namba za usajili T 512 AJR. Chassis namba 9911802. Engine namba. 487955.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**DOMR/TR/605/2019.**

115180602

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya piki piki aina ya BOXER yenye namba za usajili MC 377 BLW. Chassis namba MD2A21BZ2GWF96328. Engine PFZWGF14191. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/547/2019**

115180702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

### MAOMBI YA URAIA



**BW. AMAN PREET SHARMA**

**BW. AMAN PREET SHARMA** anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.Ni raia wa India na nchi atokayo ni India.yeyote mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa Afisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma,S.L.P 558.

215180302

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**MWANZA**
**RM.CIVIL CASE NO 22 OF 2019**
**MDAI.....................MUSSA JACKSON MAKARANGA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA........... 1. HAMADI ALLY SELEMAN@SELEYUM S/O MOHAMAED**
**MDAIWA...........2. MAYUNGA ALLY OMARY**

KWA: MAYUNGA ALLY OMARY,
MWANZA AU POPOTE ULIPO.

**WITO WA SHAURINI.**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba mdai ameleta madai dhidi yako nakala ya madai inapatikana katika mahakama hii.

Shauri limepangwa kutajwa mnamo tarehe 18 mwezi April, 2019 na unatakiwa kuleta utetezi wako na unatakiwa uwepo mahakamani au kuwasilishwa kisheria.

Zingatia kwamba kutofika siku hiyo shauri litapangwa tarehe ya kusikilizwa na maamuzi yatatolewa.

Imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii, leo tarehe 15 mwezi April, 2019.

215180202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: MANZESE/SINZA
Usimamizi wa Mirathi No. 83 /2019

Ombi la MUSSA SEIF ITANDULA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu MWAMVUA HASSAN KATALAMBULA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 29/4/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 29/4/2019

115180102


### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DAVIES JONATHAN KISAMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili T319 AFG,aina ya SUZUKI SAMURAI. Chasisi No. SJ70301412. Engine No.G13BA129450 .

Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu nae.
**OB/RB/3143/2019.**

115179802

### CHETI KIMEPOTEA



**IDDI M. NDALO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1263/0062** kilichotolewa na **MKUYU SECONDARY** mwaka 2013.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**STK/RB/3764/2019.**

115179102

### CHETI KIMEPOTEA



**JACQUELINE SIMON MBOGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1071/0094** kilichotolewa na ST.MATHEW SEC. SCHOOL mwaka 2008.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **WMB/RB/S149/19**

115180002

**THE UNITED NREPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA**
**AT ARUSHA**
**MISC. CIVIL APPLIC. CASE NO 112 OF 2018**
**TANELEC LIMITED PLAINTIFF/APPELLANT**
**VERSUS**
**USANGU LOGISTICS LTD& AM DEFENDANT/RESPONDENT**
**NOTICE FOR HEARING/MENTION**

**To ABDI MAHAMOUD**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/hearing in the Resident Magistrate court of Arusha at Arusha on the 2nd day of MAY 2019 at 08:30 a.m. o'clock in the forenoon.

You may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to reply in support of your case.

**TAKE FUTHER NOTICE** that in default of your appearance on that day and time before mention or hearing the court may proceed in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this 9th day of APRIL 2019.

215179502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 15/04/2019.

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI** tarehe 20/04/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka MOROGORO kuelekea LONGIDO gari hilo lenye namba za usajili: T188 **APK ,T741 CPB,T985 ABJ.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 17
   Upana –mita 3.0
   Kimo – mita 4.4

3. Njia itakayotumika **MOROGORO** hadi **LONGIDO** kupitia **MSATA ROAD** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

215179702


**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# JUVENTUS YAMTENGEA JOAO EURO MIL. 100

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imeripotiwa kuwa ina uwezekano wa kumuuza Paulo Dybala kipindi cha majira ya joto ili kupata fedha za kumnunua nyota wa Ureno, Joao Felix, ambaye kwa sasa anaichezea Benfica.

Felix mwenye umri wa miaka 19, ni mmoja wa vijana wenye vipaji vikubwa Ulaya ambapo anatabiriwa kuwa atakuwa nyota mkubwa kwa siku za usoni.

Amefunga mabao 16 na kutoa pasi za mwisho tisa katika mashindano yote, huku pia akifunga 'hat-trick' kwenye mchezo wa robo fainali ya Europa dhidi ya Eintracht Frankfurt wiki iliyopita.

Na alikuwa mhimili mkubwa wakati Benfica wakipata ushindi wa mabao 4-2 kwenye Ligi Kuu ya Ureno, Primeira Liga, dhidi ya Vitoria Setubal Jumapili.

Taarifa kupitia gazeti moja la Italia, zimebainisha kwamba, Juventus wapo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili Felix.

Na Gazeti la Ureno la O Jogo limeripoti kwamba, miamba hao wa Italia walitoa ofa ya euro milioni 75 ambazo tayari zimekataliwa na Rais wa Benfica, Luis Filipe Vieira.

Inaaminika kwamba Felix, ambaye alichezea kwa mara ya kwanza timu hiyo Agosti mwaka jana, thamani yake ni euro milioni 120.



# *Valverde kuibadilishia kikosi Man United leo*

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, anaweza kufanya mabadiliko kwenye mchezo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester United leo Jumanne.

Wakati kwenye mchezo wa kwanza ikiwa imeshinda bao 1-0 kwenye dimba la Old Trafford, miamba hao wa Catalunya watacheza leo katika dimba la Camp Nou.

Huku Lionel Messi, Luis Suarez na Gerard Pique wakitarajiwa kuwa kikosi cha kwanza, Gazeti la Mundo Deportivo limedai kwamba, Valverde pia anapanga kufanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi hcho.

Ripoti zinadai kwamba, Ousmane Dembele ambaye alirudi dimbani kwenye mchezo dhidi ya Huesca mwishoni mwa wiki, anaweza kurudi uwanjani, huku nyota wa zamani wa Liverpool, Philippe Coutinho ikianzia benchi.

Kwingineko kiwango cha Arturo Vidal kwenye safu ya kiungo katika mchezo wa Jumamosi kinaweza kumfanya akaanzia benchi, huku Arthur Melo akirudi katika kikosi cha kwanza.

# Sanchez, Matic kuivaa Barca



**MANCHESTER,** England

ALEXIS Sanchez na Nemanja Matic wamerudi kwenye kikosi cha Manchester United kwa ajili ya mchezo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona leo Jumanne.

Katika mchezo wa kwanza Luke Shaw aliwazawadia bao miamba hao wa Catalunya wakipata ushindi wa 1-0 kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Kurudi kwa wachezaji hao kumeimarisha matumaini ya Man United ya kupindua matokeo kwenye mchezo huo wa marudiano.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer alithibitisha baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya West Ham Jumamosi kuwa Sanchez atakuwa kwenye mchezo dhidi ya Barcelona baada ya kuwa majeruhi kwa muda mrefu.

Pamoja na Sanchez, Gazeti la Times pia limethibitisha kwamba mchezaji mwenzake, Matic anaweza kuwa fiti kwa ajili ya mchezo huo baada ya kupona nyama za paja.

Hata hivyo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia 'patina' wake katika kiungo, Ander Herrera bado ni majeruhi na hajasafiri kwenda Hispania.

Wote Sanchez na Matic walitajwa kwenye kikosi cha wachezaji 22 kilichosafiri kwenda Hispania, huku pia Matteo Darmian akijumuishwa kwenye kikosi hicho. Mchezaji wa kimataifa wa Chile, Sanchez hajawachezea 'Mashetani Wekundu' hao tangu alipotolewa nje baada ya kuumia goti kwenye mchezo wa ushindi wa 3-2 dhidi ya Southampton Machi 2.

HABARI MICHEZO

# Mbappe: PSG imecheza 'kitoto' kipigo cha 5-1




**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe ameshutumu kiwango cha Paris Saint-Germain, wakati ikifungwa mabao 5-1 mikononi mwa Lille, akibainisha kwamba mabingwa hao wa Ligue 1 walicheza kama wanajifunza.

Ulikuwa ni usiku usiosaulika kwa PSG ambayo ilimaliza ikiwa na wachezaji 10 ugenini dhidi ya Lille kwenye Uwanja wa Pierre-Mauroy, ambapo kama wangeshinda mchezo huo wangetangazwa kuwa mabingwa wapya.

Juan Bernat - ambaye alisawazisha baada ya bao la kujifunga la Thomas Meunier, alitolewa nje kipindi cha kwanza, ambapo tayari Meunier na Thiago Silva walikuwa wameshakumbwa na majeraha.

Na PSG ikakumbana na kichapo zaidi kwa mabao pengine kutoka kwa Nicolas Pepe, Jonathan Bamba, Gabriel na Jose Fonte, ambao mabingwa hao waliruhusu kufungwa mabao matano kwenye mchezo wa Ligue 1 kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2000.

Na nyota wa PSG, Mbappe aliiambiaCanal+: "Sisi ni wakubwa, hata tukifungwa, tufungwe hatuwezi kufungwa kwa staili ile.

"Huwezi kufungwa kwa staili kama ile, mabao manne, matano si sawa, hilo halingeweza kuwa sawa, timu ilicheza kama ndio inajifunza.

"Lille ni timu nzuri. Wana mashabiki wazuri na uwanja mzuri, lakini sisi hatukucheza kwenye kiwango chetu."

# DE GEA: MAN UTD IJIPANGE KWA BARCA



**MANCHESTER,** England

GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea, ameonya 'Mashetani Wekundu' hao kutakiwa kuimarika kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona.

United leo Jumanne itashuka dimbani ugenini kuivaa Barcelona, wakati ikiwa imefungwa bao 1-0 katika mchezo wa robo fanali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na juzi katika mchezo wa Ligi Kuu England, Man United iliibuka na ushindi dhidi ya West Ham na hivyo De Gea anaona kwamba wana nafasi nzuri ya kuimarisha kikosi chao.

Man United inayonolewa na kocha, Ole Gunnar Solskjaer ilipoteza mechi zake nne kati ya tano zilizopita kabla ya mchezo huo wa Jumamosi ambapo walishinda kwa bao la penalti ya dakika za majeruhi kupitia kwa Paul Pogba na kuweza kupata ushindi 2-1 dhidi ya West Ham katika Uwanja wa Trafford.

Na De Gea amesema kwamba wanatakiwa kuwa kwenye ari nzuri zaidi wakati wakishuka kwenye dimba la Camp Nou ili kuweza kupindua matokeo na kuibuka na ushindi.




# Klopp asifia kiwango cha Henderson

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesifia kiwango cha Jordan Henderson na uongozi wake baada ya nahodha huyo wa Liverpool kutoa mchango mkubwa wakati wakipata ushindi wa 2-0 dhidi ya Chelsea Jumapili.

Sadio Mane na Mohamed Salah wote walifunga na kuwawezesha vijana hao wa Anfield kurudi tena kileleni kwa msimamo wa Ligi Kuu.

Kiungo huyo raia wa Uingereza, Henderson alifanya kazi ya ziada kumtengenezea Mane aliyefunga bao la kwanza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alikuwa kwenye kiwango cha juu kwenye mchezo huo na hivyo, Klopp aliamua kumsifia.

"Nilishasema tangu nawasili hapa na mawazo yangu bado hayajabadilika, ni nahodha wa timu na anajua kuiongoza," alisema Klopp akiiambia Sky Sports.

"Ndani ya uwanja, yeye ni bora zaidi.

"Alicheza nafasi nyingi na nikalazimika kuendelea kumchezesha na ni mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi changu."

# DO A SOKA MAG A ULAYA




# SALAH AHESABU ZA UBINGWA LIVERPOOL

●●● Tunahitaji kutazama mechi zetu, tunatumai Man City itapoteza pointi, EPL ni kitu...

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL itatwaa ubingwa kama itashinda mechi nne za mwisho za Ligi Kuu England (EPL), kwa mujibu wa Mohamed Salah.

**Wekundu hao walirejea kileleni mwa msimamo wa EPL kufuatia ushindi wa mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Chelsea jana.**

Mabingwa watetezi, Manchester City mapema jana walikishusha kikosi hicho cha Jurgen Klopp kwa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Crystal Palace, lakini baada ya Sadio Mane kufunga kwa kichwa bao la kwanza katika dimba la Anfield, Salah alifunga kwa mkwaju wa mbali na kuihakikishia Liverpool pointi tatu, hivyo kurejea kileleni.

Liverpool kwa sasa inaongoza kwa pointi mbili zaidi ya City, ambayo ina mechi moja mkononi, lakini ikikabiliwa na mchezo mgumu ugenini dhidi ya mahasimu wao, Manchester United Aprili 24, mwaka huu.

Kikosi cha Klopp, kina mechi rahisi katika ratiba yake, ambapo kimebakiza mechi dhidi ya Cardiff City na Newcastle United ugenini wakati Huddersfield Town na Wolves zikiifuata Anfield.

Na Salah anaona kuvuna pointi katika mechi zote nne kutoka katika ratiba hiyo, zitakuwa zinatosha kuipa Liverpool ubingwa wao wa kwanza wa EPL katika kipindi cha miaka 10.

"Maoni yangu, ndiyo," Salah aliiambia Sky Sports wakati alipoulizwa kama anahisi kushinda mechi nne kunatosha kuipiku City.

"Tunahitaji kutazama katika mechi zetu. Tunatumai Man City itapoteza pointi. EPL ni kitu muhimu kwangu.

"Nitaifuatilia Man City kuona matokeo. Itasaidia na kuweza kutoa msukumo kwetu kufanya vizuri. Tutatazama zaidi katika mchezo wetu, lakini ninajua matokeo ya Man City [dhidi ya Palace]."

Salah alifikia mabao ya straika wa City, Sergio Aguero katika mbio za Kiatu cha Dahabu EPL kwa bao lake hilo dhidi ya Chelsea.

"Sikufikiria, nilijisikia tu," alisema akizungumzia bao lake hilo la 19 kwenye ligi msimu huu.

"Niliingia ndani na kawaida nilichia mkwaju kwa upande wa ndani wa mguu wangu, lakini hili ilikwenda kwa nguvu.

"Nilikuwa na bahati mpira ulijaa nyavuni kama vile."

## ZISIKUPITE

### DEMBELE AIVUTIA MAN UNITED

MANCHESTER United inavutiwa na mshambuliaji wa zamani wa Celtic anayeichezea Lyon kwa sasa, Moussa Dembele. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 22, ameshafunga mabao 18 msimu huu. ***(Mirror)***

### ALDERWEIRELD AWINDWA

ARSENAL inataka kumsajili beki wa Tottenham, Mbelgiji Toby Alderweireld, 30. ***(Talksport)***

### MADRID YAMTUPIA JICHO RICE

KIUNGO wa West Ham, Muingereza Declan Rice, 20, anawindwa na Real Madrid, kwa mujibu wa beki wa zamani, Scott Minto. ***(Stadium Astro, via Star)***

### ERIKSEN KUIGHARIMU SANA UTD

MANCHESTER United itapaswa kulipa pauni milioni 95 ili kumsajili kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, 27, ingawa nyota huyo wa kimataifa wa Denmark ameripotiwa anataka kujiunga na Real Madrid. ***(Express)***

### ICARDI KUACHANA NA INTER

MSHAMBULIAJI Muargentina Mauro Icardi anajiandaa kuondoka Inter Milan majira haya yote. Straika huyo mwenye umri wa miaka 26 anaweza kujiunga na Real Madrid kwa pauni milioni 52. ***(AS)***

### VARANE KAZI KUNG'OKA REAL

REAL Madrid itamruhusu Raphael Varane, kuondoka kama kiasi cha pauni milioni 437 zinazohitaji kuvunja mkataba wake zitalipwa. ***(RAI Sport via Calciomercato)***

### FERNANDES AKUSANYA VIGOGO

WAWAKILISHI kutoka Manchester United, Juventus na Paris St-Germain walikuwa Aves wakimtazama kiungo wa Sporting Lisbon, Mreno Bruno Fernandes, 24. ***(A Bola)***

### WERNER ANUKIA BAYERN, LIVER

LIVERPOOL na Bayern Munich zinamuwinda Timo Werner, 23, na habari nje ni kwamba hatasaini mkataba mpya na RB Leipzig. Mshambuliaji huyo raia wa Ujerumani atakuwa nje ya mkataba na miamba hiyo ya Bundesliga mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Germany)***

### CHELSEA, MADRID VITANI

CHELSEA itaingia vitani na Real Madrid kuwania saini ya mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Msweden Alexander Isak, 19. ***(Sun)***

### LUNDO KUPELEKWA SOKONI

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amesema klabu hiyo itauza wachezaji wake wenye thamani majira haya ya joto. Mfaransa huyo anataka kufanya mabadiliko makubwa baada ya kukatishwa tamaa kwenye msimu huu wa La Liga. ***(Sky Sports)***

### INTER NAYO YAMFUATA ERIKSEN

INTER Milan imefungua mazungumzo ya kumsajili Christian Eriksen, kwa pauni milioni 130, ambaye mkataba wake na Spurs unamalizika 2020. ***(Tuttosport, via Sun)***

### BAYERN YAMTAKA ZANIOLO

BAYERN Munich inavutiwa na kiungo wa Roma, Mtaliano Nicolo Zaniolo, 19. ***(Bild - in German)***

## HABARI MICHEZO

# Nigeria watamba kubeba ubingwa

Na Mwandishi Wetu

MAJIGAMBO na hali ya kujiamini imeanza kuonekana mapema kwa Kocha Mkuu wa timu ya Vijana ya Nigeria, Manu Garba, kwa kusema kuwa anakiamini kikosi chake kina uwezo wa kuchukua ubingwa wa fainali za Afrika za Vijana (Afcon U-17) mwaka huu zinazoendelea hapa nchini.

Nigeria ilianza kampeni za kuwania ubingwa wa michuano hiyo kwa ushindi wa mabao 5-4 dhidi ya wenyeji Tanzania (Serengeti Boys).

Garba alisema kuwa walifanya maandalizi ya muda mrefu na lengo lao ni kupata matokeo mazuri katika mechi zote watakazocheza katika michuano hiyo.

"Haikuwa kazi rahisi, tuliongoza mchezo na baadaye hali ilibadilika kwa kufungwa mabao ya haraka, ila walitulia na kuona kwamba hakuna kisichowezekana, kwa sababu muda bado ulikuwa unaruhusu," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa kiu kubwa waliyonayo ni kuchukua kombe hilo na si kufikiria kukata tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia kwa Vijana ambazo zitachezwa baadaye mwaka huu huko Brazil.

"Wachezaji wangu si wazuri sana, ila ninashukuru wanajitahidi kupambana, nusu ni wapya na wanashiriki kwa mara ya kwanza michuano hii, ila bado wanaonekana watatupa kile tunachokihitaji," alisema Garba.

Yosso hao wa Nigeria watashuka tena kucheza mechi yao ya pili kesho kwa kuwavaa Angola wakati wenyeji Serengeti Boys watachuana na Uganda.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 31 | 23 | 5 | 3 | 51 | 22 | 74 |
| 2. Azam | 30 | 18 | 9 | 3 | 48 | 18 | 63 |
| 3. Simba | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 5. Mtibwa Sugar | 31 | 13 | 6 | 12 | 32 | 24 | 45 |
| 6. KMC | 32 | 9 | 15 | 8 | 32 | 23 | 42 |
| 7. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 8. Coastal Union | 32 | 9 | 14 | 9 | 28 | 31 | 41 |
| 9. Singida Utd | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 10. Ndanda | 31 | 10 | 10 | 11 | 21 | 30 | 40 |
| 11. Mbao | 34 | 10 | 10 | 14 | 20 | 33 | 40 |
| 12. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 20 | 27 | 39 |
| 13. Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 14. Mbeya City | 30 | 10 | 7 | 13 | 30 | 33 | 37 |
| 15. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 16. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 24 | 34 | 37 |
| 17. Kagera Sugar | 32 | 8 | 12 | 12 | 26 | 34 | 36 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara Unite | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# KOCHA ATOA MSIMAMO KIPA SERENGETI BOYS

Na Somoe Ng'itu

LICHA ya kuonyesha uwezo mdogo, Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), Oscar Mirambo, amesema ataendelea kumtumia kipa Mwinyi Yahya, katika mechi ya pili ya mashindano ya Afrika (Afcon U-17).

Serengeti Boys ilikubali kichapo cha mabao 5-4 kutoka kwa yosso wenzao wa Nigeria katika mechi ya ufunguzi, lakini ilionekana mabao mawili kati ya hayo yaliyofungwa yalitokana na makosa binafsi ya Mwinyi.

Wenyeji hao wa fainali hizo zinazofanyika kwa mara ya kwanza hapa nchini, Serengeti Boys watashuka tena uwanjani kesho kuwakabili Uganda kuanzia saa 1:00 usiku wakati mapema saa 10:00 katika Kundi A, Angola watavaana na Nigeria.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mirambo, alisema kufanya uamuzi wa kumbadilisha golikipa hautakuwa wa kujenga na kitakachofanyika ni kurekebisha makosa yaliyojitokeza na hapo ndio watakuwa wamefanikiwa 'kutibu tatizo'.**

Mirambo alisema mechi hiyo ilikuwa ni ngumu na kitendo cha kufanikiwa kupata mabao mawili ya haraka baada ya kuanza kwa kipindi cha pili ni cha kujivunia, kwa sababu ilionekana wachezaji wake wameelewa mawaidha waliyopewa wakati wa mapumziko.

"Nafasi bado ipo, tumemaliza mechi ya Nigeria, tuna michezo miwili mkononi, tutaimarisha nidhamu mchezoni, tunajifunza kutokana na makosa, ni wazi kuwa suala la golikipa ni changamoto," alisema kocha huyo.

Leo ni mapumziko na mechi nyingine za fainali hizo za Kundi B zitachezwa keshokutwa kwa Cameroon kuwakabili Morocco wakati Senegal watawavaa Guinea kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akikabidhi Kitambulisho cha Klabu ya Waogeleaji Tanzania kwa Bingwa wa Waogeleaji nchini, Hilal Hemed Hilal katika mashindano ya 12 ya Klabu ya Waogeleaji Tanzania yaliyodhaminiwa na Benki ya DTB-Tanzania. Mashindano hayo yalifanyika Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST), Upanga jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Wasichana wang'ara mbio Standard Chartered*

Na Mwandishi Wetu

WASICHANA walioshiriki mradi wa Goal Initiatives wamenogesha mbio za Benki ya Standard Chartered zilizofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Katika mbio hizo zilizozinduliwa na Balozi wa China nchini Tanzania, Wang Ke, walishiriki pia wasichana kutoka kwenye mradi wa Goal Initiatives, ambao waliongeza chachu na kuzinogesha mbio hizo za kilometa kumi.

Mbio hizo zijulikanazo kama 'Standard Chartered Belt and Relay' ziliwashirikirikisha pia wafanyakazi kutoka ubalozi wa China, wafanyakazi wa benki hiyo na wanariadha wengine kutoka jijini Dar es Salaam wakiwamo wanaoshiriki mbio za kimataifa.



Katika mbio hizo, wasichana hao waling'ara kwa kushinda nafasi tatu za juu kwa upande wa wanawake walioshiriki.

Mshindi wa kwanza alikuwa ni Asia Rambo, akifuatiwa na Zainab Tweve, huku Donata Charles akishika nafasi ya tatu na wote walikabidhiwa medali. Kwa upande wa wanaume, mshindi alikuwa Lin Xtaoping, nafasi ya pili Antony Silayo na wa tatu Hui Feng na kukabidhiwa medali.

Kwa washindi wa jumla nafasi ya kwanza ilichukuliwa na Henry Li, ya pili ikaenda kwa Henry Kambugu na wa tatu ni Jack Messen na wote walikabidhiwa medali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, alielezea furaha yake kuona mbio hizo na kwamba mkakati wao ni kuitangaza Tanzania kupitia uwekezaji.

Alisema mbio hizo zinalenga pia kukuza uhusiano wa kibiashara baina ya wafanyabiashara wa kutoka nchini China na Tanzania.

Washiriki wengine wa kimataifa walioshiriki mbio hizo ni pamoja na Therese Neo (Singapore), Danny Chang (Malaysia), Serena Leung (Hong Kong), Dina Elessaway (Dubai), Lynsey McGarry (Marekani), huku timu hiyo ya wakimbiaji wa kimataifa ikiongozwa na Selina Donald kutoka nchini Uingereza.

# Michezo

Jumanne Aprili 16, 2019

Nipashe



Salah ahesabu za ubingwa Liverpool UKURASA 30



Mohamed Salah (katikati), akishangilia kwa staili mpya baada ya kuachia mkwaju wa takriban yadi 30 uliojaa moja kwa moja nyavuni na kuiandikia Liverpool bao la pili wakati ikishinda 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi. **HABARI UK. 30**

## Kocha atoa msimamo kipa Serengeti Boys

**Na Somoe Ng'itu**

LICHA ya kuonyesha uwezo mdogo, Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), Oscar Mirambo, amesema...



HABARI UK.31

## De Gea: Man Utd ijipange kwa Barca

**MANCHESTER,** England

GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea, amewaonya 'Mashetani Wekundu' hao kutakiwa kuimarika kwenye mchezo wa marudiano...



HABARI UK.29

# Simba, Yanga zatangaza vita

## ●●● Coastal, Mtibwa Sugar kazi wanayo kesho Mkwakwani na Jamhuri, makocha wasema...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kikiwasili salama jijini Tanga jana mchana tayari kuwavaa wenyeji wao Coastal Union katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa kesho Jumatano kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani, watani zao Yanga wamesema hawakamatiki na wamejipanga kuidunda Mtibwa Sugar siku hiyo.

**Hata hivyo, Simba ambayo Jumamosi iliyopita walitolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imetua Tanga bila nyota wake watatu wa kimataifa ambao ni majeruhi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliwataja wachezaji hao ambao ni majeruhi ni pamoja na kiungo James Kotei, mabeki, Juuko Murshid na Paschal Wawa.

Rweyemamu alisema kuwa Kotei na Juuko waliumia katika mechi ya marudiano dhidi ya TP Mazembe wakati Wawa yeye aliumia katika mechi ya kwanza iliyochezwa hapa nchini na kumalizika kwa sare ya bila kufungana.

"Tumeshafika Tanga, mechi ni Jumatano, lakini tumeamua kuja mapema kwa sababu ya kufanya mazoezi kwa utulivu, tunajua huu mchezo utakuwa mgumu kama mechi nyingine ambazo tumeshacheza za ligi, Simba ina malengo yake na wenzetu pia wana malengo yao," alisema Rweyemamu.

Meneja huyo aliongeza kuwa benchi la ufundi la timu hiyo lililoko chini ya Mbelgiji Patrick Aussems linajipanga kuandaa kikosi kitakachoshuka dimbani kwenda kulingana na wachezaji watakaokuwa tayari kwa mechi hiyo.

Taarifa kutoka Tanga zinaeleza kuwa kikosi cha Coastal Union kimekwenda Pangani kuweka kambi maalumu kwa ajili ya kujiandaa na mchezo.

Pia taarifa zaidi zimeeleza kuwa timu hiyo huenda ikapata motisha kutoka kwa wafadhili wao endapo itafanikiwa kuondoka na ushindi kwenye mechi hiyo.

Baada ya mechi hiyo ya kesho, Simba yenye pointi 57 ikiwa imecheza mechi 22, itasafiri kuelekea mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kucheza mechi nne dhidi ya Kagera Sugar, Alliance FC, KMC na Biashara United, ambazo zitachezwa ndani ya siku nane.

Kwa upande wa Yanga, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mwinyi Zahera, amesema wamejipanga kuhakikisha wanashinda mechi yao ya kesho dhidi ya Mtibwa Sugar na hakuna timu ambayo itawasimamisha kwenye mbio zao za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Mchezo huo wa raundi ya 32 kati ya Mtibwa Sugar dhidi ya Yanga utachezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro kuanzia saa 10:00 jioni.

Zahera alisema wachezaji wake wanajua malengo waliyokuwa nayo na wanaamini kutwaa ubingwa ndiyo kutawaweka katika nafasi nzuri ya maandalizi ya msimu mpya.

"Sijaona timu ambayo inaweza kutusumbua kama wachezaji wangu watafanya kile ninachowaelekeza, hakuna mechi ngumu, ila kuna ushindani kwenye ligi, tumefaulu kwa kushinda mechi zilizopita, na zilizoko mbele yetu pia tutahakikisha tunashinda, hayo ndiyo malengo yetu," alisema kocha huyo.

Naye Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kuwa wachezaji wote wako katika hali nzuri na jana jioni walitarajiwa kufanya mazoezi kwenye Uwanja wa Jamhuri akiwamo nahodha wao, Ibrahim Ajibu.

"Tutamkosa Yondani (Kelvin) kutokana na kadi nyekundu aliyopewa, Ninja (Shaibu) alishamaliza adhabu yake, Ajibu naye yuko fiti, mashabiki wetu watarajie kuona kiwango bora," alisema meneja huyo.

Yanga wenye pointi 74 ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakati African Lyon ambao wamecheza mechi 33, wanaburuza mkia wakiwa na pointi 22.